Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 18 Julai, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA AFYA (K.n.y.WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Shirika la Nyumba la Taifa kwa Mwaka 2002/2003 *(The Annual Report and Accounts of the National Housing Corporation for the year 2002/2003)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo kwa Mwaka Ulioishia tarehe 30 Juni, 2003 *(The Annual Report and Accounts of Small Industries Development Organisation (SIDO) for the year ended 30th June, 2003.*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006

**MHE. LUCAS L. SELELII (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA):**

Maoni ya Kamati ya Maliasili na Mazingira Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni yake Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 274

### Ruaha Kidodi Kuwa Mji Mdogo

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO (K.n.y. MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mji wa Ruaha Kidodi umekua sana na una hadhi ya kuwa Mji Mdogo sasa:

Je, ni lini Mji huo utapandishwa hadhi na kuwa Mji Mdogo Ruaha?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christopher Semanini Wegga, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya hatua muhimu ya kupandisha hadhi ya Kijiji au eneo la Makazi kuwa Mji Mdogo ni kuomba Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Kijiji au eneo hilo kutangazwa kuwa "*Planning Area*" chini ya kifungu 13 cha Sheria ya Mipango Miji sura ya 378. Hata hivyo maombi hayo sharti yaambatane na maamuzi ya vikao vya Kata na Halmashauri na michoro ya mipaka. Hatua ya pili ni kuangalia iwapo vigezo muhimu vinavyofanya eneo kuwa Mji Mdogo vimetimizwa. Vigezo hivyo ni pamoja na idadi ya wakazi wasiopungua 9,000. Kata, uwakilishi wa Udiwani, mapato ya Mji mdogo kwa mwaka, pato la mkazi kwa mwaka, huduma za kijamii na uchumi na

eneo lisilopungua kilomita za mraba 2,580. Kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Wilaya) Na. 7 ya mwaka 1982 kifungu Na. 27 aya ya 2 iliyorekebishwa na Sheria Na. 6 ya mwaka 1999, Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa baada ya kuridhika na sifa za eneo na kukamilika kwa taratibu za Sera ya Maendeleo ya Makazi Mijini, anaweza kulitangaza eneo hilo kuwa Mji Mdogo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutangazwa kuwa Mji Mdogo, Mji huo utakuwa na Mamlaka ya kujiendesha na kukusanya kodi na kupata ruzuku kutoka Halmashauri husika. Napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge kuwa vigezo na masharti niliyoyataja kwa eneo la Ruaha Kidodi yatimizwe ili ipate hadhi ya kuwa Mji Mdogo.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa hivi karibuni wakati Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI akisoma hotuba yake ya Bajeti alitamka kwamba kuna miji zaidi ya 80 ambayo imepandishwa hadhi vijiji kuwa Halmashauri ya Miji Midogo. Je, kwa nini wasitangaze kwenye gazeti la Serikali ili miji iweze kufahamu kwamba sasa ni Miji Midogo na sio vijiji kama vile Mpwapwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika hotuba yetu ya Bajeti Waziri alitangaza baadhi ya vijiji kuwa Miji Midogo pamoja na kijiji cha Mpwapwa. Sasa hiyo ilikuwa ni hatua ya kwanza ya kuarifu tu umma ujue kwamba Waziri amechukua hiyo hatua. Kwa hiyo, hatua ya pili itakuwa ni kurasimisha kisheria kwa vijiji hivyo kutangazwa rasmi katika gazeti la Serikali.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niulize swali dogo moja la nyongeza.

Kwa kuwa Miji Midogo ya Kongwa, Kibaigwa, Mlali na Mkoka katika Wilaya ya Kongwa tayari imerasimishwa kisheria. Lakini bado utaratibu wa kuwa na uongozi wa kimamlaka ya Mji Mdogo kuwezeshwa kukusanya kodi na kupata ruzuku haujaanza. Si kwa miji hiyo tu bali kwa Miji Midogo yote nchi nzima. Swali langu je, ni lini miji hii midogo itakuwa na mamlaka zake za kuweza kujiendesha kikamilifu tofauti na hali ilivyo sasa ambavyo inaendeshwa kama Serikali za Vijiji?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya vijiji ambavyo vilishakamilishiwa taratibu za kuwa Miji Midogo. Sasa hivi kinachofanywa ni maandalizi tu kwa sababu kuwa Mji Mdogo maana yake lazima uwe na wafanyakazi watakaohudumia hiyo Mamlaka ya Mji Mdogo, lazima uwe na vyanzo vya mapato vitakavyokusanywa na huo Mji Mdogo, yako maandalizi mengi. Kwa hiyo, ndiyo maana hayo maandalizi yanafanywa yakishakamilika basi mtaanza kupata ruzuku na kuwa na Serikali ya Mji Mdogo.Tuwe na subira maandalizi yakamilike.

Na. 275

**Ruzuku Katika Mbolea**

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi karibuni Serikali ilikubali hoja muhimu ya kuweka ruzuku katika mbolea za aina mbalimbali hapa nchini:-

(a) Je, ni kiasi gani cha mbolea yenye ruzuku ya Serikali kilipelekwa katika Wilaya ya Hai?

(b) Katika kiasi hicho kilichopelekwa Hai. Je, ni kiasi gani kilipelekwa katika Jimbo la Siha na kilipitishwa kwa Mawakala gani au Taasisi zipi ili kuwafikia wakulima?

(c) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuongeza kiasi hicho ili kila mkulima aweze kupata nafuu hiyo na kuongeza kiasi cha chakula nchini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Chakula, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Deaisile Joshua Mwanri, Mbunge wa Siha, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Katika msimu wa 2004/2005, Mkoa wa Kilimanjaro ulipangiwa kupatiwa jumla ya tani 3,242 za mbolea ya ruzuku, ambapo Wilaya ya Hai ilikuwa imepangiwa kupatiwa tani 1,742. Hadi tarehe 26 Juni, 2005, mbolea iliyopelekwa Mkoani Kilimanjaro ilikuwa tani 944.9. Kiasi kilichopelekwa katika Mkoa wa Kilimanjaro ni kidogo ikilinganishwa na mpango kwa sababu wakulima wa Mkoa wa Kilimanjaro walipendelea kutumia mbolea aina ya *Urea* kwa wingi ambayo ilikuwa na fidia kubwa na hivyo kutumia kiasi kikubwa cha fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mkoa. Kiasi cha tani 786 za *Urea* zilifidiwa na kusafirishwa kwenda Kilimanjaro, badala ya tani 469 zilizopangwa. Mbolea nyingine zilizofidiwa na kusambazwa katika Mkoa wa Kilimanjaro ni *DAP* tani 80.7 na *CAN* tani 78.2. Kiasi cha mbolea iliyopelekwa katika Wilaya ya Hai kilikuwa ni tani 289.5.

(b) Katika mbolea iliyopelekwa Wilaya ya Hai, iliyouzwa katika jimbo la Siha ilikuwa tani 135.0 na jimbo la Hai ilikuwa tani 154.5 Mawakala walioshiriki katika kusambaza mbolea yenye ruzuku katika jimbo la Siha walikuwa *Doladae Enterprises*, MUVIMAHA na Karansi *R.C.S.* Mawakala hawa waliteuliwa na Kamati ya Mbolea ya Ruzuku ya Wilaya ya Hai katika kikao chake cha tarehe 23 Februari, 2005.

(c) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2005/2006, Serikali itaongeza kiasi cha mbolea ya ruzuku kwa nchi nzima. Kufuatia ongezeko hilo, Wilaya ya Hai nayo

itaongezewa kiasi cha mbolea ya ruzuku itakayosafirishwa na kusambazwa Wilayani humo. Lengo ni kuhakikisha kuwa kila mkulima anapata nafuu hiyo ya ruzuku ya mbolea na hivyo kuongeza kiasi cha uzalishaji wa mazao nchini.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Namshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa. Kwa kuwa wananchi wa jimbo la Siha wanategemea zaidi ushirika na ushirika ndicho chombo ambacho wanakitumia sana katika masuala haya ya mazao na mambo mengine yoyote yanayohusiana na zao la kahawa, mahindi na kila kitu. Je, Serikali haioni kwamba ni vizuri sasa ikatumia utaratibu wa ushirika kuhakikisha kwamba mbolea hizi zinazosambazwa kwa wananchi kupitia ushirika?

Pili, ni wazi kabisa kwamba katika jimbo la Siha na Wilaya ya Hai na Mkoa wa Kilimanjaro kwa ujumla wake *Urea* imeonekana kwamba inafanya vizuri zaidi kuliko mbolea nyingine zozote. Anazungumzia habari ya mpango hapa ni kwa nini mpango huo haukuona kwamba kinachotengwa ni *Urea* na sio zile nyingine anazozungumza ili kazi hii ya kuongeza chakula katika nchi yetu iweze kufanyika kama ilivyokusudiwa na Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nchi ya Tanzania hutegemea sana shughuli zake za kilimo kupitia ushirika.

Aidha, tukumbuke kuwa wanaofanya utaratibu wa kuchagua Wakala ni Kamati inayoshughulikia masuala ya Ruzuku ya Wilaya huko Wilayani alikotoka Mheshimiwa. Kwa bahati nzuri sisi Wabunge wote hata mimi kwenye Wilaya yangu ni Mjumbe wa Kamati hizo. Kwa hivi ushauri wangu ni kuwa akitaka kutumia sana ushirika, sio Wizara ya Kilimo isukumize suala lakini namwomba Mheshimiwa aliibue suala hilo katika Kamati yake kusudi ushirika ushirikishwe na mambo yakamilike. Kwa sababu *ultimately* anayewajibika na kusambaza mbolea hii ni Kamati hii ya Ruzuku ya Wilaya ambaye sisi Wabunge ni Wajumbe.

Pili, ni kweli *Urea* ilionekana inapendwa sana kuliko aina nyingine ya mbolea. Hapo nina maelezo mawili. Kwanza zile aina kama *DAP* ni nzuri sana kwa kupandia halafu *Urea* ni kwa kukuzia. Kwa hiyo, ndiyo maana Wizara iliona ni busara kupeleka mbolea zote za aina hizo kusudi ifanye kazi zile zinazotakiwa kufanywa kitaalamu. Sasa kama wao wanaona nyingine hawahitaji ya kupandia basi maamuzi ni ya huko. Kamati itoe mapendekezo ilivyo. Lakini ushauri wangu *Urea* ina nafasi yake katika kuzalisha mahindi na mazao mengine hasa mahindi, mpunga na kadhalika.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Ningependa kuuliza maswali madogo ya nyongeza.

Moja je, si vizuri Wizara ikaamua kutoa mbolea ya ruzuku kwa mwaka mzima badala ya utaratibu wa sasa ambapo wanaishia mwezi Machi na kufanya wafanyabiashara kuficha mbolea kwa visingizio kwamba hiyo sio mbolea iliyopangwa na Serikali? Pili, si vizuri Serikali ikaamua kuwa na ratiba ya usambazaji wa mbolea hii kwa mwaka mzima ili kuzingatia tofauti za kimazingira katika nchi?

**SPIKA:** Unaruhusiwa swali moja tu lakini yamekuwa mawili. Sio neno ni mwaka wa Uchaguzi Mheshimiwa Naibu Waziri jibu? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Wizara ilipenda sana kutoa mbolea kwa mwaka mzima. Lakini kwa bahati mbaya matumizi ni mengi sana kuliko upatikanaji wake. Hii itawezekana tu wakati mpango unaoandaliwa sasa wa kutoa mbolea nyingine kutoka Uholanzi labda hapo tunaweza kufikiria. Lakini mpaka hapo itakapoonekana mbolea iko nyingi sana itakuwa vigumu kutoa kwa mwaka mzima. Ila ushauri wangu ni kuwa ni vizuri Kamati iwafahamu Mawakala wale na kukagua wanakoweka hizi mbolea. Akisema imekwisha, wajue kweli imekwisha. Maana ukiona *inventory* imeingia kiasi fulani na anayepata ni nani na ukafuatilia unaweza kujua utapeli wa aina hiyo.

Pili, ratiba kama nilivyosema tunaweza kuwa na ratiba kama tukiwa na mbolea nyingi iliyofurika. Kwa sasa bado tunadunduliza kwa sababu inaletwa chache kulingana na Bajeti yetu kama ulivyosikia wakati wa kuwasilisha Makisio yetu mwezi Juni, 2005.

Na. 276

**Zao la Ufuta**

**MHE. ARIDI M. ULEDI (K.n.y. MHE. MARIA D. WATONDOHA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, zao la Ufuta ni mojawapo ya zao la biashara linaloipatia nchi yetu fedha za kigeni; na kwa kuwa, Mkoa wa Lindi na Mtwara ni miongoni mwa Mikoa inayolima zao hilo:-

(a) Je, kuanzia msimu wa mwaka 2000 hadi 2002 ni kiasi gani cha ufuta kimezalishwa katika mikoa hiyo?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha za kigeni kimepatikana?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza zao hilo na kubaini mazao mengine ya biashara zaidi ya Ufuta na Korosho katika mikoa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Chakula, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Watondoha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kati ya mwaka wa 2000 na 2002, jumla ya tani 111,513 za ufuta zilizalishwa katika Mikoa ya Mtwara na Lindi, ikiwa ni sawa na asilimia 69 ya ufuta uliozalishwa

kwa nchi nzima. Uzalishaji wa ufuta katika Mkoa wa Mtwara ulikuwa tani 60,844 na Mkoa wa Lindi ulikuwa tani 50,669.

(b) Kati ya mwaka wa 2000 na 2002, nchi yetu iliuza nje kilo 45,364,771 (sawa na tani 45,365) za ufuta na kuingiza *USD. 18.8* milioni. Kati ya kiasi hicho, kilo 16,715,667 zilizokuwa na thamani ya *USD 6.9* milioni, zilitoka Mtwara na kilo 13,920,288 zilizokuwa na thamani ya *USD. 5.8* milioni zilizotoka Lindi.

(c) Kituo cha Utafiti wa Naliendele kilichopo Mtwara, kinafanya utafiti wa mazao mbalimbali yanayoweza kustawi katika Mikoa ya Mtwara na Lindi, ikiwa ni pamoja na ufuta. Hadi sasa kituo kimekwishatoa aina tatu mpya za mbegu za ufuta ambazo ni Ziada 94, Naliendele 92 na Zawadi 94. Mazao mengine yaliyotafitiwa na kuonekana yanafaa kulimwa katika Mikoa hiyo ni karanga, michikichi, mihogo na maembe. Halmashauri za Wilaya za Mikoa ya Lindi na Mtwara zinashauriwa kuamua ni mazao gani wananchi wangependa kuyapa kipaumbele na kisha kuandaa mipango ya kuyaendeleza ambapo itatengwa fedha kwenye Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa imeonekana kuwa zao la ufuta linawapatia kipato kikubwa zaidi wananchi na Taifa je, Serikali sasa itakuwa tayari kuunda Mamlaka Maalum ambayo itasimamia zao hili la ufuta ili kuliendeleza? Swali la pili, kwa kuwa wakulima wengi wanaolima zao hili la ufuta wanakabiliwa na tatizo la soko. Je, Serikali sasa itakuwa na utaratibu gani wa kutatua tatizo hili la soko kwa wakulima hasa wale walioko vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli zao la ufuta lina kipato kikubwa. Lakini si zao pekee lenye kipato katika mkoa ule. Kwa taarifa Serikali inaandaa rasimu ya kuwa na Bodi ya Mazao mchanganyiko ikijumuishwa na hili. Kwa hiyo naomba subira kwa Mheshimiwa Mbunge ufumbuzi utapatikana hivi karibuni. Wakulima wanakabiliwa na tatizo la soko. Mheshimiwa Uledi si kweli kuwa wanakabiliwa sana na tatizo la soko. Kwa sababu haya mamilioni ya dola yamepatikana kwa soko hili hili unalosema lina matatizo. Kwa hivi mimi nafikiri tu tunaweza kuboresha tutakapokuwa na Bodi lakini tatizo hasa halipo ufuta unatakiwa sana.Kupitia Bunge lako Tukufu nataka kuwaambia wafanyabiashara wote nchini ufuta unapatikana kwa wingi Mtwara na Lindi. *(Makofi)*

Na. 277

**Ujenzi wa *Hostel***

**MHE. LEONARD M. SHANGO( K.n.y. MHE. DIANA M. CHILOLO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Shule za Sekondari zilizojengwa kwa nguvu za wananchi nchini zikiwemo zile za Mkoa wa Singida, nyingi hazina hosteli hasa kwa ajili ya wasichana na wavulana, kama vile Shule ya Sekondari za Shelui, Kibaya, Kizaga, Puma na kadhalika;

na kwa kuwa mpango wa MMES umeanzishwa baada ya mafanikio makubwa ya MMEM:-

Je, ndani ya mpango wa MMES kutakuwa na ujenzi wa hosteli ili kusaidia kupunguza tatizo la mimba kwa wanafunzi wa kike na nidhamu kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Utamaduni, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) ni mpango wa miaka mitano kuanzia mwaka 2004 – 2009 una lengo la kuboresha na kuongeza nafasi za Sekondari *(Improvement of Access)* kufikia 50% ya rika lengwa yaani watoto wa miaka 14 – 17 ya wahitimu wa darasa la Saba na asilimia 50% ya wahitimu wa Kidato cha 4 kujiunga na Kidato cha 5 kila mwaka ifikapo mwaka 2010. Ili kufikia lengo hilo MMES unatoa Ruzuku ya Maendeleo ya Ujenzi wa Shule mpya 1,500 kwa nchi nzima za kutwa zinazotakiwa kujengwa katika kipindi cha mpango na pia kukarabati na kuongeza nafasi katika shule zilizopo na kutoa Ruzuku ya Uendeshaji wa Shule.

Aidha, ndani ya MMES, upo mkakati wa kusaidia ujenzi wa Hosteli kwa kulipia vifaa vya ujenzi, vinavyotengenezwa Viwandani kama vile mabati, saruji, nondo, misumari, rangi ya vioo vya madirisha. Lakini kutokana na idadi hiyo ya Shule za Sekondari zinazotakiwa kujengwa ni dhahiri kuwa ujenzi wa hosteli utazingatiwa katika baadhi ya maeneo hususan ya wafugaji na pale itakapoonekana upo umuhimu wa lazima wa kujenga hosteli.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa wanafunzi wasichana wanapopanga kwenye majumba ya watu binafsi wananyanyaswa sana. Je, Serikali haioni kuwa ni wakati kuwa masharti ya kufungua shule hizi iwe ni pamoja na kuwa na hosteli za wasichana katika hizi Shule za Sekondari za Kutwa?

Pili, kwa kuwa unyanyasaji huu ni wa kijinsia na wakati mwingine wanawapunguzia nafasi wanafunzi kuendelea kwa ajili ya usumbufu wanaopata katika upangaji wao. Je, Serikali haioni ni wakati muafaka kutunga Sheria Maalum kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapopanga kwa majumba ya watu binafsi wasinyanyaswe na kama wakinyanyaswa wale wanaowanyanyasa wachukuliwe hatua za kisheria za kutosha kabisa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali au Wizara ya Elimu na Utamaduni iweke masharti kwamba kila kwenye Shule ya Sekondari pawepo na hosteli.

Mheshimiwa Spika, hizi shule zinazojengwa sasa hivi ni Shule za Kutwa na zinatakiwa zijengwe katika eneo jirani na wanafunzi walipo. Ndiyo maana sasa hivi tunakwenda mpaka kwenye Kata ili Shule ya Sekondari iwe karibu, watoto watoke nyumbani waende shule na kurudi nyumbani.

Sasa tuweke masharti lazima kila shule ya namna hiyo iwe na hosteli sio sahihi. Isipokuwa wazazi wenyewe wakiona kuna umuhimu wa kujenga hosteli kama nilivyosema katika jibu letu la msingi upo utaratibu wa kuwasaidia kama hilo hitaji litakuwepo.

Kuhusu kutunga Sheria Maalum ya Kuzuia Unyanyasaji wa Wasichana. Nataka kusema kwamba kwa kweli sheria zilizopo zinatosheleza kabisa na tena kali sana. Sheria iliyopo sasa hivi ya Makosa ya Kujamiiana ina vipengele vyote kabisa hata kumshika tu msichana hata kumkonyeza yaani sheria kali kweli.

Kwa hiyo hakuna tena haja ya kutunga nyingine. Nataka kutoa wito tu kwa Watanzania wenzangu popote pale tulipo tuwape nafasi wasichana waweze kuanza Kidato cha Kwanza hadi cha Sita mpaka Chuo Kikuu bila kuwanyanyasa na bila kuwasumbuasumbua tunataka wasichana nao vile vile wasome.

Mheshimiwa Spika, ikitokea tatizo la unyanyasaji sheria kali ipo na kifungo chake ni miaka 30 ya kunyanyasa msichana.

Na. 278

**Vitambulisho Vya Uraia**

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD (K.n.y. MHE. PONSIANO D. NYAMI)** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi za Zambia, Afrika ya Kusini, Rwanda na Kenya zimefanikiwa kutoa vitambulisho vya uraia kwa wananchi wao wote:-

(a) Je, ni kwanini Tanzania haitaki kutekeleza zoezi hilo la utoaji wa vitambulisho vya uraia?

(b) Je, kwanini wahusika katika nchi yetu wasipelekwe kujifunza kwenye hizo nchi zilizofanikiwa katika zoezi hilo?

(c) Je, vitambulisho hivyo vitatolewa lini hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Nyami Mbunge wa Nkasi lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kutoa vitambulisho vya uraia na inayo nia thabiti kabisa ya kuanza kutekeleza mradi huu mapema iwezekanavyo. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeanza mchakato wa maandalizi ya mradi huu. Kwa sasa zoezi hili liko hatua ya upembuzi yakinifu yaani *feasibility study* Baada ya hatua hiyo kukamilika, itafuata hatua ya kutangaza tenda ili makapuni yenye uwezo na uzoefu katika fani hii yajitokeze na atakayeshinda tenda hiyo atapatiwa kazi ya kutengeneza vitambulisho hivyo. Hatua hii itachukua muda wa kati ya miezi sita hadi tisa.

Mheshimiwa Spika katika kutilia maanani jambo hili, Serikali katika Bajeti yake ya mwaka 2004/2005 ilitenga shilingi milioni 700, na mwaka huu wa fedha hii bajeti mliyoipitisha juzi 2005/2006, Serikali imetenga shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya maandalizi ya awali ya mradi huu wa kutoa vitambulisho vya uraia.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kutoa vitambulisho vya uraia ni mkubwa, na utagharimu kiasi kikubwa sana cha fedha, hivyo ni lazima uandaliwe kwa makini na utekelezwe kwa makini. Tutawaomba wananchi wawe na subira na tunawahakikishia Watanzania kwamba watapata kitu bora na chenye kiwango cha kimataifa.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni kwamba hiki kilio kipo siku nyingi cha Watanzania kutaka vitambulisho ili kuwa na haki yao kujijua kama ni Watanzania na hawana tofauti na watu wengine. Je, uharaka huu lini utakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba vitambulisho ni haki ya kila Mtanzania awe nacho maana ndicho kinachomtambulisha popote pale kwamba yeye ni Mtanzania. Tunajua vilevile kwamba Watanzania wanayohamu kubwa sana ya kuwa na vitambulisho hivyo lakini kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba huu ni mradi mkubwa sana na utagharimu mabilioni ya fedha si chini ya bilioni 100.

Kwa hiyo, ni vizuri katika kuanza kutekeleza mradi mkubwa kiasi hiki tujipe muda wa kufanya huo upembuzi yakinifu ukishakamilika tenda itatangazwa. Kwa hiyo siwezi kusema kwamba uharaka huu ni wa kesho au kesho kutwa, lakini mchakato mzima umeshaanza nataka niwahakikishie Watanzania kwamba suala la vitambulisho tuko makini sana katika Serikali na vitapatikana muda si mrefu sana.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Sheria iliyopitishwa mwaka 1987 ya kuanzishwa kwa vitambulisho vya uraia ilihusu Watanzania wote na kwa kuwa hivi sasa Zanzibar wanatoa vitambulisho vya uraia je, Tanzania tumekuwa na uraia wa aina mbili ule wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ule wa Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, uraia ni suala la Muungano kwa hiyo wananchi wa Bara na wananchi wa Visiwani katika suala la uraia wote uraia wetu ni mmoja ni Watanzania. (*Makofi*)

Kinachofanyika sasa hivi Zanzibar si kwamba wanapewa vitambulishop vya uraia, kule Zanzibar wanapewa vitambulisho vya ukazi,yule ambaye ni mkazi wa Zanzibar ndiyo anapata hicho kitambulisho. Vitambulisho vya uraia ni hivi ambavyo nilikuwa navisemea katika jibu la msingi ambavyo vitatolewa kwa wote Tanzania Bara na Visiwani. (*Makofi*)

Na. 279

**Zoezi la Kupeleka Umeme Kwenye Makao Makuu ya Wilaya**

**MHE. ROBERT K. MASHALA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliazimia kufikisha umeme Makao Makuu ya Wilaya zote ambazo hazina umeme nchini ikiwemo Wilaya ya Bukombe ifikapo mwaka 2005 na kwa kuwa azma hiyo imeshindwa kufikiwa kwenye Wilaya nyingi kwa sababu hazina umeme.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani mpya wa kupeleka umeme kwenye Wilaya ambazo hazina umeme baada ya mkakati wa mwanzo kushindwa kufikiwa; na Je, ni Wilaya zipi ambazo hazikupatiwa umeme kwa mpango huo?

(b) Je, *Sub-station* inayojengwa (Ilogi-Kahama *Mine*) kwa ajili ya kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Bukombe itakamilika lini na kazi ya kuweka nguzo za umeme kuelekea Bukombe itaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Robert Kaji Mashala, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali wa kufikisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya haukushindwa. Kati ya mwaka 1995 hadi 2005 na kama ilivyotamkwa katika hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ukurasa wa saba, Wilaya 23 zimepatiwa umeme kwenye Makao Makuu yake.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumewahi kusema mara nyingi hapa Bungeni, utekelezaji wa mpango mzima wa kufikisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya unatokana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 1995 na Ilani ya Uchaguzi ya CCM

ya mwaka 2000. Kwa mfano, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000 katika Ibara ya 51 (iii) imeahidi na napenda ninukuu, kutoa kipaumbele katika usambazaji umeme katika Miji Mikuu ya Wilaya iliyobaki. Napenda kumaliza nukuu hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000, Wilaya 18 wakati huo hazikuwa na umeme, na hadi sasa 13 kati ya hizo 18 za mwaka 2000 ama zimepata au ziko njiani kupata umeme. Kwa maneno mengine zaidi ya asilimia 70% ya Ilani ya Uchaguzi itakuwa imetekelezwa ifikapo mwishoni mwa mwaka huu wa 2005.

Hata, hivyo kati ya mwaka 2000 na 2005, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alianzisha Wilaya mpya saba, hivyo kufanya idadi ya Wilaya ambazo hazina umeme kwa sasa na kama zilivyotajwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kufikia 13. Kati ya Wilaya hizi 13 wilaya mpya 7 hazikuwa na ahadi iliyomo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000. Wilaya ambazo bado hazijapata umeme zimetajwa katika ukurasa wa saba wa hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini ya mwaka huu wa 2005. Nazo ni Bukombe, Simanjiro, Namtumbo, Mbinga, Kibondo, Nkasi, Ngorongoro, Ludewa, Kilolo, Kilindi. Uyuwi na Kasulu.

Mheshimiwa Spika, makakati ambao umeleta mafanikio makubwa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ni ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania, *TANESCO*, Wafadhili na Wawekezaji. Serikali inatarajia kuendelea na mkakati huu ambao hivi sasa umeongezewa nguvu kwa kuanzisha mpango kabambe wa usambazaji vijijini wa *ERT* na uanzishwaji wa mfuko na Wakala wa Umeme Vijijini yaani *REF*/*REA*.

Kimsingi mradi wa umeme wa Makao Makuu ya Wilaya ya Bukombe-Ushirombo umeshakubaliwa kufadhiliwa na Serikali ya Sweeden kupitia shirika lake la *SIDA*. Mradi huu utahusisha ujenzi na njia ya umeme wa msongo *33KV,* kutoka kijiji cha Ilogi. Hivi sasa ujenzi wa njia ya umeme kuelekea Bugarama hadi Ilogi kutoka kituo cha kupozea umeme yaani *sub-station* cha Bulyankulu umeshaanza na vifaa vyote vya laini kubwa na ndogo vimeshafikishwa kwenye bohari za mgodi wa kampuni ya madini wa Kahama. Kazi ya usambazaji umeme kwenye vijiji vya Bagarama na Iligo pia imeshaanza.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa *sub-station* ya Bulyankulu kwa ajili ya kupeleka umeme miji ya Bugarama na Ilogi na baadaye ya Wilaya ya Bukombe umeshakamilika.

Hivyo kazi ya ujenzi wa njia ya umeme kuelekea Bukombe itaanza mara taratibu za kupata fedha kutoka *SIDA* ya Sweeden zitakapokamilika na mara kazi ya kuufikisha umeme Ilogi itakapokwisha.(*Makofi*)

**MHE. ROBERT K. MASHALA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba kuuliza swali mmoja la Nyongeza. Kwa kuwa kwa mujibu wa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri inaonekana zoezi hili linaweza likachukua muda

mrefu na kwa kuwa wananchi wa Bukombe kama walivyo wananchi wa sehemu nyingine, wanahitaji huduma ya umeme.

Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa sasa wa kupeleka angalau huduma ya *generator* kwa ajili ya umeme ili kusaidia wananchi wa Wilaya ya Bukombe kama vile Hospitali ya Wilaya na huduma zingine muhimu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, mimi naamini kabisa kwamba wananchi wa Bukombe wanabahati kubwa kwamba sasa hivi Serikali imo katika utaratibu wa utekelezaji wa kufikisha umeme wa uhakika kwenye Makao Makuu ya Wilaya yao.

Ningependa kuwashauri tu kwamba wasubiri mradi huuambao ni muhimu na ni mradi utakao waletea umeme wa uhakika. Kupeleka *generator,* uzalishaji kupitia *generator* ni wa gharama kubwa na kwa sasa hvi kwa kweli shirika letu la umeme nchini *TANESCO* haliwezi kumudu gharama hizo.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo lililopo Bukombe linafanana sana na lile lililoko katika Jimbo la Siha, na kwa kuwa Naibu Waziri alifika katika Jimbo la Siha na kuagiza kwamba umeme uende katika vijiji mbalimbali na sasa hivi nguzo zimeshawekwa chini, je, vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya huo umeme vitafika lini kule?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI :** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli nilifika na kama ambavyo nilishawahi kuwashukuru wananchi wa sehemu husika nawashukuru tena kwa kunipokea na ni kweli kwamba kuna mradi ambao unaendelea wa kufikisha umeme, napenda kusema tu kwamba sasa hivi kuna tatizo la vifaa vinavyoitwa *conductors* karibu nchi nzima.

*TANESCO* wameagiza vifaa hivi, ni matumaini yetu kwamba vifaa hivi vitapatikana katika muda mfupi ujao, na napenda nichuke nafasi hii niwafahamishe wananchi wa Jimbo la Siha kwamba zile ahadi zilizotolewa na Serikali pale haikuwa ya kudanganya, ilikuwa ni ahadi madhubuti na kinachokosekana sasa hivi ni ukesefu wa vifaa ambavyo haviko katika mradi ule tu lakini miradi mingine vipo na ni matumaini yetu kwamba katika muda mfupi ujao vifaa vikipatikana miradi ile itaendelea kutekelezwa.

Na. 280

**Mahitaji ya Umeme**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE (K.n.y. MHE. BENSON M. MPESYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa umeme umekuwa ni nyenzo muhimu ya kichocheo cha maendeleo ya watu hasa katika maeneo ya pembezoni mwa miji yetu:-

(a) Je, Serikali itapelekea umeme wa *Three phase line* kwenye kata ya Itende badala ya *One phase line* ambayo hiakidhi matumizi ya uendeshaji wa mitambo kama vile mashinie za kusaga nafaka, mbao na kadhalika?

(b) Kwa kuwa, eneo lote linalozunguka Chuo cha Ufundi Mbeya, mtaa wa Ikuti wapo watu wengi sana wanaohitaji huduma ya umeme. Je, ni lini eneo hilo litapatiwa umeme wa uhakika ili nao wafaidike kwa kuwa jirani na maeneo ya Chuo hicho?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, kama ifuatavyo:-

(a) Kazi ya kupeleka umeme maeneo ya Itende itahusisha ujenzi wa laini ya *11KV* yenye urefu wa kilomita 1.5, ufungaji wa transfoma ya kupoozea umeme yenye ukubwa wa *100KVA* na ujenzi wa *low voltage line* yenye urefu wa kilomita 2. Gharama ya kazi hii inakadiriwa kuwa Shilingi milioni 37.

(b) Kazi ya kupeleka umeme katika maeneo yanayozunguka eneo la Chuo cha Ufundi na eneo la Itende Mbeya itahusisha maeneo ya Ikuti I na II, Lumbila-Iyunga pamoja na Iwambi. Kazi zitakazofanyika ni ujenzi wa laini yenye kilomita 2 ya *11KV* ujenzi wa laini ya kilomita 5.5 ya *low voltage*, ufungaji wa transfoma 4 zenye uwezo wa *100KVA.*

Mheshimiwa Spika, gharama za kupeleka umeme maeneo hayo yanayozunguka Chuo cha Ufundi Mbeya na Iyunga inakadiriwa kuwa Shilingi milioni 73. *TANESCO* na Serikali inafahamu umuhimu wa kuweka umeme wenye nguvu kubwa kwenye maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge na *TANESCO* kwa upande wake imepanga kuitekeleza kazi hii katika mwaka huu wa 2005. Sasa hivi wako katika utaratibu wa kutafuta fedha. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, nina swali la nyongeza.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba iwapo Vijiji vyetu vitapata umeme katika nchi hii, itasaidia sana maendeleo katika Vijiji hivyo vikiwemo Vijiji vya Mbeya pamoja na Mpwapwa, Berege, Mima na Chunyu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye Mheshimiwa Mbunge mia kwa mia na ndiyo maana Serikali imeweka mpango kabambe wa usambazaji umeme vijijini ambao nimeutaja katika majibu yangu ya msingi wakati najibu swali hapa Bungeni la Mradi wa *ERT* na ndiyo maana pia Serikali imeanzisha Wakala wa Usambazaji Umeme Vijijini na Mfuko Maalum wa Usambazaji Umeme Vijijini.

Na. 281

**Barabara ya Mpanga – Ipinda**

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA (K.n.y. MHE. JOHN L. MWAKIPESILE)** Aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inafanya kazi nzuri ya kutengeneza barabara ya Kikusya – Ipinda – Matema;

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa kuna haja sasa ya kutandaza changarawe katika barabara hiyo na kati ya Mpunguti na Kisyosyo ili kuondoa kero ya kukwama kwa magari wakati wa mvua za masika?

(b) Je, Serikali itakubali kutekeleza ombi la kutembelea na kukagua kazi inayofanywa na wananchi wa Ikombe wanaovunja miamba ili kuchonga barabara kutoka Lyulilo hadi Ikombe Kilomita 4 na kuondokana na kero kubwa ya kusafiri kwa mitumbwi?

(c) Je, Serikali inaweza kutusaidia shilingi milioni 50 kwa ajili ya kumalizia barabara hiyo na kuwakomboa wananchi wa Ikombe?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII , JINSIA NA WATOTO (K. n. y. WAZIRI WA UJENZI)** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa John L. Mwakipesile, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kikusya – Ipinda – Matema yenye urefu wa kilomita 40 ni barabara ya Mkoa na inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Mbeya. Barabara hiyo imejengwa kwa kiwango cha changarawe kilomita 32 na kilomita 8 zilizobaki kwa udongo.

Mheshimiwa Spika, barabara hiyo imekuwa ikifanyiwa matengenezo ya kawaida na ya sehemu korofi na hivyo kupitika bila matatizo makubwa. Katika mwaka wa Fedha 2003/2004 Wizara yangu ilitumia kiasi cha shilingi milioni 17.8 kwa matengenezo ya sehemu korofi yaliyohusisha pia kuweka changarawe kilomita 4.

Aidha, mwaka wa fedha 2004/2005 Wizara yangu pia ilitumia shilingi milioni 82.6 kwa matengenezo ya sehemu korofi kwa kuweka changarawe kilomita 4 na kutengeneza madaraja matatu.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Lyulilo hadi Ikombe yenye urefu wa Kilomita 4 inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kyela. Mwaka 2002 barabara hii ilianza kulimwa kwakutumia fedha za *TASAF*. Katika kutekeleza kazi hiyo, palijitokeza tatizo kubwa la miamba mikubwa na hivyo kulazimu kutumia baruti kulipua miamba. Kazi hiyo ilifanywa na wataalam kutoka *Kiwira Coal Mine* na baadaye aliwekwa Mkandarasi kwa ajili ya kazi hiyo.

Aidha, kazi ya kulipua miamba imekamilika, kazi iliyobaki ni ya kutoa mawe pamoja na udongo uliopo kwenye barabara hii. Kazi hii itaendelea baada ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kupata fedha nyingine.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa John L. Mwakipesile, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, kuna haja ya kutandaza changarawe katika barabara hiyo. Kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya awali, Serikali itaendelea kutenga fedha za matengenezo ikiwa ni pamoja na kipande cha Mpunguti na Kisyosyo hadi Matema kulingana na uwezo wa kifedha ili kuondoa kero ya kukwama kwa magari wakati wa masika.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubali ombi la Mheshimiwa Mbunge la kutembelea kuona kazi inayofanywa na wananchi wa Ikombe pindi nafasi itakapopatikana.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kwa sasa haina shilingi milioni 50 alizoomba Mheshimiwa Mbunge. Ili kuendeleza Mradi, Serikali itaendelea kutafuta fedha toka vyanzo mbali mbali ili kukamilisha mradi huu.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Ahsante sana kwa majibu mazuri na nataka niipongeze Serikali kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kufanya kwenye barabara hiyo.

Kwa kuwa eneo la Kyela liko kwenye Bonde la Ufa *(Lift Valley)* kwa hiyo barabara zinazotengenezwa pale usipoweka kokoto kwa wingi na changarawe kwa kuinua tuta, bado tatizo litaendelea vile vile. Je, Serikali sasa itatoa hela za kutosha kwa sababu ile iliyowekwa imeishachukuliwa na maji kwa ajili ya mafuriko ili iweze kuinuliwa mapema kabla mvua kubwa hazijaanza kunyesha?

Pili, nashukuru kwa kuwa Serikali imekubali kwamba itakwenda kuangalia eneo ambalo wananchi wanapasua miamba. Je mnapokwenda pale kukagua si ni vizuri mngeenda mapema na baadaye muweze kuwaunga mkono kama Serikali ili wananchi waweze kutiwa moyo?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO (K. n. y. WAZIRI WA UJENZI):-**

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Eliachim J. Simpasa amezungumzia suala la kuweka changarawe kwa wingi na kujenga tuta. Nakubaliana na Mheshimiwa Eliachim J. Simpasa kwamba iko haja ya kufanya hivyo na ndiyo sababu Wizara yangu imekuwa ikaweka changarawe na kufanyia matengenezo eneo korofi kila mara ilipojitokeza na tunachukua ushauri wake.

Lakini ningeomba pia kuchukua fursa hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba tuendelee kushirikiana kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara na kutumia Halmashauri na nguvu za Serikali na Wizara itaendelea kutoa mchango wake.

Mheshimiwa Spika, pili tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba iko haja ya kwenda pale mapema kwa sababu kwa kweli nia ya kuzifanyia matengenezo ya mara kwa mara barabara hizi ni ili ziweze kupitika wakati wote, tutafanya hivyo.

Lakini mwisho napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Eliachim J. Simpasa kwa juhudi zake kwa sababu amekuwa akifuatilia barabara hizi toka mwaka wa 2001. Tunampongeza yeye na pia Mheshimiwa John L. Mwakipesile. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda kujua sheria hii ambayo inaweka sehemu ya akiba ya kutengeneza barabara *(road reserve)* imewekwa kwa ajili ya maendeleo ya watu.

Je, si vizuri sheria hii ikatekelezwa kufuatana na mazingira, kwa mfano ukiitekeleza ilivyo katika sehemu za milimani kama kule Lushoto, Mwanga, Upare Juu milimani na sehemu zingine kama hizo, basi itabidi usiwe na watu katika maeneo hayo?

**SPIKA:** Hilo ni swali jipya kabisa sijui kama Waziri ana jibu. Inaelekea hana jibu, basi tunaendelea na swali linalofuata. (*Kicheko*)

Na. 282

## Ubomoaji wa Nyumba Kando ya Barabara

**MHE. GWASSA A. SEBABILI** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wanaipongeza Serikali kwa juhudi zake za kuharakisha maendeleo likiwemo suala la ujenzi wa barabara zetu kwa kiwango cha lami.

Lakini pamoja na juhudi hizo, suala la ubomoaji wa nyumba/vibanda zilizo kwenye *road reserves* limezua gumzo mijini hata vijijini ambako baadhi ya majengo yamewekwa alama nyekundu ya X inayoashiria kubomolewa kwa nyumba hizo; na kwa kuwa baadhi ya barabara zilichimbwa wakati wa kupigania Uhuru na kwa nguvu za wananchi huko vijijini kwa utaratibu wa kujitolea/ kujenga Taifa, na ili sasa nchi yetu iweze kuendelea ni lazima kuwa na miundombinu imara ya barabara:-

(a) Kwa kuwa, tofauti ya barabara za Mijini na barabara za vijijini zilikuja wakati wananchi wameishajenga vijumba vyao. Je, sheria ya *Road Reserves* na Serikali kwa ujumla itawafikiriaje raia wa aina hiyo hata kama sheria hiyo ilikuwepo?

(b) Je, Serikali itafanya uchunguzi na uchambuzi wa kina na wa muda mrefu ili kubaini gharama za kubomoa nyumba zinaendana na ujenzi wa nyumba aina yoyote miaka 10 - 30 iliyopita ikilinganishwa na ujenzi wa nyumba hiyo hiyo leo hii ili kufanikisha zoezi hilo?

(c) Kwa kuwa huko Mijini, mtu anayejenga hupata idhini ya Serikalini kabla ya kujenga. Serikali itawezaje kuvunja nyumba na kutomfidia mwenye nyumba aliyeidhinishiwa kujenga?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO (K. n. y. WAZIRI WA UJENZI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gwassa A. Sebabili, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikiendesha zoezi la uwekaji wa alama ya X kwenye nyumba zote ambazo zipo ndani ya eneo la miliki ya barabara *(Road Reserve)* kwa lengo la kuzitambua na kisha kuwataka wahusika wazibomoe ili kutoa nafasi kwa mipango mbali mbali ya upanuzi wa barabara.

Aidha, katika yale maeneo ambayo shughuli za ujenzi mpya ama upanuzi wa barabara umefanywa nje ya mipaka ya eneo la miliki ya barabara, Wizara yangu imekuwa ikitoa fidia mara zote kwa wenye nyumba hizo ili waziondoe kwenye maeneo hayo na hivyo kutoa nafasi kwa matengenezo yaliyokusudiwa kuweza kufanyika.

Sambamba na nyumba hizo, mazao yaliyomo mashambani pia hufanyiwa tathmini na fidia kulipwa kwa wahusika.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kabla ya kufanya malipo na fidia huwa inawasiliana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ili kupata wataalam wa kufanya tathmini ya nyumba ama mazao ili kutambua gharama halisi ya fidia kwa mwananchi aliyeathiriwa na zoezi hilo. Wataalam hao hutoa tathmini ya gharama mbali mbali ambazo atafidiwa mwananchi aliyebomolewa nyumba ambazo ni hizi zifuatazo:-

(i) Gharama halisi ya nyumba kwa bei za wakati wa kufanya tathmini;

(ii) Gharama za usumbufu;

(iii) Gharama za malazi iwapo mwananchi huyo atalazimika kupanga kabla ya kukamilisha kazi ya ujenzi wa nyumba mpya; na

(iv) Gharama za usafirishaji wa vifaa.

Hivyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wataalam wa Wizara ya Ardhi na Mendeleo ya Makazi huwa wanafanya uchunguzi wa kina ili kubaini gharama halisi ya ujenzi wa nyumba kwa wakati huo wa tathmini ili kulipa thamani halisi ya kujenga nyumba mpya na siyo thamani ya miaka 10 hadi 30 iliyopita.

(c)Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kabisa kuwa mtu anapojenga nyumba hupata idhini Serikalini kabla ya kufanya ujenzi huo.

Kwa kutambua hilo, Wizara yangu huwa inawasiliana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi pamoja na Serikali za Miji ama Wilaya husika wakati wa tathmini za fidia kwa wamiliki halali wa nyumba na mazao.

Iwapo itathibitika kwamba mmiliki wa nyumba anastahili fidia kwa mujibu wa sheria, huwa anafidiwa nyumba iliyowekwa alama ya X ili kuruhusu shughuli za ujenzi.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake ya kupendeza na kutia moyo. Hapa ndipo Serikali inaweza kutamkwa kwamba sasa inaujua Utawala wake Bora.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, naomba niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa hapo kwanza ujumla wa bomoa bomoa ulikuwa kwamba yeyote aliye kando kando

ya eneo la barabara katika eneo la akiba nyumba zitabomolewa, lakini haikutajwa kwamba kungekuwa na tathmini na hivyo hatimaye kutoa fidia.

Likini sasa maswali yanakuja katika hali hii ya kutia moyo waliojenga kando kando ya barabara na wale ambao wamekutwa na barabara kwamba wataweza kufidiwa. Je, taarifa hizi zinawafikiaje waathirika? Haitakuwa vizuri kwamba pengine Wilaya zinazohusika na Mikoa inayohusika, ikapewa taarifa za namna hii kusudi wale wanaoweza kuhusika wakaweza kujiaandaa kupewa maelezo ya kina?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO (K. n. y. WAZIRI WA UJENZI):** Mheshimiwa Spika, Sheria inayohusika na ujenzi na ubomoaji wa majengo ambayo yapo kando kando ya barabara inataka kwamba wale ambao walikaa pale wakakutwa na barababa wanaweza wakafidiwa.

Wale ambao wanapaswa kufidia wanakuwa wanapata taarifa hizo kwa sababu Wizara yangu inaanza kwanza kuweka X ikiwa kama ni ilani kwamba hii nyumba iko nje ya barabara na ikifahamika kwamba jengo lile au mazao yale yapo baada ya barabara kuanza kupanuliwa, kisheria wao huweza kulipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, taarifa za kulipwa fidia huwa zinapelekwa. Kwanza Wizara yangu imehusika sana na kutoa elimu. Pili, *Regional Managers* wanakuwa na kazi za kuangalia ni wakati gani ambapo majengo haya yanastahili kubomolewa kwa hiyo huwa wanafahamisha. Lakini tatu, Wakurugenzi na Halmashauri husika huwa pia zinapata taarifa za utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Gwassa A. Sebabili kwamba Wizara pamoja na vyombo hivyo nilivyovitaja vitaendelea kutoa elimu hiyo na wananchi mara kwa mara wale ambao wanastahili kufidiwa kisheria huwa wanapata fidia zao.

Lakini pia naomba nimwombe Mheshimiwa Gwassa A. Sebabili kama ambavyo amekuwa akifuatilia suala hili toka siku za nyuma, aendelee pia kuwahamasisha na kuwaelewesha wananchi umuhimu wa kutojenga ndani ya maeneo ya barabara, basi pale linapotokea basi tushirikiane katika kuwafahamisha wananchi haki zao.

Na. 283

**Fidia ya Mali – Barabara ya Kibiti – Mingoyo**

**MHE. ALHAJI AHAMADI HASSAN MPEME (K. n. y. MHE. OMARI MOHAMED MWENDA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wengi waliolipwa fidia ya mali zao katika ujenzi wa Barabara ya Kibiti – Lindi – Mingoyo wanamlalamikia Mthamini aliyethamini mali zao kuwa hakutenda haki:-

(a) Je, huyo Mthamini alichaguliwa kwa kigezo gani?

(b) Je, kwa nini alichaguliwa Bwana Ardhi wa Wilaya kufanywa Mthamini wakati inafahamika kuwa uwezo wake ni mdogo?

(c) Je, Serikali haioni kuwa haikuwatendea haki wananchi hao?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO (K. n. y. WAZIRI WA UJENZI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Mwenda, Mbunge wa Kilwa Kusini, naomba kutoa maelezo ya fuatayo:-

Mheshimiwa Spika, malipo ya fidia kwa wananchi wanaoathirika na zoezi la kuhamishwa wao, mali zao au wao pamoja na mali zao ili kupisha ujenzi wa barabara hufanyika baada ya fomu maalum za uthamini wa mali kuidhinishwa na Wakuu wa Wilaya husika pamoja na Wakuu wa Mikoa wao wenyewe.

Fomu hizi huandaliwa na Wathamini wa Serikali ambao ni wataalam waliopo katika Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri kwa kutumia Sheria Na. 4 na Sheria Na. 5 ya mwaka 1999 pamoja na Kanuni zake chini ya Matangazo ya Serikali *(Government Notes)* Namba 75 na 86 za mwaka 2001.

Fomu hizo za fidia huandaliwa sambamba na ripoti ya uthamini ambayo ni lazima ikaguliwe na kuidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali ambaye ni *Chief Government Valuer* aliyeko Makao Makuu ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Wizara ya Ujenzi baada ya kupata ripoti hizo na fomu maalum za fidia vikiwa vimekamilika kwa kupitia katika hatua nilizozitaja hivi punde, hutayarisha hundi na kulipa Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri husika ambao hufanya malipo kwa waathirika. Katika miradi ya barabara inayoendelea kwa barabara ya Kibiti – Lindi – Mingoyo, Wakurugenzi Watendaji wamekuwa wakilipa waathirika kwa hundi au fedha taslimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Mwenda, Mbunge wa Kilwa Kusini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wataalam waliothamini mali katika miradi ya barabara inayondelea katika barabara ya Kibiti – Lindi – Mingoyo, waliteuliwa na Wakurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Lindi na Halmashauri ya Wilaya ya Lindi.

Wataalam hao ambao ni Watumishi wa Halmashauri husika wana Taaluma ya Uthamini wao ni *Valuers*. Mthamini kutoka Halmashauri ya Mji wa Lindi ana

sifa na amesajiliwa. Aidha, yule wa Halmashauri ya Wilaya ya Lindi naye ana sifa na ni Mthamini Mwandamizi.

(b) Mheshimiwa Spika, Wathamini waliotumika kuthamini mali katika miradi ya ujenzi wa barabara katika barabara ya Kibiti – Lindi – Mingoyo hawakuwa ma-Bwana Ardhi bali walikuwa ni Wathamini wenye sifa za Taaluma hiyo. Hata hivyo ili kazi ya uthamini ifanyike kwa ufanisi, Maafisa hawa kila inapowezekana hufuatana na Maafisa wengine ikiwa ni pamoja na Wataalam wa Ardhi na Maafisa kutoka Wizara ya Ujenzi.

Kama nilivyoeleza katika maelezo ya utangulizi, ripoti zote za uthamini ni lazima ziidhinishwe na Mthamini Mkuu wa Serikali aliyeko Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa vile Sheria, Kanuni na Taratibu zote za Uthamini zilifuatwa, Serikali haioni kama haikuwatendea haki wananchi husika. Badala yake, malipo halali na ya haki ndiyo yaliyofanyika.

Hata hivyo kama kuna ushahidi wa mwananchi yeyote kupunjwa stahili yake ya fidia, anaweza kupeleka malalamiko yake kwa Mkurugenzi wa Wilaya husika kwa maandishi na suala lake litashughulikiwa ipasavyo.

**MHE. ALHAJI AHAMADI HASSAN MPEME:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, isipokuwa nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa wapo wananchi ambao wamebomolewa nyumba zao lakini hawakulipwa chochote kwa sababu ya kwamba wamejenga katika *road reserve*; na kwa kuwa wananchi hao kupitia Operesheni Vijiji, Mpango wa Serikali walihamishwa kutoka katika Vijiji vyao vya asili na kuwapa viwanja katika maeneo ya Vijiji vya Ujamaa karibu na barabara. Sasa Je, nani mwenye kosa ni Serikali au mwananchi na kama ni Serikali, kwa nini leo wanabomolewa na wasilipwe chochote?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO (K. n. y. WAZIRI WA UJENZI):** Mheshimiwa Spika, sheria inayohusu hifadhi ya barabara ni sheria ambayo imekuwepo katika nchi yetu toka mwaka wa 30 na utaratibu wa kuhamisha wananchi ulikuja baadaye. Ni vigumu kukubali kwamba Serikali yenyewe ambayo ndiyo msimamizi Mkuu wa sheria hiyo inaweza ikawahamisha wananchi kutoka maeneo ambayo siyo ya hifadhi ya barabara iweke kwenye hifadhi ya barabara.

Lakini ninaamini kwamba kama kuna suala hilo liliweza kutokea, inawezekana lilifanywa kimakosa na Wizara inaweza kuwa tayari kuliangalia pamoja na wahusika ili ione kama kwa mujibu wa sheria, wanastahili malipo, kwa sababu kujenga ndani ya barabara ni kosa linalofahamika kwa Serikali na linapaswa kufahamika kwa wananchi wenyewe. Lakini endapo imetokea kwamba suala hilo imekuwa ni kazi ya Serikali,

itabidi tuliangalie upya. Lakini si rahisi kwa Serikali kuvunja sheria yake yenyewe ambayo ndiyo inaisimamia.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha. Sina matangazo ya Vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge kwa leo, lakini ningependa kuwatambulisha wageni wa Kimataifa walioko kwenye *Gallery* ya Spika leo asubuhi. Hawa ni wageni wanatoka Uingereza ni wageni wa Mheshimiwa Peter Kabisa naye amekaa nao huko ni Dr. Ian Mourine kutoka Chuo Kikuu Cha Oxford Uingereza na Ndugu Sandra Worthington ambaye ni Mjumbe wa Shirika la *Armnesty International*. Karibuni. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006 -<br>Wizara ya Maliasili na Utalii

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu, likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kupokea, kujadili na kisha kuidhinisha makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2005/2006 kwa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Napenda niwashukuru Wajumbe wa Kamati hii, kwa ushirikiano walioutoa kwa Wizara katika kutekeleza majukumu yake. Naahidi kuwa, Wizara itazingatia mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwa lengo la kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Chama cha Mapinduzi, kwa kumteua Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kuwa, Mgombea wake katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba, 2005. Ninampongeza na kumtakia kila la kheri. *(Makofi)*

Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kuwa, Mgombea Mwenza na Mheshimiwa Amani Abeid Karume kuwa, Mgombea wa Urais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nawatakia afya njema na ushindi mkubwa katika uchaguzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, tumewapoteza Wabunge kadhaa, natoa pole kwa ndugu, wafiwa na Wananchi wa Majimbo yaliyofikwa na misiba hiyo. Mwenyezi Mungu, azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1995 hadi 2005, Wizara kwa kuzingatia Sera na Sheria zake, imetekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na Wananchi, Taasisi na Wahisani mbalimbali katika kutunza na kuhifadhi rasilimali za maliasili, mambo ya kale na vivutio vya utalii. Wizara imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa Taifa letu kwa kuchangia takriban asilimia 16 ya Pato la Taifa. Ukweli huu

unathibitishwa na kuongezeka kwa maduhuli kutoka shilingi bilioni 4.26 mwaka 1995/96 hadi shilingi bilioni 28.0 mwezi Mei, 2005.

Katika kipindi hiki, idadi ya watalii waliotembelea vivutio mbalimbali imeongezeka kutoka watalii 295,312 mwaka 1995 hadi kufikia watalii 582,807 mwaka 2004. Aidha, nchi yetu imeweza kupata tuzo za Kimataifa kama vile *Global Equator Initiative Award* na *Global 100 Eco-Tech Award.* Tuzo hizo zinatolewa kwa miradi inayofanikiwa kuhifadhi mazingira na kupunguza umaskini kwa kushirikisha jamii. Tuzo nyingine nne zimepatikana kutokana na ubora na wasifu wa filamu ya utangazaji wa utalii inayojulikana kama *Tanzania - Authentic Africa.*

Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha Sera ya Uvuvi (1997), Sera za Wanyamapori, Misitu na Nyuki (1998) na Sera ya Utalii (1999). Sera ya Wanyamapori imeanza kufanyiwa tena mapitio ili kujumuisha masuala ya ardhioevu, ambayo yanapewa kipaumbele Kimataifa. Rasimu ya Sera ya Mambo ya Kale, imetayarishwa kwa kushirikisha maoni ya wadau mbalimbali. Sheria za Misitu na Nyuki zilitayarishwa na kuidhinishwa mwaka 2002 na Sheria ya Uvuvi mwaka 2003. Baadhi ya Sheria hizi (Misitu, Ufugaji Nyuki na Uvuvi), zimetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili ili zieleweke zaidi kwa wadau. Rasimu ya Sheria ya Utalii, imetayarishwa kwa kuunganisha Sheria ya Hoteli ya Mwaka 1963 na Sheria ya Wakala wa Utalii ya mwaka 1969.

Mheshimiwa Spika, Sera za Wizara zimeainisha majukumu ya utekelezaji yatakayofanywa na wadau mbalimbali ikiwemo Sekta Binafsi na Wananchi. Katika kutekeleza jukumu kuu la uhifadhi wa rasilimali za maliasili, mambo ya kale na kuendeleza vivutio vya utalii, Wananchi wameshirikishwa kwa namna nyingi. Katika Sekta ndogo ya Wanyamapori, Wananchi waishio katika vijiji vinavyozunguka maeneo ya Hifadhi za Taifa za Serengeti na Ruaha, Mapori ya Akiba ya *Selous,* Maswa, Saadani na Mkomazi, walishirikishwa katika uhifadhi endelevu wa wanyamapori. Mwongozo wa Kanuni za namna ya kushirikisha Wananchi katika uhifadhi wa wanyamapori zilikamilika na kuanza kutumika Januari, 2003 katika maeneo 16 ya majaribio.

Mheshimiwa Spika, katika usimamizi shirikishi wa misitu, Wananchi wa vijiji 1,084 vya Wilaya 12 za Morogoro/Mvomero, Kilombero, Kilosa, Lindi Vijijini, Kilwa, Liwale, Mbozi, Chunya, Mbarali, Kilolo, Njombe na Mufindi, walishirikishwa katika usimamizi wa misitu katika maeneo yao. Vile vile, Wananchi katika vijiji 525 katika Wilaya 63 nchini walishiriki katika kusimamia misitu 37 ya Hifadhi ya Serikali Kuu na ya Halmashauri za Wilaya yenye jumla ya hekta 1,863,623.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa Wananchi katika ufugaji nyuki uliongezeka na kuboresha kipato cha mwananchi kutoka wastani wa pato la Sh.180,000.00 mwaka 1998/99 hadi Sh.266,313.00 mwaka 2003/2004. Wananchi wa vijiji 18 vya Wilaya za Kibondo, Uyui, Manyoni, Kondoa na Handeni, walitenga maeneo ya Hifadhi za Nyuki yenye ukubwa wa hekta 82,931. Katika sekta ndogo ya uvuvi, Wananchi walishirikishwa kuunda vikundi vya ulinzi ili kusimamia rasilimali ya uvuvi kwa kulinda mazingira ya ufukweni katika Ukanda wa Ziwa Victoria, ambako vikundi 511 vimeanzishwa.

Wananchi pia walielimishwa kuhusu umuhimu wa mambo ya kale na kuhamasishwa kushiriki katika kuhifadhi na kuendeleza urithi huo. Kamati nne za kuhifadhi na kulinda maeneo ya mambo ya kale ziliundwa na Wananchi wanaozunguka vituo vya Bagamoyo, Kilwa Kisiwani, Kolo - Kondoa na Mikindani. Vikundi vya vijana wapatao 50 kutoka maeneo ya Kalenga, Isimila, Bagamoyo, Kilwa Kisiwani na Tanga, vilihamasishwa na kushirikishwa katika shughuli za kutembeza wageni katika maeneo ya Hifadhi ya Mambo ya Kale. Aidha, vikundi vya utalii wa utamaduni viliongezeka kutoka 18 mwaka 2003 hadi vikundi 24 mwaka 2004. Vikundi hivyo viko katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Pwani, Tanga, Mbeya, Iringa na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1995 hadi 2005, ulinzi wa wanyamapori uliimarishwa katika mapori 18 ya akiba na Vikosi Dhidi ya Ujangili vinane kwa kupatiwa vitendea kazi ikiwemo magari, sare za kazi, silaha, pamoja na ujenzi wa nyumba 25 za kuishi, maghala mawili ya kuhifadhi silaha na ofisi 10. Aidha, vituo vipya vinane vya doria vimeanzishwa, ujenzi wa zahanati tatu, maabara mbili na madaraja mawili. Uwezo wa kuendesha doria umeongezeka kutoka siku 11,000 hadi 41,000 katika kipindi cha 1995 hadi 2005, ambapo watuhumiwa 5,160 walikamatwa kwa tuhuma mbalimbali.

Katika kuhakikisha mazingira yanadumishwa, Serikali ilizuia uvunaji wa misitu na mazao mengine yaliyo kwenye vyanzo vya maji, kando ya mito na mabonde. Usafirishaji magogo nje ya nchi ulisitishwa kuanzia Oktoba, 2004 ili kutoa fursa ya kuendeleza viwanda vya ndani na kuongeza thamani ya bidhaa. Doria za uvuvi ziliendelezwa na katika bahari kuu, doria hizo zilifanyika kwa kutumia ndege na meli chini ya mradi unaoshirikisha Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, kwa ufadhili wa Jumuiya ya Nchi za Ulaya.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wamekuwa wakinufaika na rasilimali za maliasili kwa namna mbalimbali. Kwa upande wa wanyamapori, Wananchi wanaoishi ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro, maeneo yanayozunguka mapori ya akiba, pamoja na Hifadhi za Taifa, wamepatiwa kiasi cha Sh.4,638,034,923.13 kwa ajili ya kuendeleza miradi ya elimu, afya, maji, mabwawa na vituo vya kuhudumia mifugo. Kati ya mwaka 2000 na 2003, makampuni ya uwindaji wa kitalii yamechangia jumla ya Sh.2,198,903,875.00 kwa ajili ya huduma za jamii na uhifadhi katika Wilaya zenye shughuli za uwindaji wa kitalii. Kwa upande wa miundombinu, barabara zenye urefu wa kilomita 71 zilizogharimu jumla ya Sh. 739,783,000.00 zilitengenezwa nje ya maeneo ya hifadhi katika Wilaya za Kilombero na Ulanga. Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, ilisaidia kupunguza umaskini kwa familia 4,000 za Kimasai kwa kuwapatia mifugo bora yenye thamani ya Sh.180,000,000.00.

Vile vile, Halmashauri za Wilaya 41 zenye maeneo ya uwindaji wa kitalii ziligawiwa Sh.1,961,487,653.40, ambazo zilitokana na asilimia 25 ya mgao wa fedha za uwindaji wa kitalii. Mafunzo kuhusu mbinu sahihi za ufugaji nyuki, yalitolewa kwa wafugaji nyuki wa Wilaya za Kibondo, Uyui, Kondoa na Handeni. Wastani wa mizinga bora uliongezeka kutoka mizinga sita kwa mfugaji nyuki hadi mizinga 62 kwa mfugaji katika mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, idadi ya watalii wanaotembelea nchini imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia kumi kwa mwaka kuanzia mwaka 1995. Watalii 295,312 walitembelea vivutio mbalimbali nchini na kuingiza pato la Dola za Kimarekani milioni 259.44 ukilinganisha na watalii 582,807 walioingiza pato la Dola za Kimarekani milioni 746.02 mwaka 2004. Mafanikio hayo yamechangiwa na hali ya amani na utulivu iliyoko nchini, pamoja na jitihada kubwa za utangazaji wa utalii ndani na nje ya nchi kwa kutumia tovuti zilizozinduliwa Kitaifa kutangaza utalii ambazo ni *www.tourismtanzania.go.tz* na *www.tanzaniatouristboard.com.* Aidha, mkutano wa wawekezaji katika Sekta ya Utalii uliandaliwa, ambao ulibaini maeneo yanayofaa kwa uwekezaji katika utalii nchini. Katika kuimarisha vivutio vya mambo ya kale, ukarabati wa majengo ya kale ulifanyika katika vituo vya Kaole, Bagamoyo, Olduvai, Kalenga, Kilwa Kisiwani na Songo Mnara. Idadi ya wageni waliotembelea Makumbusho ya Taifa imeongezeka toka 21,674 mwaka 2000/2001 hadi 156,696 hapo Machi, 2005.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake, Wizara katika kipindi hiki ilitilia mkazo katika mafunzo na utafiti. Ili kuimarisha utafiti wa Wanyamapori, idadi ya watumishi katika Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori imeongezeka kutoka 33 mwaka 1995 hadi watumishi 106 mwaka 2004 na idadi ya sensa ya wanyamapori imeongezeka toka tano mwaka 1995 hadi sensa 10 mwaka 2004. Shughuli za utafiti ziliongezeka kutoka moja mwaka 1995 hadi tano mwaka 2004. Aidha, idadi ya Watafiti wa wanyamapori wameongezeka sawia toka watafiti 40 hadi 105.

Mheshimiwa Spika, mafunzo kwenye Sekta ndogo ya Misitu na Nyuki yaliendeshwa katika Vyuo vya Misitu, ambapo jumla ya wanafunzi 601 walihitimu katika fani za astashahada na shahada.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ndogo ya Uvuvi, Elimu ya Ufugaji wa Samaki ilitolewa kwa wafugaji wa samaki katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Mbeya, Pwani, Singida, Mtwara na Lindi. Elimu kuhusu ukulima wa mwani ilitolewa katika Mikoa ya Tanga, Pwani, Mtwara na Lindi.

Chuo cha Taifa cha Utalii kimeweza kutoa mafunzo ya cheti kwa wahitimu 1,220 katika fani ya hoteli na utalii. Aidha, programu za kutoa elimu ya uhifadhi wa urithi wa utamaduni kwa shule na vyuo hapa nchini uliandaliwa. Wataalam wa utafiti wa Mambo ya Kale waliongezeka kutoka sita mwaka 1995 hadi kufikia wataalam 25 mwaka 2004.

Tafiti za Mambo ya Kale ziliongezeka kutoka 12 mpaka 22, ambazo zilifanyika katika maeneo ya Singida, Morogoro, Laetoli, Olduvai, Njombe, Milima ya Udzungwa na Usambara na Ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora, amani na utulivu ni misingi mikuu katika kuleta maendeleo katika Taifa, yenye uwiano, kuvutia watalii na wawekezaji kutoka nje na ndani. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu, uwekezaji katika Sekta za Maliasili na Utalii umeendelea kuongeza ajira nchini. Hoteli tisa kati ya 11 zilizobinafsishwa zinaendelea vizuri, kwa kutoa huduma bora zenye kiwango cha

Kimataifa; baadhi zikiwa ni *New Kunduchi Beach Hotel, New Africa Hotel* na *New Safari Hotel.* Aidha, Hoteli ya *Kempinski* - Kilimanjaro itafunguliwa karibuni.

Katika juhudi za kukuza uwekezaji, Wizara kwa kushirikiana na Wakala wa Udhamini wa Kimataifa *(MIGA),* imeanzisha programu ya kuongeza nguvu za mitaji za wawekezaji wa ndani kwa kupitia uunganishwaji na wawekezaji wa nje. Kutokana na programu hii, michanganuo ya miradi mbalimbali imeanzishwa kwa utaratibu huo katika Sekta ya Utalii na kuwasilishwa katika mkutano wa wawekezaji Maputo.

Mheshimiwa Spika, biashara ya wanyamapori hai imeongezeka na kuingiza mapato ya Sh.162,103.50 mwaka 2003/2004, ukilinganisha na Sh.29,724,721 mwaka 1995. Idadi ya Wananchi wanaojihusisha na ufugaji nyuki iliongezeka pia kutoka wafugaji 91 mwaka 1998/99 hadi kufikia 1,400 mwaka 2003/2004. Kufuatia mwongozo unaoonesha utaratibu wa uwekezaji katika Sekta za Misitu na Nyuki mwaka 2001, viwanda vya kupasua magogo viliongezeka kutoka 64 mwaka 2001 hadi 194 mwaka 2004. Kampuni ya *Kilombero Valley Teak Project* imeshapanda hekta 12,121 za miti katika Wilaya ya Kilombero na Kampuni ya *Escarpment Forest* imepanda miti hekta 2,700 katika Wilaya za Mufindi na Kilombero.

Aidha, mauzo ya mazao ya misitu yaliyofanywa na Sekta Binafsi nje ya nchi yamefikia Dola za Kimarekani 11,637.30 mwaka 2003/2004, ukilinganisha na Dola za Kimarekani 5,840.68 mwaka 1995/96. Katika uvuvi wa kibiashara, uvuvi wa kambamiti uliongezeka kutoka vyombo 19 mwaka 1995 hadi vyombo 25 mwaka 2004. Aidha, meli 44 zilipewa leseni za kuvua katika bahari kuu, jambo ambalo kabla ya mwaka 1995 halikuwepo. Biashara ya nje ya mazao ya uvuvi iliongezeka kutoka Dola za Kimarekani 22,244,676 mwaka 1995 hadi Dola za Kimarekani 129,605,815.44 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa muhtasari wa mafanikio ya Wizara katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, sasa naomba niwasilishe mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Wizara kwa mwaka 2004/2005 na malengo ya mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara yangu iliendelea kutekeleza majukumu yake mbalimbali. Ninayo furaha kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ujenzi wa Soko la Samaki la Kirumba, Mwanza, umekamilika na limefunguliwa rasmi Juni, 2005 na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Mheshimiwa Rais, aliweka Jiwe la Msingi wa Jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi, iliyoko eneo la Kunduchi Dar es Salaam, tarehe 16 Desemba, 2004.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilishiriki Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Saba Saba na kupata ushindi wa kwanza kati ya Wizara zilizoshiriki. Filamu ya kutangaza utalii inayoitwa *Tanzania Authentic Africa,* iliyotayarishwa na Bodi ya Utalii Tanzania, ilishinda tuzo nne za Kimataifa kutokana na ubora na wasifu wa filamu yenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara iliendelea kutayarisha Sera ya Mambo ya Kale kwa kuendesha warsha tano za Kanda za kukusanya maoni ya wadau. Aidha, Sera ya Wanyamapori ya Mwaka 1998 imefanyiwa mapitio ili

kujumuisha masuala ya ardhioevu. Wizara iliandaa rasimu ya Sheria ya Utalii na kufanya marekebisho ya Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Na. 12 ya mwaka 1974.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005/2006, Wizara itaandaa Rasimu ya Sera ya Mambo ya Kale na kuendeleza taratibu za kukamilisha Sheria ya Utalii na Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori. Aidha, kanuni za kuendesha na kusimamia utalii wa picha na kanuni za kutekeleza Mkataba wa Kimataifa wa Biashara ya Wanyama na Mimea iliyo hatarini kutoweka, zitatayarishwa ili kuboresha usimamizi na matumizi endelevu ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushirikisha jamii katika kusimamia, kuhifadhi maliasili na matumizi endelevu ya raslimali hizo. Katika kipindi cha 2004/2005, Wizara ilihamasisha jamii ya wavuvi chini ya programu ya ushirikishwaji wa jamii ya uvuvi kwenye menejimenti ya uvuvi katika Bwawa la Mtera. Vikundi 29 vya usimamiaji wa rasilimali ya uvuvi vimeanzishwa kwenye bwawa hilo kwa lengo la kuwa na uvuvi endelevu. Programu kama hii itaendelezwa kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu na Ziwa Rukwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara ililenga kutekeleza mpango wa usimamizi shirikishi wa misitu katika wilaya 37. Mafunzo na warsha za mipango ya usimamizi shirikishi wa misitu zilifanyika katika wilaya 52. Aidha, Wilaya 12 katika Mikoa ya Lindi, Iringa, Mbeya na Morogoro, zimetekeleza mpango wa usimamizi shirikishi wa misitu na Wilaya 25 zimekamilisha taratibu za kutekeleza mpango wa usimamizi shirikishi wa misitu. Katika kipindi cha 2005/2006, wilaya 15 zaidi zitahusishwa katika kutekeleza mpango huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kuwashirikisha Wananchi katika uhifadhi wa wanyamapori, Wizara iliendeleza shughuli za uhifadhi uliojikita katika kushirikisha jamii na utekelezaji wa kanuni za maeneo ya jumuiya ya hifadhi ya wanyamapori katika maeneo 16 yaliyotengwa kwa majaribio.

Katika kipindi cha 2004/2005, Wizara iliendesha mafunzo ya kanuni za maeneo ya jumuiya ya hifadhi ya wanyamapori kwa jumuiya za jamii 11 kati ya 16. Vilevile, jumuiya hizo zilipata mafunzo ya jinsi ya kutumia viashiria katika ufuatiliaji wa shughuli za uhifadhi katika maeneo yao. Aidha, tathmini ya mafunzo kwa wadau wa maeneo ya jumuiya ya hifadhi ya wanyamapori na mtaala wa mafunzo vimeandaliwa.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara itaendelea kuhamasisha Wananchi katika uhifadhi wa wanyamapori na kutoa elimu kuhusu kanuni za maeneo ya jumuiya ya hifadhi ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha uundaji wa vikundi vinavyoendesha utalii wa utamaduni. Mwaka 2004/2005, vikundi hivyo viliongezeka kutoka 18 hadi 24. Vilevile, idadi ya Wananchi wanaoendesha utalii wa aina hii iliongezeka kutoka 250 hadi 270. Aidha, maeneo matano katika Mikoa ya Iringa,

Arusha, Pwani, Dar es Salaam na Morogoro, yalifanyiwa tathmini ili yajumuishwe kwenye vituo vya utalii wa utamaduni nchini.

Katika kipindi cha 2005/2006, Wizara itaandaa Mwongozo wa Utalii wa Utamaduni na kukamilisha zoezi la kutathmini shughuli za utalii wa utamaduni kwa lengo la kubaini mchango halisi kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara iliandaa warsha ya wadau kuhimiza uhifadhi wa maeneo ya mambo ya kale yaliyo katika njia kuu ya kati ya barabara ya utumwa na vipusa. Warsha hii ilihusisha Halmashauri za Wilaya na Manispaa, ambako njia ya utumwa ilipita kuanzia Ujiji (Kigoma) hadi Bagamoyo (Pwani). Aidha, Wananchi wa Kilwa Kisiwani wameshirikishwa katika uhifadhi, ukarabati wa magofu na kuandaa mpango wa uendelezaji wa Kilwa. Mwaka 2005/2006, Wizara itaendelea kuihamasisha jamii juu ya uhifadhi wa njia kuu ya utumwa na vipusa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, doria 199 dhidi ya uvuvi haramu na biashara ya magendo ziliendeshwa baharini, Ziwa Victoria na Tanganyika, ambapo watuhumiwa 361 walikamatwa. Zana haramu 4,206 zilikamatwa na nyingine 5,615 zilisalimishwa kutokana na ushirikiano mzuri uliopo kati ya Serikali na Wananchi. Aidha, kilo 328,863 za samaki wakavu na samaki wa mapambo 1,659 vilikamatwa.

Mwaka 2005/2006, Wizara itaongeza na kuimarisha doria mipakani katika Ziwa Victoria. Doria za kawaida 50 zitaendeshwa katika bahari, Ziwa Victoria na Tanganyika. Mienendo ya vyombo vya uvuvi baharini itadhibitiwa kwa kutumia mfumo wa kuratibu mienendo ya meli *(Vessel Monitoring System).* Aidha, injini 20 zenye ukubwa wa *horse power* 25 zitanunuliwa kwa ajili ya vikundi mbalimbali vya ulinzi wa rasilimali zilizopo Ziwa Victoria na Bwawa la Mtera.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilifanya tathmini ya uvunaji wa miti katika Wilaya ya Rufiji na Mikoa ya Lindi na Mtwara. Tathmini hiyo ilibaini kuwa kulikuwa na uvunaji mkubwa wa miti katika maeneo hayo. Kufuatia matokeo ya tathmini hiyo, mwezi Julai, 2004 doria maalum ilifanyika katika Mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara. Katika doria hiyo, magogo 17,856 yenye mita za ujazo 5,357; mbao za kawaida 3,606 na za sakafu 3,444 zilikamatwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara iliimarisha ulinzi wa wanyamapori kwa kuwapatia watumishi vitendea kazi na kutoa mafunzo kwa Askari Wanyamapori 126. Hadi kufikia Machi 2005, watuhumiwa 1,582 walikamatwa kwa makosa mbalimbali. Nyara za Serikali zikiwemo meno ya tembo 61 yenye uzito wa kilo 539, ngozi 114 za wanyama mbali mbali, nyamapori kilo 106 na wanyamapori hai 14 wa aina mbalimbali walikamatwa. Vilevile, bunduki 153 za aina mbalimbali, mikuki 18, mishale 31, mapanga 338 na nyaya 672 za kutegea wanyamapori zilikamatwa. Magari matano na baiskeli 65 zilizohusika kwenye ujangili zilikamatwa. Katika kipindi cha 2005/2006, Wizara itaendelea kuimarisha uwezo wa kuendesha doria kwa kutoa vitendea kazi na kuwapatia watumishi mafunzo kuhusu mbinu mbalimbali za kupambana na majangili.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara iliendelea kutoa elimu kuhusu uvuvi bora; uhifadhi na matumizi endelevu ya misitu na wanyamapori; umuhimu wa maeneo ya kihistoria na uhifadhi kwa kurusha hewani vipindi 82 vya redio na 14 vya televisheni. Aidha, elimu kwa jamii imetolewa kwa kusambaza vipeperushi, mabango, majarida, kuendesha mikutano, warsha na semina mbalimbali. Mwaka 2005/2006, Wizara itarusha vipindi 104 vya redio, 21 vya televisheni, pamoja na kuchapisha majarida, vipeperushi na mabango. Aidha, Wizara itaendelea kuielimisha jamii kwa kuendesha mikutano, semina na warsha mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhifadhi misitu ya lindimaji na mikoko kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo ushirikishaji wa jamii. Katika mwaka 2004/2005, vijiji 245 vinavyopakana na misitu ya lindimaji na vijiji 100 vinavyopakana na misitu ya mikoko vilishiriki katika usimamizi, ulinzi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu hiyo. Katika kupunguza shinikizo la matumizi ya misitu hiyo, Wizara imewapatia wanavijiji 1,077 mafunzo ya ufugaji wa kisasa wa nyuki na samaki, matumizi ya majiko banifu na matumizi ya mazao yasiyo timbao. Vile vile, kitini *(manual)* cha kufundishia elimu ya mfumo-ikolojia wa mikoko na misitu ya lindimaji kimeanza kutumika kwenye Shule za Msingi 32 zilizoko ukanda wa pwani kwa majaribio.

Aidha, Wizara imeanzisha utalii-ikolojia na mila kama shughuli mbadala kwenye maeneo ya misitu ya hifadhi ya Ziwa Duluti, Mlima Meru, Mlima Kilimanjaro, Shume-Magamba na kisiwa cha Toten katika Manispaa ya Tanga. Shughuli hizi zinalenga kuwapatia wanavijiji ajira, kuongeza kipato, na kuongeza ari ya kuhifadhi misitu. Katika mwaka 2005/2006, Wizara itaendelea kushirikisha vijiji katika hifadhi ya misitu ya lindimaji na mikoko, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya mazingira katika shule 60 na kupanda hekta 200 za mikoko katika maeneo yaliyoathirika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara ilielekeza juhudi katika kuboresha miundombinu ndani ya mapori ya akiba na katika maeneo yanayozunguka mapori hayo. Barabara mpya zenye urefu wa kilometa 410 zilijengwa kwenye mapori ya akiba ya Pande, Liparamba, Mpanga-Kipengere, Ugalla, Maswa na Rungwa. Aidha, barabara za zamani zenye urefu wa kilometa 341.7 zilifanyiwa ukarabati na kuwekewa alama za kudumu, mpango wa uendeshaji wa mapori ya akiba ya Ugalla na Mkomazi uliandaliwa. Vile vile, nyumba 103 za watumishi zimejengwa kwenye mapori ya akiba ya Swagaswaga, Lukwika-Lumesule, Rungwa-Kizigo-Muhesi, Usangu, Mpanga-Kipengere, Ugalla, Pande, Burigi-Biharamulo na Selous.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005/2006, Wizara itaendelea kupanua mtandao wa barabara katika mapori ya akiba kwa kulima kilometa 500 za barabara mpya na kukarabati barabara zenye urefu wa kilometa 500. Aidha, Wizara itakamilisha mipango ya uendeshaji kwa mapori ya akiba ya *Selous,* Moyowosi-Kigosi, Burigi-Biharamulo, Rukwa-Lukwati na Ibanda- Rumanyika na kuweka alama za kudumu katika mapori hayo.

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Taifa, Wizara ya Maliasili na Utalii inatoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa Taifa kwa kuchangia karibu asilimia 16 kwenye Pato la Taifa.

Katika mwaka 2004/2005, Wizara ililenga kukusanya shilingi bilioni 23.96. Hadi Mei, 2005, Wizara ilikusanya shilingi bilioni 28.0, hili ni ongezeko la asilimia 22 ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2003/2004, ambayo ni shilingi bilioni 22.92. Katika mwaka 2005/2006, Wizara itaongeza ada mbalimbali za uwindaji wa kitalii na kuongeza mapato ya Serikali kutoka Shilingi bilioni 10.7 za sasa hadi kufikia shilingi bilioni 12.0 kwa mwaka. Jumla ya shilingi bilioni 32.86 zitakusanywa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara iliendelea kusimamia uvuvi wa kibiashara wa kamba na samaki. Jumla ya tani 362,510 za samaki na tani 661.16 za kamba zilivuliwa katika msimu wa uvuvi 2004/2005. Aidha, matokeo ya sensa ya uvuvi iliyofanyika Ziwa Victoria yameonyesha kuwa ziwa hilo lina jumla ya wavuvi 76,749 walioandikishwa ambao wanatumia vyombo 22,272 vya uvuvi.

Katika kipindi cha 2005/2006, Wizara itaendelea kuboresha takwimu za uvuvi kwa kutoa mafunzo kwa wakusanyaji wa takwimu na kufanya sensa ya uvuvi katika ukanda wa pwani na Bwawa la Mtera.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara iliendeleza juhudi za kuboresha ukuzaji viumbe katika maji kwa lengo la kuinua kipato na kupunguza shinikizo la uvuvi kwenye maji ya asili. Mafunzo ya ufugaji bora wa samaki yaliyonufaisha Wananchi 1,320 katika mikoa ya Ruvuma, Kagera na Mara yalitolewa. Katika kuendeleza kilimo cha mwani kwenye mwambao wa Bahari ya Hindi, wadau 37 walipata mafunzo.

Katika kipindi cha 2005/2006, Wizara itaboresha ufugaji samaki kwa kufanya majaribio ya kufuga samaki aina ya perege na sangara kwenye uzio katika Ziwa Victoria. Aidha, Wizara itafanya majaribio ya kisayansi ya kuboresha mbegu ya samaki aina ya perege na kambale.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua mchango wa wavuvi wadogo wadogo katika sekta, Wizara imeendeleza juhudi za kuwajengea uwezo wa uzalishaji ili waweze kunufaika zaidi na rasilimali ya uvuvi.

Mwaka 2005/2006, Wizara itaanza kutekeleza mradi wa Uhifadhi wa Mazingira ya Bahari na Matumizi Endelevu ya Raslimali za Bahari *(Marine and Coastal Environment Management Project).* Mradi huo utajenga uwezo wa jamii ya wavuvi kwa kuwapatia mikopo ya kuendesha miradi midogo midogo. Aidha, mradi unalenga kuboresha usimamizi wa rasilimali zilizopo katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari *(Exclusive Economic Zone).*

Mheshimiwa Spika, mradi huu utatekelezwa kwa kipindi cha miaka sita kuanzia mwaka 2005 hadi 2011 na utagharimu kiasi cha dola za Kimarekani milioni 62.75. Kiasi cha dola milioni 52.0 zitatolewa na Benki ya Dunia kama mkopo na dola milioni 10.0

zitatolewa na *Global Environmetal Facility (GEF)* kama ruzuku. Serikali itachangia kiasi cha Dola milioni 0.75.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi, mwaka 2004/2005, Wizara ilichunguza sampuli 562 za matope, maji, samaki na minofu ya sangara kutoka Ziwa Victoria kuona kama kuna mabaki ya sumu. Aidha, sampuli 2,842 za minofu ya sangara zilichunguzwa ili kuhakiki kiwango cha vimelea haribifu. Wizara ilikagua na kuruhusu viwanda 18, maeneo 13, pamoja na maghala matano ya kuchakata na kutunzia mazao ya uvuvi. Aidha, meli 25 na vyombo vidogo sita vya uvuvi vilikaguliwa na kuruhusiwa kuvua kamba.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ukaguzi na uhakiki wa mazao ya uvuvi, watumishi 40 walipata mafunzo ya muda mfupi na wavuvi wadogo wadogo 1,520 walipata elimu kuhusu njia bora za uvunaji, uchakataji na uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi. Vituo vya ukaguzi katika Wilaya za Bukoba, Mwanza, Musoma, Mafia na Kilwa viliimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi. Maabara ya uvuvi Nyegezi imekamilika na itaanza kutumika baada ya kuweka vifaa vya uchunguzi wa kimaabara.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005/2006, viwanda 18 vya kuchakata mazao ya uvuvi na meli 31 za uvuvi vitakaguliwa. Sampuli 546 za samaki, 46 za matope na 92 za maji kutoka katika maeneo ya uvuvi katika Ziwa Victoria zitachunguzwa. Aidha, Wizara itaendelea kuhakiki ubora wa mazao ya uvuvi yanayosafirishwa nje ya nchi kwa kuyafanyia uchunguzi wa vimelea haribifu.

Mheshimiwa Spika, Utafiti wa Uvuvi unaendelea kufanyika kwa lengo la kubaini wingi wa rasilimali na kushauri kuhusu uhifadhi na matumizi endelevu.

Mwaka 2004/2005, Taasisi imefanya utafiti wa kutotoa vifaranga wa samaki aina ya kambale kutumika kama chambo kwa ajili ya uvuvi wa sangara katika Ziwa Victoria. Wavuvi 30 kutoka Wilaya za Magu na Sengerema wamepata ujuzi huo. Aidha, Taasisi itaendelea kutoa mafunzo kwa wavuvi wengi kwa lengo la kuwawezesha kujipatia chambo kwa gharama nafuu na kupunguza shinikizo la uvuvi wa samaki wachanga wanaotumika kama chambo.

Mheshimiwa Spika, Samaki Kisukuku *(Fossil Fish),* anayesadikika kuishi zaidi ya takriban miaka milioni 60 iliyopita na kuanza kupatikana katika maji ya Tanzania kwenye Bahari ya Hindi, amepewa jina rasmi la Kiswahili kuwa ni *Silikanti.* Taasisi imeingia Mkataba na taasisi moja ya Japan ili kufanya utafiti wa undani zaidi kuhusu *Silikanti* na mazingira yake.

Mwaka 2005/2006, Taasisi itaendelea na utafiti wa kamba ili kubaini wingi wa kamba na hatimaye kuwezesha Serikali kuamua idadi ya leseni zitakazotolewa kwa msimu ujao. Aidha, Taasisi itaendelea na utafiti katika Maziwa Makuu (Nyasa, Tanganyika na Victoria) na maziwa madogo, mabwawa na mito mikubwa ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara ilikamilisha utayarishaji wa mpango mkakati wa muda mrefu wa Taasisi. Wizara pia imekamilisha

mpango wa jumla wa usimamizi wa Hifadhi ya Ghuba ya Mnazi na Maeneo Tengefu ya Dar es Salaam, pamoja na mwongozo wa uwekezaji katika visiwa vidogo vidogo vilivyopo ukanda wa pwani. Aidha, Wizara ilikamilisha utayarishaji wa mkakati wa usimamizi wa utalii katika Hifadhi ya Ghuba ya Mnazi *(Integrated Tourism Framework).* Kwa kuzingatia umuhimu wa nishati katika maendeleo ya nchi, Wizara iliruhusu utafiti wa kina kubainisha wingi wa gesi iliyopo katika eneo la Hifadhi ya Bahari ya Ghuba ya Mnazi. Mwaka 2005/2006, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau kutekeleza mipango iliyoandaliwa katika kipindi cha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa uvunaji wa miti katika misitu ya asili unafanyika kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu, Wizara ilisitisha uvunaji nchi nzima kuanzia 1 Septemba, 2004. Usitishwaji huo ulitoa fursa kwa Wizara na Halmashauri za Wilaya kufanya mapitio ya taratibu za kuvuna miti ili kudhibiti uvunaji. Halikadhalika, orodha *(inventory)* katika misitu ya asili yenye hekta 13,507,350 unafanyika katika Wilaya 11 zenye maeneo makubwa ya misitu ili kubaini rasilimali zilizopo.

Hadi kufikia Machi, 2005, magogo yenye mita za ujazo 26,468 yalivunwa katika misitu ya asili. Magogo haya yanajumuisha yale yaliyovunwa kabla ya kusitisha uvunaji na yaliyovunwa kwa vibali maalum. Vile vile, mita za ujazo 352,990 zilivunwa katika mashamba ya miti. Aidha, Wizara ilikadiria kuwa Sekta Binafsi itauza mazao ya misitu nje ya nchi yenye thamani ya shilingi bilioni 10.9. Hadi kufikia Machi, 2005, mazao ya misitu yenye thamani ya shilingi bilioni 3.046 yaliuzwa. Mwaka 2005/2006, magogo yenye mita za ujazo 32,293 katika misitu ya asili na mita za ujazo 630,000 katika mashamba ya miti yatavunwa. Wizara inatarajia Sekta Binafsi kuuza mazao ya misitu nje ya nchi yenye thamani ya shilingi bilioni 11.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara iliendelea kusimamia mashamba 16 ya miti kwa kukuza miche milioni 7.4 na kupanda hekta 6,600 za miti. Taratibu za kushirikisha Sekta Binafsi kusimamia mashamba ya miti zimeanza kwa kupiga picha za anga ili kuchora upya ramani za mashamba ya *Sao Hill,* Kiwira, Buhindi, Meru na Kilimanjaro Kaskazini. Aidha, Wizara imeanza kutayarisha Mikataba ya makubaliano ya uendelezaji na usimamizi wa mashamba hayo. Katika mwaka 2005/2006, Wizara itakuza miche milioni 7,770,000 na kupanda miti hekta 5,917.

Ufugaji nyuki unachangia katika kuwapatia Wananchi kipato, ajira na lishe. Mwaka 2004/2005, Wizara ilifanya uhamasishaji wa ufugaji nyuki katika Vijiji vya Nyambulu, Mgeule, Zavala, Pugukajiungeni na Kiboga vinavyozunguka misitu ya Pugu, Kazimzumbwi na Zingiziwa. Katika kuinua viwango vya ubora wa mazao ya nyuki, mafunzo maalum yalitolewa kwa wadau mbalimbali katika Wilaya 11. Vile vile, Wizara iliwezesha vijiji vitatu katika Wilaya ya Manyoni na vijiji viwili katika Wilaya ya Uyui, kutenga maeneo na kuchora ramani za hifadhi za nyuki. Katika mwaka 2005/2006, Wizara itatoa huduma za ugani katika Wilaya 10 ili kupata mazao bora ya nyuki. Aidha, Wizara itaweka viwango vya ubora wa mazao ya nyuki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Taasisi ya Utafiti wa Misitu ilipanua na kuimarisha shughuli za utafiti wa kilimo misitu kwa kushirikisha wakulima katika Mikoa ya Pwani, Shinyanga, Mwanza, Tabora na Tanga. Vile vile, Taasisi ilipanda mashamba ya kuzalisha vyahuso *(cloning)* ya mikaratusi inayokua haraka katika vitalu vya majaribio vya Kingolwira (Morogoro), Kigwe (Dodoma), Lushoto, Kwamarukamda, Mombo na Korogwe (Tanga), Kibaha (Pwani), Ilkuruti (Arusha) na Mufindi (Iringa). Aidha, semina ya kuhamasisha wadau wa ndani na nje ya nchi kuhusu uzuri na athari za kupanda mikaratusi ilifanyika Dar es Salaam. Katika mwaka 2005/2006, Taasisi itaendeleza na kupanua utafiti wa mikaratusi, kilimo misitu, utambuzi wa miti na kuboresha miti kwa ajili ya mazao bora. Aidha, Taasisi itaanza ujenzi wa ofisi za makao yake makuu eneo la Kingolwira, Morogoro.

Mheshimiwa Spika, wakala wa mbegu za miti umeendelea kuzalisha na kusambaza mbegu bora za miti pamoja na vipandikizi. Hadi kufikia Aprili, 2005, Wakala ulikusanya kilo 10,500 za mbegu za miti, na kuuza kilo 9,490 nchini na kilo 20 nchi za nje. Vile vile, miche 9,875 ilisambazwa kwa wateja wa humu nchini. Katika kipindi cha 2005/2006, Wakala utaendeleza upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora za miti kwa kukusanya kilo 11,000 na kuuza kilo 11,000 nchini na kilo 55 nchi za nje, pamoja na kusambaza miche 13,000 humu nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendeleza ulinzi wa maisha na mali za Wananchi dhidi ya wanyamapori waharibifu. Mwaka 2004/2005, siku 1,322 za doria zilitumika kusaka wanyamapori wakali na waharibifu katika Wilaya 22. Aidha, risasi 2,251 zilitolewa katika Halmashauri za Wilaya 20 kwa ajili ya kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu. Askari Wanyamapori wa Vijiji *(Village Game Scouts)* 86 kutoka katika vijiji vilivyoko kwenye maeneo ya majaribio ya uhifadhi wa wanyamapori kwa jumuiya, walipewa mafunzo ya kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu. Askari hao waliendelea kushirikiana na Wizara pamoja na Halmashauri za Wilaya kufanya ulinzi dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliruhusu uwindaji wa mamba 1,500 kwa ajili ya kukabiliana na uharibifu wa wanyama hao kwa maisha ya watu na mali zao. Hadi Machi, 2005, mamba 1,331 waliwindwa katika maeneo yenye matukio ya mara kwa mara ya mamba kushambulia watu. Maeneo yaliyohusika ni pamoja na Mto Kilombero, Ruvu, Rufiji, Malagarasi, Ugalla, Ruhuhu, Pangani na Momba. Maeneo mengine ni Bwawa la Mtera na Nyumba ya Mungu pamoja na Ziwa Rukwa na Nyasa. Katika kipindi cha 2005/2006, Wizara itaendeleza ulinzi wa maisha na mali za Wananchi dhidi ya wanyamapori, kutoa elimu na kuhamasisha Wananchi walio katika maeneo yenye wanyama wakali na waharibifu jinsi ya kujikinga. Aidha, Wizara itaendelea kuruhusu uwindaji wa mamba katika maeneo yenye matatizo ili kuwaondolea wananchi kero.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa ardhioevu katika uhifadhi wa viumbe hai na mazingira, mwaka 2004/2005, Wizara ilifanya maandalizi ya Mkakati wa Kitaifa wa kusimamia ardhioevu na kukamilisha mpango wa Taifa wa kuhamasisha, kuelimisha na kuimarisha mawasiliano baina ya wadau wa ardhioevu. Vilevile, Wizara

ilifanya uhamasishaji wa uhifadhi katika maeneo ya ardhioevu yenye umuhimu wa Kimataifa *(Ramsar Sites)* ya Kilombero na Ziwa Natron. Maandalizi ya kuorodhesha vinamasi vya bonde la Mto Kagera yalianza.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005/2006, Wizara itakamilisha mkakati wa usimamizi wa ardhioevu na kuanza utekelezaji wake. Aidha, Wizara itakamilisha maandalizi ya kulitangaza eneo chepechepe la Mto *(Kagera Floots)* kuwa eneo la ardhioevu lenye umuhimu wa kimataifa na kuandaa na kutekeleza mpango kamambe wa usimamizi wa *Ramsar Sites* za Ziwa Natron na Bonde la Mto Kilombero.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa wanyamapori uliendelezwa ili kubaini magonjwa na kutathmini wingi wa raslimali. Katika kipindi cha 2004/2005, Taasisi ilifanya sensa za kawaida za wanyamapori katika maeneo ya Hifadhi za Taifa za Tarangire na Manyara na Mapori ya Akiba ya Saadani, Moyowosi na Kigosi. Sensa ya ndege wa majini ilifanyika nchi nzima mwezi Januari hadi Februari 2005. Utafiti wa kwaru manjano *(Fischer's Lovebirds)* ulifanyika katika mikoa ya Arusha, Manyara, Shinyanga, Singida na Tabora. Aidha, Taasisi ilifanya utafiti wa masoko ya mazao ya nyuki katika mikoa 12. Vilevile, Taasisi iliendesha mafunzo ya ufugaji nyuki kwa wafugaji wa Wilaya za Monduli, Arumeru na Manispaa ya Arusha. Taasisi ilikamilisha ukarabati wa baadhi ya majengo ya Kituo cha Utafiti cha Tabora pamoja na jengo la ofisi na nyumba ya watafiti katika Kituo cha Utafiti cha Kingupira katika Pori la Akiba la Selous. Ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Taasisi huko Njiro, Arusha unaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2005/2006, Taasisi itaendelea kuhesabu wanyamapori ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Pia, itaendesha tafiti za mbwa mwitu katika maeneo ya Serengeti na Ngorongoro na mahusiano ya tembo na watu katika maeneo ya magharibi mwa Hifadhi ya Serengeti. Aidha, Taasisi itakamilisha utafiti wa masoko ya mazao ya nyuki katika mikoa yote nchini na kuendesha mafunzo mbalimbali ya ufugaji nyuki kwa njia za kisasa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, mfuko ulikusanya shilingi bilioni 4.4. Fedha hizo zilitumika kuimarisha doria, utafiti na mafunzo ya uhifadhi. Mfuko pia uligharamia kazi za maendeleo katika mapori ya akiba na baadhi ya miradi ya ushirikishaji wa Wananchi katika uhifadhi. Mwaka 2005/2006, Mfuko unatarajia kukusanya shilingi bilioni 4.5.

Mheshimiwa Spika, Shirika liliendelea kusimamia uhifadhi wa maliasili na mazingira; kufanya doria na kuangalia mwenendo wa shughuli za utalii ndani ya hifadhi. Mwaka 2004/2005, Shirika liliendelea kuandaa mipango ya uendeshaji ya Hifadhi za Serengeti, Mahale, Kilimanjaro na Mikumi. Katika kipindi cha Julai 2004 hadi Machi 2005, idadi ya watalii iliongezeka kwa asilimia 39.9 ambapo watalii 466,891 walitembelea Hifadhi za Taifa ikilinganishwa na watalii 334,341 wa mwaka 2003/2004. Ongezeko hili limechangiwa kwa kiasi kikubwa na juhudi za kutangaza utalii hapa nchini na nje ya nchi. Watalii hao waliliingizia Shirika mapato ya shilingi bilioni 26.9 ikiwa ni ongezeko la asilimia 46.6. Aidha, Shirika lilitoa Sh.601,932,514.92 kuchangia maendeleo ya Wananchi wanaozunguka hifadhi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2005/2006, Shirika litaendelea kuandaa mipango ya uendeshaji ya hifadhi, kuimarisha doria, kuboresha miundombinu kwa ajili ya utalii na kutekeleza miradi ya maendeleo ya ujirani mwema. Aidha, Shirika litaendelea kushiriki kwenye maonyesho mbalimbali ya utalii pamoja na kupanua wigo wa shughuli za watalii kwa lengo la kuvutia watalii zaidi kuzitembelea hifadhi.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka iliendelea kusimamia eneo la Ngorongoro linalojumuisha hifadhi ya wanyamapori na makazi ya watu. Hadi kufikia Machi, 2005, watalii 246,261 walitembelea Hifadhi ya Ngorongoro. Kati ya hao 175,272 walitoka nje ya nchi na 70,989 ni watalii wa ndani. Idadi hii ni ongezeko la watalii 26,500 sawa na asilimia 12.1 ikilinganishwa na watalii 219,761 waliotembelea Ngorongoro katika kipindi cha 2003/2004. Watalii hao waliingizia Mamlaka Shilingi bilioni 10.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 8.5 mwaka 2003/2004. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 23.5. Katika kipindi cha 2005/2006, Hifadhi ya Ngorongoro inatazamia ongezeko la asilimia 10 ya watalii ambao wanatazamiwa kuingiza shilingi bilioni 12.0.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeendelea kuchangia maendeleo ya Wananchi kwa kununua mashine ya kufyatulia matofali yasiyochomwa katika Wilaya ya Karatu, kujenga madarasa manne na nyumba moja ya mwalimu katika Shule ya Sekondari Embarway. Mamlaka imepata kiwanja Mjini Arusha kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kitega uchumi. Aidha, Mamlaka imejenga nyumba saba za watumishi na imepata shamba mjini Karatu kwa ajili ya kujenga nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2005/2006, Mamlaka itaanza kujenga jengo la kitega uchumi Mjini Arusha na kutengeneza barabara ya Osinoni-Kakesio. Pia, itajenga shule mpya ndani ya Tarafa ya Ngorongoro na kuweka umeme wa Gridi ya Taifa katika eneo la Hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utalii umechukua nafasi muhimu katika maendeleo ya uchumi wa Taifa letu, hasa katika kuchangia fedha za kigeni. Watalii waliongezeka kutoka 295,312 mwaka 1995 hadi 582,807 mwaka 2004, ikiwa ni wastani wa ongezeko la asilimia 10 kwa mwaka. Hali kadhalika, mapato yatokanayo na utalii yaliongezeka toka Dola za Kimarekani milioni 259.4 mwaka 1995 hadi milioni 746.0 mwaka 2004. Hadi kufikia mwaka 2004 Sekta ya Utalii ilikuwa imetoa ajira kwa watu wapatao 199,000.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara ilibaini vivutio na maeneo ya uendelezaji utalii katika mikoa ya Ruvuma na Kagera na kuandaa picha za video kwa maeneo ya Singida na Mtwara. Aidha, Wizara ilianza maandalizi ya programu ya uendelezaji utalii ambayo ni mpango wa utekelezaji wa Sera ya Utalii. Pamoja na mambo mengine, mpango huu utaainisha na kuweka bayana zaidi dhima ya wadau mbalimbali katika uendelezaji utalii na kuweka muda wa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara ilitoa mafunzo kuhusu tathmini ya athari kwa mazingira, uwezo wa kustahimili ongezeko la watalii na utalii ikolojia. Mafunzo haya yalitolewa kutokana na msukumo wa kuvutia uwekezaji Kanda ya Kusini ya utalii na kwa lengo la kuweka mazingira ya utalii endelevu nchini. Maafisa Maliasili

37 kutoka Wilaya ya Bagamoyo na Wilaya zote za mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma na Iringa walinufaika na mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2005/2006, Wizara itakamilisha maandalizi ya programu ya uendelezaji utalii ambayo itaainisha dhima ya kila sekta katika utekelezaji wa Sera ya Utalii. Hatua hii itaharakisha na kurahisisha utekelezaji wa sera. Aidha, Wizara itabaini vivutio na maeneo ya uwekezaji katika mikoa ya Rukwa, Morogoro na Pwani na kufanya semina za uhamasishaji kuhusu utalii ikolojia na utalii wa utamaduni katika mikoa mitatu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara ilikuwa mwenyeji wa semina ya kimataifa kuhusu uendelezaji utalii endelevu na kupunguza umaskini. Semina hii ilihudhuriwa na washiriki 163 kutoka nchi 12, ambapo washiriki 130 walikuwa Watanzania kutoka Sekta ya Umma na Binafsi. Aidha, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa mikutano ya *Regional Tourism Organisation of Southern Africa,* pamoja na kushiriki mikutano ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Katika kipindi cha 2005/2006, Wizara itafanya vikao viwili vya *Tourism Facilitation Committee* na mkutano mmoja wa mashirikiano na Zanzibar. Aidha, itaendelea kudumisha ushirikiano wa Kitaifa na Kimataifa katika utalii na kuhakikisha kuwa maslahi ya Taifa yanazingatiwa na kulindwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma, ilikamilisha taratibu za kubinafsisha hoteli zilizokuwa chini ya Wizara. Aidha, Wizara inaendelea kutafuta ufumbuzi wa matatizo yaliyojitokeza katika kubinafsisha Loji ya Mikumi na Hoteli ya Saba Saba. Vile vile, kupitia Kituo cha Uwekezaji wa Rasilimali nchini, miradi mipya 56 ya utalii imepitishwa. Katika juhudi za kukuza na kuimarisha uwekezaji katika Sekta ya Utalii nchini, mwaka 2004/2005, Wizara imeanzisha programu ya kuongeza nguvu za mitaji kwa wawekezaji wa ndani kwa kuwaunganisha na wale wa nje. Aidha, programu hiyo inatangaza fursa za uwekezaji katika Sekta ya Utalii nchini kupitia makongamano mbalimbali ya uwekezaji duniani.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara iliendesha warsha kwa wadau 140 kuhusu vigezo vya kupanga hoteli katika madaraja kwenye Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Mwanza. Zoezi la kupanga hoteli katika madaraja limeanza kwa kuhakiki hoteli katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Manyara, Arusha na Kilimanjaro. Katika Mwaka 2005/2006, Wizara itaendelea na zoezi la kuhakiki hoteli katika mikoa 10.

Mheshimiwa Spika, Bodi imeendelea na jukumu la kutangaza utalii ili kuharakisha ukuaji wa Sekta ya Utalii. Katika kipindi cha 2004/2005, Bodi ilishiriki katika maonesho ya utalii 24 ndani na nje ya nchi. Aidha, Tanzania ilijitangaza kwa mara ya kwanza katika soko jipya la China ambalo lina matumaini makubwa. Vile vile, Bodi ilizindua tovuti mpya *http://www.tanzaniatouristboard.com,* ambayo imerahisisha kufikisha taarifa kwa wadau. Bodi inaandaa mkakati wenye mwelekeo mpya wa kutangaza utalii ndani na nje ya nchi. Mwaka 2005/2006, Bodi itaendeleza ushirikiano na Sekta Binafsi na Taasisi nyingine katika kukuza utalii wa ndani ikiwa ni pamoja na

utalii wa fukwe, utalii wa majini na utalii wa kitamaduni. Jitihada pia zinaelekezwa katika kuendeleza masoko mapya kama vile China, Urusi, Japan, Korea na Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa mafunzo ya utalii umepewa kipaumbele ili kukabiliana na ushindani uliopo katika biashara ya utalii. Katika mwaka 2004/2005, Wizara imeanza taratibu za ujenzi wa Chuo cha Taifa cha Utalii. Chuo kitapokamilika kitakuwa na uwezo wa kutoa wahitimu 500 wa ngazi ya stashahada kwa mwaka katika fani mbalimbali za usimamizi wa hoteli na utalii. Katika kipindi cha 2005/2006, Wizara itaendeleza ujenzi wa chuo hicho ambacho kitajengwa katika Mtaa wa Shaaban Robert, Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea na jukumu la kulinda, kutafiti na kuhifadhi urithi wa Mambo ya Kale. Mwaka 2004/2005, maandalizi ya kujenga sehemu ya kumbukumbu na taarifa katika vituo vya Ujiji (Kigoma), Kilwa Kisiwani (Lindi) na Kaole (Pwani) yalikamilika na ujenzi utaanza katika mwaka 2005/2006. Aidha, Wizara inatarajia kuweka wazi mipaka ya eneo la kituo cha mapango ya Amboni, Mkoani Tanga. Katika kipindi cha 2004/2005, Wizara ilikarabati magofu ya Husuni Kubwa na msikiti mdogo, pamoja na kuandaa kitabu cha mwongozo kwa eneo la Kilwa Kisiwani. Aidha, Wizara iliandaa mpango wa uendeshaji wa Kilwa Kisiwani na Songo Mnara. Aidha, Wizara ilifanya utafiti wa akiolojia wa kuboresha historia ya eneo hilo na Wilaya ya Kilwa kwa ujumla. Mwaka 2005/2006, Wizara itaendelea kukarabati na kuimarisha magofu na majengo ya kale katika maeneo ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara iliandaa programu ya kuboresha njia ya kati ya biashara ya utumwa na vipusa, pamoja na uhifadhi wa Mji Mkongwe wa Bagamoyo ili viingizwe kwenye orodha ya urithi wa dunia. Mwaka 2005/2006, Wizara itaanza utekelezaji wa programu hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara ilifanya utafiti wa akiolojia kwenye mireshe Wilayani Moshi, eneo la Kola, Morogoro Mjini na Morogoro Vijijini huko Kinole. Aidha, Wizara imeanza maandalizi ya kutafiti njia kuu ya biashara ya utumwa na vipusa iliyopitia nchini mwetu ikijumuisha Bagamoyo Mkoani Pwani hadi Ujiji mji wa mpakani magharibi mwa Tanzania, Mkoani Kigoma. Aidha, Wizara iliratibu na kusimamia tafiti za akiolojia huko Mkiu, Wilaya ya Mkuranga; Sonjo na Engaruka Wilaya ya Monduli; Wilaya ya Kilwa, Wilaya ya Bagamoyo na Mkoa wa Dar es Salaam, Peninj na Natron Wilaya ya Monduli.

Mwaka 2005/2006, Wizara itaendelea kufanya utafiti wa akiolojia kwenye mireshe, Wilaya ya Moshi Vijijini. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia tafiti za akiolojia zitakazofanywa na watafiti mbali mbali wa ndani na nje ya nchi kwa mujibu wa sheria na kanuni.

Mheshimiwa Spika, Dira ya Shirika ni kuwa mojawapo ya vituo vya kutukuka katika uhifadhi endelevu wa urithi wa utamaduni na maliasili. Katika juhudi za kujitangaza, mwaka 2004/2005, Shirika lilizindua tovuti yake *http://www.museum.or.tz,*

pamoja na Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Aidha, Vituo vya Makumbusho ya Elimu Viumbe Arusha na Dar es Salaam viliboreshwa kwa kufanyiwa ukarabati. Katika mwaka 2005/2006, ukarabati utaendelezwa kwa kituo cha Makumbusho ya Azimio la Arusha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Shirika lilihamasisha jamii za Wairaqw na Wakerewe kufanya tamasha la Siku ya Utamaduni wa Mtanzania. Mwaka 2005/2006, Shirika litaendelea kuhamasisha na kuzishirikisha jamii za Mkoa wa Singida ziweze kuandaa tamasha lao. Shirika lilianza maandalizi ya kutekeleza mradi wa Nyumba ya Utamaduni kwa kuandaa michoro ya jengo na kufanya warsha tatu za wadau za kutayarisha dira pamoja na mpango mkakati wa mradi huo. Vilevile, kupitia mradi huo, ukumbi wa maonyesho ya Historia uliboreshwa. Katika kipindi cha 2005/2006, Mradi wa Nyumba ya Utamaduni ambao ni wa miaka mitatu utaanza kutekelezwa na kuboresha huduma zinazotolewa na Shirika la Makumbusho ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Shirika lilifanya utafiti wa awali wa viumbe wa bahari katika ukanda wa maji kupwa na kujaa Kisiwani Mafia. Katika utafiti huo, aina mbalimbali za viumbe wasio na uti wa mgongo walikusanywa, kutambuliwa na kuhifadhiwa katika Makumbusho ya Taifa kwa ajili ya rejea. Katika mwaka 2005/2006, Shirika litaendeleza utafiti wa viumbe bahari.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kutambua umuhimu wa watumishi katika kufanikisha utendaji, ilipata kibali cha kuajiri watumishi 152. Hadi Aprili, 2005, Wizara iliajiri watumishi 127 na nafasi 25 zilizobaki hazikujazwa kwa kutopatikana watu wenye sifa na taaluma stahili. Katika kushughulikia tatizo hili, Wizara imeanza kugharimia wanafunzi watarajali *(pre-service)* katika taaluma za uvuvi, wanyamapori, misitu na ufugaji nyuki. Hatua hii inakusudia kuhakikisha kuwa Watanzania wenye taaluma hizo wanapatikana ili kuwezesha Serikali na Sekta Binafsi kupata watu wenye sifa zinazotakiwa. Katika mwaka 2005/2006, Wizara itaajiri watumishi wapya 142, baada ya kupata kibali toka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara ilitarajia kuwapandisha vyeo watumishi wa kada mbalimbali 326 kwa kufuata utaratibu mpya wa ushindani. Hadi Mei 2005, watumishi 286 wamepandishwa cheo. Mwaka 2005/2006, watumishi 350 watapandishwa cheo kwa utaratibu huo wa ushindani. Lengo ni kutatua tatizo la watumishi waliokaa katika cheo kimoja kwa miaka mingi bila kupandishwa cheo.Wizara imeweka mkakati wa kuimarisha mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2004/2005, watumishi 548 wamepata mafunzo.

Mwaka 2005/2006, Wizara inatarajia kutoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi 669 na itaendelea kuhamasisha watumishi wake kujiendeleza kitaaluma. Aidha, Wizara itaendelea kuwapatia watumishi mafunzo ya muda mrefu na mfupi ili kuongeza ufanisi katika utendaji na kwa kuzingatia mpango wa mafunzo uliopitishwa kwa watumishi wote. Ili kukabiliana na tatizo la watumishi wasiokuwa na sifa kwa mujibu wa miundo yao ya kiutumishi, Wizara imeanza kupeleka watumishi hao katika vyuo mbalimbali ili kuwawezesha kupata sifa zinazostahili. Aidha, katika mwaka 2005/2006, Wizara itaanza kutekeleza Mpango wa Mafunzo kwa Watumishi wake wote.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha ustawi wa watumishi, Wizara imehamasisha watumishi kuendelea kuchukua mikopo kutoka Taasisi mbalimbali ili kuinua hali yao ya maisha, hususan katika kujijengea nyumba za kuishi na kulipia gharama za elimu kwa watoto wao. Ili kudumisha mahusiano mazuri na kujenga afya, wafanyakazi wamekuwa wakishiriki katika michezo mbalimbali inayoandaliwa Kiwizara na Kitaifa. Aidha, katika kujenga uwezo wa watumishi kimichezo, Wizara ilipeleka watumishi watatu kujifunza ukocha katika kituo cha mafunzo cha Malya Mkoani Mwanza.

Katika mwaka 2004/2005, Wizara iliendelea kuboresha vyuo vyake kwa kukarabati majengo, kuboresha mitaala pamoja na kuvipatia vifaa vya kufundishia ili kukidhi mahitaji ya soko. Vyuo viko katika hatua mbalimbali za kupata usajili wa kudumu kutoka Baraza la Taifa la Usajili wa vyuo vya Elimu na Ufundi *(NACTE).* Chuo cha Misitu Olmotonyi na Vyuo vya Uvuvi Mbegani na Nyegezi vimepata usajili wa muda. Aidha, Chuo cha Uvuvi Nyegezi, kinaandaa mtaala mpya kwa ajili ya kupata usajili kamili. Mwaka 2005/2006, Wizara itaendeleza taratibu za usajili, kuboresha na kuongeza vitendea kazi pamoja na kupitia mitaala ili kukidhi mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa viongozi na watumishi ikiwa ni hatua ya kujenga uwezo wao katika utendaji unaozingatia misingi ya Utawala Bora. Katika mwaka 2004/2005, watumishi 130 walipata mafunzo ya Huduma kwa Mteja, 50 masuala ya jinsia na 20 mbinu za kuendesha mikutano. Katika kipindi cha 2005/2006, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi katika ngazi mbalimbali ili kuimarisha Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, kama kila mmoja wetu anavyofahamu, Ukimwi umekuwa janga na tishio kubwa kwa Taifa letu. Katika jitihada za kupambana na janga hili, Wizara katika mwaka wa 2004/2005, imeanza kutekeleza mkakati wa kudhibiti Ukimwi miaka mitatu (2004 - 2007). Lengo la mkakati huo ni kuhakikisha Wizara inachukua hatua za kudhibiti kuenea kwa Ukimwi miongoni mwa wafanyakazi wake na wadau wengine. Aidha, katika mwaka 2004/2005, Wizara iliandaa na kutoa mafunzo ya Waelimishaji Rika na Ushauri Nasaha, Upimaji wa Hiari wa Ukimwi na Kamati ya Ushauri ya Ukimwi ili kujenga uwezo wa Wizara katika kupambana na janga hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho, jitihada za kuleta ufanisi katika Wizara yangu, zimefanyika kwa ushirikiano na wadau mbalimbali. Napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, Wananchi na wote waliotoa ushirikiano katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Vile vile, natoa shukrani kwa washirika wetu wa maendeleo kwa michango yao ya kifedha na kitaalamu kama ifuatavyo: Denmark, Finland, Japan, Norway, Marekani, Ufaransa, Ubelgiji, Ujerumani, Sweden, Jumuiya ya Nchi za Ulaya, *ADB, AWF, FAO, FZS, GTZ, IUCN, KfW, Trade Aid, MIGA, AFRICARE, UNESCO, UNDP, World Bank, WWF, ICCROM* na mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani kwa Katibu Mkuu, Bwana Salmon Odunga, viongozi na watumishi wa Wizara, Taasisi, Mashirika na Wakala, kwa

ushirikiano walionipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa mwaka 2004/2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu, naomba Bunge lako Tukufu, liidhinishe makadirio ya matumizi ya shilingi 55,442,163,500. Kiasi hicho kinajumuisha fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo Sh.22,471,839,500.00 na kwa Matumizi ya Kawaida Sh.32,970,324,000.00

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. LUCAS L. SELELII (k.n.y. MHE. ANNE S. MAKINDA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu Na. 81 (1) cha Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, kuhusu utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2004/2005, pamoja na maoni juu ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba ya Kamati yangu, nachukua fursa hii kwa masikitiko makubwa, kuwapa pole za dhati, familia na Wananchi wa Mkoa wa Rukwa, kwa kufiwa na mpendwa Mbunge waom Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, tarehe 23 Juni, 2005. Pia nachukua nafasi hii kuwapa pole, familia na Wananchi wa Jimbo la Kilombero, Mkoani Morogoro, kwa kufiwa na Mbunge wao, Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, kilichotokea tarehe 2 Juni, 2005. Mwenyezi Mungu, aziweke roho za Marehemu hawa mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, napenda kuuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumpongeza kwa dhati, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwake na Chama hicho kupeperusha bendera ya Chama cha Mapinduzi katika kinyang'anyiro cha Urais katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba, 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati yameanishwa katika Kanuni Na. 101 (2), ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004. Majukumu hayo ni pamoja na kushughulikia Bajeti za Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Kuondoa Umaskini na Shughuli za Muungano) na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari, Kamati ilitoa ushauri na mapendekezo yake baada ya kuelezwa kwa kina kuhusu mambo yafuatayo: Dira ya Wizara ya Maliasili na Utalii; Muundo wa Wizara; majukumu ya Wizara; utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa mwaka 2004/2005; mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya mwaka 2004/2005; na Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kutekeleza ipasavyo, maagizo karibu yote, ambayo ilipewa na Kamati mwaka 2004/2005. Kamati imeridhishwa na maelezo, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Wizara ambayo ilitembelewa na Wajumbe wa Kamati katika kipindi cha mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli ya Sh. 24,976,671,000/= kwa mwaka 2004/2005, hadi Aprili, 2005 ilikuwa imekusanya jumla Sh. 26,904,247,296/=, zaidi ya asilimia 100. Kamati inaipongeza sana Wizara kwa juhudi hizi. Wakati huo huo Kamati imeridhika na matumizi ya Wizara ambayo hadi kufikia Aprili, 2005, ilikuwa imetumia asilimia 73 ya makadirio ya matumizi ya mwaka mzima wa 2004/2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2004/2005, Kamati inaipongeza Wizara katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kwanza, wameandaa hadidu za rejea *(TOR)* kwa ajili ya kufanya hesabu ya maeneo ya ardhioevu/chepechepe;

(ii) Kupanga mapitio ya rasimu za Kanuni za uvuvi za Zanzibar na Tanzania Bara kwa lengo la kuoanisha kanuni hizo, kwa kushirikisha wadau wa kutoka pande zote mbili; *(Makofi)*

(iii) Warsha ya kujadili na kupokea maoni kuhusiana na rasimu ya sera ya mambo ya kale zilifanyika katika kanda ya kati - Tabora, Kanda ya Kusini - Lindi, Kanda ya Nyanda za Juu - Mbeya na Kanda ya Ziwa - Mwanza; *(Makofi)*

(iv) Warsha ilifanyika Dar es Salaam na Arusha kuhusu kutengeneza Kanuni za sheria ya utalii;

(v) Kuweka mazingira mazuri ya kuwawezesha wadau kushiriki kikamilifu katika uhifadhi wa maliasili, mambo ya kale na vivutio vya utalii kwa mfano, kufanya hesabu ya rasilimali za misitu *(Forest Inventory)* katika Wilaya 11; timu ya watalaamu iliundwa kupanga madaraja ya mahoteli; hifadhi nane za nyuki zilitambuliwa katika Wilaya za Tabora, Manyoni na Handeni na vijiji vinne vilisaidiwa kutengeneza mipango ya usimamizi wa hifadhi ya nyuki;

(vi) Kulinda maliasili, mambo ya kale na vivutio vya utalii dhidi ya matumizi haramu kwa kufanya yafuatayo: Ulifanyika udhibiti wa wanyama waharibifu katika Wilaya nane ambazo zimeathirika sana na wanyamapori; kaguzi 713 zilifanyika katika kusimamia ubora wa mazao yatokanayo na uvuvi katika sampuli 341 za minofu ya samaki; Wizara imefanikiwa kuimarisha na kuendeleza ushirikiano ndani na nje ya nchi na wamefanikiwa kuboresha huduma kwa wateja kwa kufanya mikutano na wadau wa sekta zilizopo chini ya Wizara ili kufanya mapitio ya Mkataba wa huduma kwa mteja; na

(ix) Semina mbalimbali zimefanywa ili kuimarisha uongozi unaojali Utawala Bora na wenye kuwajibika. Kamati imeshuhudia mabadiliko makubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo hivyo, sekta hii imeanza kukua kwa kasi kubwa. Katika kuongeza Pato la Taifa, sasa inakua kwa wastani wa asilimia 6 - 7 kwa mwaka na kuchangia asilimia 16 kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha dhana nzima za kutumia kikamilifu rasilimali hii ya maliasili na mambo ya kale katika utalii, Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

(i) Kuna umuhimu kwa Serikali kuendeleza juhudi za kulinda wanyamapori wetu wasiuawe ovyo na majangiri. Wale wanyama ambao wanaendelea kutoweka, walindwe kufuatana na Mikataba ya Kimataifa ya *CITES.* Kampuni za uwindaji zisimamiwe ili kuepuka kuwinda wanyama zaidi ya wale walioruhusiwa. Mapato kutokana na Makampuni hayo yasimamiwe hasa ukizingatia kuwa, upo upungufu mkubwa wa uaminifu katika maeneo haya; *(Makofi)*

(ii) Misitu na nyuki ni eneo ambalo Wananchi wengi wangeweza kushiriki na kujiondolea umaskini wa kipato. Hatua ambazo Wizara imeanza kuchukua kuwasaidia Wananchi kutengeneza mipango ya Usimamizi wa Hifadhi za Nyuki, ziendelezwe kwa kasi kubwa. Wakati huo huo utambuzi wa masoko ya uhakika ya mazao yatokanayo na nyuki ufanyike. Masoko yatatuwezesha kujua ni mambo gani yafanyike ili Wananchi wafaidike na mazao ya nyuki. Wizara iendeleze juhudi za kufanya hesabu ya rasilimali za misitu. Hii itawezesha kujua ni utajiri gani upo kwenye misitu yetu, miti ya aina gani ipo na idadi yake;

Mazao ya misitu pia huweza kuwaondolea Wananchi umaskini wa kipato, tukihakikisha kuwa magogo yanavunwa kwa utaalamu na kwamba badala ya kusafirisha magogo nje ya nchi, tusafirishe bidhaa zilizotengenezwa hapa hapa nchini. Kwa kufanya hivyo, ajira kwa Wananchi zitapatikana kuliko biashara ya kusafirisha magogo nje ya nchi. Vilevile tunawapongeza wafanyabiashara Wazalendo wa magogo, kwa kuanzisha umoja wao kama ambavyo walishauriwa na Kamati. Wametumia umoja huu kushauriana na Serikali, basi watumie umoja huu huu kuendeleza sekta hii kwa kuanzisha viwanda vya kutengeneza bidhaa zitokanazo na magogo hapa hapa nchini;

(iii) Eneo la uvuvi pia Serikali imeanza kuchukua hatua mbalimbali kuliboresha. Wananchi wafundishwe na kusaidiwa kuanzisha ufugaji wa samaki, kwa ajili ya matumizi ya chakula na biashara ndani ya nchi na wakati huo huo kuendelea na juhudi za kuzuia uvuvi haramu katika bahari na maziwa, kwa kuwashirikisha wadau, kama ambavyo inafanyika katika Mpango wa Ziwa Victoria wa hifadhi ya mazingira *(LEVMP)* na Mpango wa Hifadhi ya Bahari *(TCMP).* Katika mipango hii miwili, ushirikishwaji wa Wananchi ni muhimu sana, kwani kinachofanyika ni kuwafanya Wananchi watumie njia bora zaidi za uvuvi ili kuhifadhi mazingira ambayo samaki wanataga mayai. Katika maeneo mengine Wananchi wanatakiwa wasiendeleze uvuvi kabisa kwani ni sehemu ya mazalia ya samaki;

Wananchi wa maeneo hayo inabidi washirikishwe kikamilifu katika kubuni namna mbadala ya kuendesha maisha. Uvuvi kwa kutumia baruti na sumu upigwe marufuku kabisa. Idara ya Uvuvi haina budi kushirikiana na watalaamu waliopo kwenye miradi hii, wote wafanye kazi kwa mkazo mmoja katika kusimamia sheria hii. Kamati imejifunza kuwa, Idara ya Uvuvi haina nyenzo za kisasa katika kudhibiti uvuvi haramu katika maeneo yao hivyo, kuwafanya washindwe kutimiza wajibu wao ipasavyo. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha Idara hi inapata nyenzo za kisasa ili kukabiliana na tatizo la uvuvi haramu;

(vi) Kamati imeridhishwa na hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Wizara katika kuboresha urithi wa asili wa mambo ya kale ikiwemo hatua ya kukusanya maoni kutoka kanda mbalimbali za nchi kuhusu rasimu ya sera ya mambo ya kale. Mategemeo ya Kamati ni kuwa, rasimu hii itakamilishwa haraka ili shughuli mbalimbali katika eneo hili, ziweze kutambuliwa na Serikali na kupewa Bajeti ya kuridhisha; na

(v) Tunapenda kuipongeza Wizara kwa hatua mbalimbali inazochukua katika kuinua utalii nchini, zikiwemo zile za kupanga madaraja ya mahoteli.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuongezeka kwa utalii siku za hivi karibuni, bado mahoteli yetu yapo kwenye hali isiyoridhisha. Makao Makuu ya Mikoa na Wilaya, hayana hoteli ambazo wageni wanaweza kufikia na kuridhika na huduma zake. Hoteli zetu nyingi ni chafu sana, zina wahudumu ambao hawana lugha ya ukarimu na chakula hakivutii wateja hata kidogo. Matokeo yake, wateja badala ya kukaa muda mrefu, wanaomba waondoke siku ya pili huku wakilaani kabisa hali hii. Pamoja na kwamba, Serikali itaanzisha Chuo cha Mambo ya Utafiti na Mahoteli, Wizara haina budi kukagua hivyo vyuo vya watu binafsi, ambavyo vinafundisha mambo ya mahoteli ili tuwe na viwango *(standards),* vya kuanzia. Wakati huo huo wale wanaotoa leseni za kufungua hoteli wakague iwapo hoteli hizo zinakidhi viwango vya hoteli. Mabwana Afya pia wasiache mahoteli kuwa na hali mbaya katika maeneo yao ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa nchi yetu inatembelewa na wageni wengi, lakini huduma za mahoteli mengi haziridhishi na hazikidhi maslahi ya wageni hao, ukianzia kwenye malazi hata chakula. Hivyo, Wizara iwe na utaratibu wa kuzitambua hoteli hizi na kuzielekeza kuhusu huduma wanazotakiwa kutoa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kwa niaba ya Kamati, kumshukuru Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii, Katibu Mkuu wake, Bwana Salmon Odunga, watumishi wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii, kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati katika kipindi chote ambacho tumefanya kazi nao. Wametupa elimu kubwa sana wakati wa semina na wakati ambapo tulitembelea shughuli zao. Kwa kweli tunamaliza muda wetu wa Ubunge tukiwa tumeelimika zaidi kupitia Wizara hii. Wizara hii inao watalaamu waliobobea sana katika maeneo yao. Kutokana na utaalam ambao Wafanyakazi/Watumishi hao wanao, ni chachu tosha ya kuondoa umaskini nchini. Tukijipanga vizuri, utaalamu huu utaondoa umaskini uliopo kwa kila mtu kutimiza wajibu wake pale alipo. Wakati huo huo kutanguliza Taifa letu kwanza. Kamati yangu inawashukuru sana na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina budi kwa niaba ya Kamati, kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Ofisi yako, kwa kufanikisha shughuli zetu kama Kamati na kama Wabunge, kwa miaka yote tuliyokuwa hapa Bungeni. Namshukuru pia Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka, Makatibu wa Kamati, Ndugu Frank Mbumi na Ndugu Michael Kadebe, wamekuwa msaada mkubwa kwa Kamati. Kwa namna ya pekee, tunamshukuru sana Bwana Sam A. Manamba, aliyekuwa Katibu wa Kamati hadi kustaafu kwake mwezi wa Aprili, 2005. Tunamtakia afya na maisha mema katika maisha hayo ya ustaafu. *(Makofi)*

Napenda kutumia nafasi hii, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, kwa ushirikiano wa hali ya juu, ambao walinipa mimi tangu wanichague hadi hivi leo. Bila ushirikiano wao, tusingeweza kufika hapa. Kwa umoja na upendo wao mkubwa sana, tunamaliza kipindi chetu kama familia moja iliyojaa upendo na kusaidiana katika matatizo mbalimbali. Kazi yangu ilikuwa nyepesi kutokana na ushirikiano huo wa kipekee. Ningekuwa na Mamlaka ningependa kabisa Wajumbe wote twende kwenye uchaguzi halafu wote tushinde, turudi Bungeni na wote tundelee na Kamati hii hii. Bahati mbaya hizi ni *wishful thinking* tu. Pamoja na mshikamano wenu kama binadamu, inawezekana nimekuwa nawakwaza bila kujijua, naomba mnisamehe kwa mapungufu hayo, nia yangu ilikuwa njema, katika kufanya maamuzi mbalimbali. *(Makofi)*

Napenda pia nichukue nafasi hii, kuwashukuru Wabunge wote na Mawaziri wote, kwa misaada mbalimbali ambayo mlinipa mimi kama Mbunge, lakini pia kama Mwenyekiti wa Bunge. Kwenu pia naomba niwatakieni kila la kheri ili mfanikiwe kurudi hapa Bungeni. Naamini wapiga kura wenu, watakumbuka utumishi wenu uliotukuka, hivyo watawachagueni tena. *(Makofi)*

Mwisho kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uhai na kuweka mkono wake katika mipango yote tuliyofanya ambayo imefanikiwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, Kamati inakubaliana na Mpango wa Maendeleo, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa Fedha wa 2005/2006 ya Sh. 55,442,163,500/= kwa mgawanyo ufuatao: Maduhuli Sh. 32,864,260,000/=; Matumizi ya Kawaida Sh. 32,970,324,000/= na Matumizi ya Maendeleo Sh. 22,471,829,500/=.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira waliohusika na zoezi zima la kujadili na kuchambua maelezo ya Bajeti ya Wizara hii ni pamoja na Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mwenyekiti, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Aziza S. Ali, Mheshimiwa Shaib Ahmada Ameir, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Ali Said Juma, Mheshimiwa Sharifa Mbarouk Khamis, Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Lekule M. Laizer, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mheshimiwa Bernadine R. Ndaboine, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa

Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Issa Mohamed Suleiman, Mheshimiwa Mathew Ole Timan na Mheshimiwa Martha Wejja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuhusu bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2005/2006, kwa mujibu wa kifungu cha 43(5) (b) (c) cha Kanuni za Bunge, Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, natoa rambi rambi zangu kwa wafiwa wote wa Jimbo langu la Moshi Mjini, kwa waliofiwa katika kipindi cha Ubunge wangu kuanzia mwaka 2000 mpaka sasa. Pia Wananchi wote wa Tanzania waliofiwa katika kipindi chote cha uhai wa Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa jinsi alivyoweza kuiongoza Wizara hii muhimu kwa miaka mingi bila msaada wa Naibu Waziri na kuifanya Tanzania kujulikana duniani kote kama moja ya nchi zenye vivutio vya utalii na ushahidi uko tele jinsi utalii ulivyokua chini ya uongozi wake. Mimi binafsi na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, sina tatizo na hotuba yake ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2005/2006. Hongera sana mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, licha ya pongezi zetu kwa Mheshimiwa Waziri, bado tunamwomba ajaribu kuyaangalia baadhi ya masuala tuliyoyabaini ili biashara nzima ya utalii iweze kuwa shindani katika soko huria, kwani watu katika soko huria wanajaji sana *value for money.*

Mheshimiwa Spika, kuna tozo la leseni tatu ambazo ni *Tour Operator Licence, Mount Climbing Licence* na *Tourist Hotel Licence,* hizi zote kwa watu wanaofanya biashara hii, kazi yake ni moja tu. Tanzania ina mkakati wa kuwafanya watalii waje kwa wingi kuona vivutio vyetu, sasa kwa hali kama hii ya tozo la leseni, ambazo zinawafanya watu waliomo kwenye *Tourism Industry* kushindwa kuwa shindani kulinganisha na nchi nyingine za Afrika zenye vivutio vilivyo kwenye mstari na sisi kutokana na bei wanayowatoza watalii ili kufidia gharama za leseni. Hapa tumesikia hoteli zetu hazitoi vyakula vizuri wala huduma nzuri, ni kwa sababu ya *licenses* hizi kubwa na *taxes* nyingi mno wanayolipa hawa waendeshaji wa mahoteli.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri, aangalie upya aina za hizo leseni ili na sisi tuweze kuwa washindani wazuri, kumbuka kitu kinachoshindana katika soko ni bei. Huko nyuma Mheshimiwa Waziri, aliwahi kutoa ahadi ya kuangalia hizi *licences.*

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida mtu yeyote anayetaka kupanda mlima ni lazima alipie gharama za siku saba za uokoaji *(Rescue Costs).* Ni lazima pesa hizi kulipwa kabla, japokuwa hali halisi ni kuwa mtalii anaweza kupanda siku mbili akashindwa kuendelea na zoezi la kupanda mlima. Sasa inapotokea hivyo, Watalii hawarudishiwi pesa zao za siku zile ambazo hawakupanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nchi iliyo makini kama yetu, jambo hili linatafsiriwa kama unyang'anyi wa mchana *(Day-light Robbery),* kitu kinachopunguza hata idadi ya watalii, kwani jambo baya halisahauliki vichwani mwa watu. Hivyo basi, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, aagize watendaji wake, wawe wanarudisha pesa za watalii pindi ijitokezapo tatizo katika safari ya kupanda mlima na wakashindwa kumaliza safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, aagize ada za *Rescue Fee* wanayotozwa watalii wanaopanda mlima, ifutwe. Wakati dharura ya *Rescue Fee* inapotekea ndipo anayetaka hiyo huduma alipwe. Hii ni moja ya sababu ya kufanya *product* hii ionekane ni *over priced* ikilinganishwa na majirani zetu wa Kenya na Uganda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuachana na sera zisizowaletea Wananchi faida ni sasa. Katika *Master Plan,* wataalamu hao walioandika wanasema wazi kuwa, bei zetu ni *over priced* na nililisema hapa mwaka 2004, wanasema wazi kuwa, *there is no value for money* kwa zile fedha wanazolipa kwa kuja kupanda mlima na sisi ni *worse than other competing destination's.* Kwa nini bei zetu zisipunguzwe ili tushindane na wenzetu? Ni kweli bei zetu humu ndani zinaonekana ni ndogo lakini wenzetu wa Ulaya, wanaotengeneza zile *tour package,* nikiwaambieni hapa ukweli, mtu akifika Kilimanjaro kupanda na kuteremka wanatoza zaidi ya dola 3,000, lakini Mtanzania anaambulia dola 600. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuleta maendeleo na mafanikio katika utendaji kwa sekta yeyote ile, uwakilishi wa wadau ni muhimu sana. Kwa njia hiyo basi, wadau wakuu katika Sekta ya Utalii ni *Tour Operators.* Hawa wana umoja wao unaojulikana kama *Tanzania Association of Tour Operators* na *Tanzania Confederation of Tourism.* Vyama hivi kukosa mwakilishi kwenye Bodi za *TANAPA* na *KINAPA,* ni kutowatendea haki wadau wakuu katika Sekta ya Utalii. Kambi ya Upinzani inamkumbusha Mheshimiwa Waziri kuwa, vyama vya wadau katika Sekta ya Utalii ndio wanaotakiwa kupendekeza majina ya watu ambao Waziri atawateua kuwa Wajumbe wa bodi hizo ili kuongeza mshikamano na kukuza *tourism industry*. Sasa hivi wako Wajumbe walioteuliwa na Waziri, hatujui kigezo alichotumia kuwateua.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inapata pato kubwa litokanalo na ada zitozwazo kwa ajili ya wanaopanda Mlima Kilimanjaro. Kitu kinachotusikitisha ni kuwa, Serikali inashindwa kutengeneza njia zitumikazo kwa ajili ya kupanda Mlima Kilimanjaro, pamoja na barabara zitokazo na kwenda kwenye hoteli za kitalii zinazozunguka Mlima Kilimanjaro. Kambi ya Upinzani inamwomba Mheshimiwa Waziri, suala hili aliangalie vizuri, kwani linapunguza *quality* kwenye macho ya watalii wanaokuja kupanda Mlima

Kilimanjaro, kitu kinacho sababisha kushuka kwa mapato yetu kutokana na utalii wa wapanda Mlima Kilimanjaro. Ikumbukwe, utalii unaliletea Taifa hili asilimia 26 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005, tuliongelea kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Moshi, ambacho ni Kiwanja cha Mji wa Mlima Kilimanjaro, mpaka sasa hakuna chochote kilichofanyika bali kuzungushia senyenge katika kiwanja kile. Ninasema hili la Uwanja wa Ndege wa Moshi kwa kuwa sasa hivi nchi yetu inakosa biashara kubwa ya watalii. Kutokana na kukosekana kwa ndege ya moja moja kuja Moshi, Mji wa Mlima Kilimanjaro na badala yake wanaishia Arusha na Nairobi na hao tunaowapata wanatumia fedha zaidi kukodishia mabasi toka Nairobi au Arusha kuja kupanda mlima, kitu kinachowazidishia gharama na kufanya utalii wetu kuwa ghali kulinganisha na nchi nyingine. Kambi ya Upinzani inaomba ukitazame tena Kiwanja cha Ndege cha Moshi ili kuongeza idadi ya watalii na kuongeza *value for money* kwa utalii wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutangaza rasmi kuwa, Moshi ni Mji wa Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, kuna njia tano kuu zitumikazo katika kupanda Mlima Kilimanjaro, ila inayotumika sana ni ile ya Marangu. Njia hii kwa sasa imeshazidiwa sana na wingi wa watumiaji. Kwa hiyo basi, Kambi ya Upinzani inamwomba Mheshimiwa Waziri, aangalie uwezekano wa kuifanya njia ya *Old Moshi* itumike wakati wa kurudi toka mlimani na hii sio mara ya kwanza kufanya hivyo. Hii itapunguza msongamano kwenye njia ya Marangu, kwa jina lingine *Coca Cola Route.* Kwa njia hii, tuna imani kabisa kuwa, hii itasaidia kuwapa kazi vijana na Wananchi wa maeneo hayo ya *Old Moshi,* kuwapa kazi na sera nzima ya MKUKUTA kuwa na maana kwa Wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, Mlima Kilimanjaro na maeneo yanayouzunguka mlima huo, ni kivutio kikubwa cha watalii. Katika *Master Plan* ya *Tourism,* yaani Mpango Kabambe wa Serikali wa Utalii Kitaifa, nilitazamia kuona Moshi Vijijini, Moshi Mjini, Hai, Rombo na Upareni, ikiwa *declared* kama *Tourist Area* na kupewa kipaumbele katika *development* ya utalii hapa nchini. Lakini cha kushangaza, Sera ya Serikali sio kukuza utalii katika eneo hili bali kuhamishia utalii Mkoani Arusha. Watalii wanapenda Kilimanjaro wafanyeje?

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka wa fedha 2004/2005, niliongelea miondoko mipya ya *(Cultural Tourism)* au Utalii wa Kitamaduni. Huu ndiyo utakuwa mkombozi katika jamii nyingi za Watanzania kwani unahusisha mambo yaliyomo kwenye mila na tamaduni zetu, kitu ambacho ni wale tu waliomo kwenye hiyo jamii, ndio watakuwa wahusika wakuu katika utalii wa namna hii na kitakachopatikana asilimia kubwa itabakia kwenye jamii husika na kutokuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, watu wa nchi za nje wanapenda sana kuelewa vitu vyetu vya kiasili na wangependa kuviboresha zaidi iliviweze kutumika katika mazingira ya

sasa ya Sayansi na Teknolojia. Tatizo watoaji wa taarifa hizo, hawazifahamu vizuri na wanazipotosha kwa makusudi kabisa hivyo, kwa njia hii, jamii mbalimbali Tanzania zinaweza kuandaa *tour package program* zao kulingana na hali halisi. Nadhani watu wa nje wanaweza kuja kuangalia na kujifunza mengi yahusuyo jamii hiyo.

Kambi ya Upinzani inaamini kabisa jamii ya watu wa Same, Marangu, Lushoto, Kibondo, Urambo, Sumbawanga, Kondoa, Kilwa, Bukoba, Masasi, Kahama na kadhalika, wana vivutio vyao ambavyo wangeweza kuwavutia wageni wengi na wakaenda kutembelea sehemu hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Mkoani Kilimanjaro, kuna mapango ya kale ya Wachagga yaliyokuwa yanatumiwa wakati wa vita, kule Upareni kuna *warm springs,* halafu kuna Nyumba ya Mungu, Miamba ya Mawe na bwawa kubwa, lenye mandhari nzuri, yote haya yanavutia sana watalii.

Mheshimiwa Spika, maonesho ya utalii yako mengi sana duniani na mara zote nchi yetu huwa na wawakilishi wa kutangaza vivutio vyetu na urithi wa nchi yetu na watu wake. Mara zote kutokana na uzoefu wangu kwenye hili, Tanzania mara nyingi huwakilishwa na *Tanzania Tourist Board (TTB), Tanzania Association of Tour Operators*, Wizara na *Tour Operators* wenye uwezo wa kushiriki.

Kwa hili, kitu kinachosikitisha ni kuwa, washiriki hawa wote kutoka Tanzania, huuza bidhaa ya aina moja tu, kitu ambacho kwa njia moja ama nyingine ni kuipunguzia hadhi nchi yetu, ambayo ina bidhaa chungu nzima kwa ajili ya utalii. Lakini mbaya zaidi ni kwa Serikali kupeleka watendaji wake, kwa fedha za walipa kodi, wakati pesa hizo zingewapeleka wadau waliomo kwenye sekta ya utalii badala ya watendaji ambao huwa kama watalii wanapokuwa huko.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa kasoro hizi ni bora Wizara iwe inafanya *coordination* kwa wote watakaokuwa wanashiriki katika hizi *Trade Fairs* ili wapangilie vizuri.

Mheshimiwa Spika, kati ya asilimia mia ya eneo la Tanzania Bara, asilimia sita ni maziwa na mito. Aidha, inamiliki ufukwe wa bahari wa kilometa za mraba 800. Asilimia 0.17% ya Watanzania wote wanaendesha maisha yao kutegemea uvuvi na hawa wote wanajihusisha na uvuvi wa kizamani wa mashua na ngalawa.

Mheshimiwa Spika, mapato makubwa kwa Serikali yanatokana na mauzo ya samaki aina ya sangara wavuliwao katika *Lake Victoria,* ambayo ni zaidi ya asilimia themanini ya mauzo yote ya samaki nje ya nchi na asilimia kumi kwa samaki wavuliwao baharini. Hivyo basi, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, awaeleze Watanzania ni kiasi gani tunapata kutoka kwenye asilimia arobaini na tano tunayoimiliki katika Ziwa

Tanganyika na asilimia ishirini tunayoimiliki *Lake Nyasa,* kwani watanzania hawaoni takwimu kimapato kutoka katika maziwa hayo mawili?

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina maziwa madogo madogo ambayo ni urithi wa asili na mengine yamechimbwa kwa shughuli za kuinua uchumi, bila kusahau mito mingi. Kwa ujumla wa maziwa na mito vinakadiriwa kuwa na kilometa za mraba 58,000. Bahati nzuri maziwa haya na mito yote katika mikoa mbali mbali ya Tanzania Bara, inaweza kuzalisha samaki. Kwa hiyo, ni vizuri Waziri akaangalia mpango wa kuongeza uzalishaji wa samaki kwa kupitia katika mito na hayo maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na takwimu hizi, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa, bado hatujafanya mikakati imara ya kuhakikisha rasilimali hii inatoa mchango wa kutosha na kuufanya kuwa endelevu katika kuinua uchumi wa Taifa letu. Aidha, bado kuna mwanya mkubwa wa kuchimba mabwawa kwa ajili ya ufugaji samaki *(aquaculture),* pembezoni mwa mito mikubwa tuliyonayo badala ya kuachia maji yote kwenda baharini. Mabwawa haya yatakuwa changamoto kubwa kwenye kilimo cha umwagiliaji ili kuondoa Umaskini.

Mheshimiwa Spika, inakisiwa kuwa kati ya hekari 130,000 na 500,000 za misitu, hupotea kila mwaka nchini Tanzania kwa uvunaji ambao hauangaliwi na hivyo Serikali kupoteza pato lake kutoka kwenye maliasili hii. Mwaka 2004 tulishuhudia jinsi uvunaji wa magogo ulivyokuwa ukifanyaika na jinsi Serikali ilivyokuwa inakosa mapato kutokana na biashara hiyo kwenda nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, baada ya udhibiti wa uvunaji wa magogo, sasa imezuka biashara nyingine ambayo ni mbaya zaidi kuliko ile ya magogo, kwani uvunaji wake hautilii maanani kama miti inayotumika imakomaa tayari kwa uvunaji au la. Hii ni biashara ya uchomaji wa mkaa, inayofanywa na Wananchi waishio maeneo ya Bagamoyo, kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi za Falme za Kiarabu kupitia Zanzibar. Katika utafiti huu uliofanywa na kuandikwa kwenye Gazeti la *The Guardian* la tarehe 4 Julai, unaonesha kuwa, kwa wiki mashua zisizopungua tano toka Zanzibar hupakia magunia 400 kila moja kwa safari ya kwenda Uarabuni kupitia Zanzibar, ambapo meli kubwa ya kupakia mzigo huo husubiria.

Mheshimiwa Spika, kitu tunachojiuliza, wakati hayo yote yanafanyika wahusika wako wapi na ni kiasi gani cha misitu kinafyekwa na Serikali ipo au imekwenda likizo?

Mheshimiwa Spika, utalii unahitaji miundombinu mizuri ambayo kwa hapa ni barabara. Hivyo basi, ili Utalii kwa Mji wa Moshi kuendelea kuwa na maana kwa Taifa na Wananchi wake, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, aziangalie barabara za Pasua, Mbokomu na Rau, ziendazo kwenye hoteli za kitalii. Barabara hizi ni mbovu sana. Sehemu mbovu ni chini ya kilometa tatu tu. Hizi hoteli huhudumia asilimai 90 ya watalii wote waingiao Moshi Mjini. Tunaomba ufanye utaratibu kama ulivyofanya kwa barabara ziendazo katika fukwe za Dar es Salaam na zile za Serengeti, ili barabara hizo za Moshi Mjini, ziweze kupitika wakati wa kipindi chote cha mwaka. Pia una uwezo wa kutoa pesa kwa ajili ya kutengeneza *run way* ya Kiwanja cha Ndege cha Moshi. Nina hakika uwezo

huo unao, nia unayo, timiza azma hii. Mheshimiwa Waziri, wewe ni shahidi kwani wakati mwingine unashindwa kufika nyumbani kwako, kwa kupitia barabara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Pato la Taifa la Taifa linapatikana asilimia 26 kutoka katika utalii, fedha za kuweza kufanya kazi hiyo, nadhani unaweza kuzitoa. Tumejaribu sana kumshirikisha Mkurugenzi wa Moshi Mjini ili azitengeneze barabara hizi zilizo katika Manispaa yake, lakini katakata amekataa japokuwa anajua ndizo zinazoingiza pesa katika nchi hii.

Kwa kuwa Serikali imetoa punguzo kwenye mafuta ya ndege kwa lengo la kuongeza idadi ya watalii wanaokuja nchini kwetu na kuinua sekta nzima ya utalii hapa kwetu, kwa lengo hilo tunamwomba Mheshimiwa Waziri, afikirie na wale wanaofanya biashara ya kusafirisha watalii kwenda na kurudi kwenye vivutio hivyo kwa kuwatolea *VAT* kwenye mafuta ya magari yao yanayosafirisha watalii. Vile vile kuondoa kabisa *licence* za *TLB* zinazokatwa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze wapiga kura wangu wa Moshi Mjini, kwa ushirikiano mzuri tuliopeana kwa kipindi chote cha miaka mitano. Ninaamini kabisa kuwa, mchango wangu kwa kipindi hicho mmeuona mpaka kufikia kiwango cha kusema kuwa, mimi ni mkombozi wenu na ninasema, asanteni sana. Sasa hivi CCM wamefikia kuchangisha pesa za kuwanunua ili mnikatae. Mimi ninasema pesa hizo ni za kwenu kuleni, lakini mjue kuwa mimi ndio mgodi wenu na wote Moshi mjue hilo, kwani bila ya mimi kuwa Mbunge wenu, hizo pesa zilizochangwa zisingechangwa. Mbiu yetu iwe Ndesa-Mgodi, Ndesa-Mgodi. Ninawaambia kuwa, kadri ninavyoendelea kuwa Mbunge wenu, ndivyo pesa za kuwapa zitakavyoendelea kuchangwa hivyo, msiwe na wasiwasi, hizo pesa zitakazochangwa ni zenu kuleni, Ndesa ni mgodi wenu, nipo kwa ajili yenu, msiwe na wasiwasi wala shaka. Jueni kule kwenye majimbo ya CCM, hawapati pesa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Maliasili na Mazingira, imepata uzoefu mkubwa na kujifunza mengi sana, chini ya Mwenyekiti wa Kudumu wa Kamati yetu, Mama yetu, Mheshimiwa Anne Makinda, pia na Makamu wake, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib. Huyu mama ana hekima ya ajabu, uwezo wake mkubwa kiuelewa na mchapa kazi wa ajabu! Nakuombea mama kwa Mwenyezi Mungu na kwa Rais ajae, uwe mmoja wa Waheshimiwa watakaokuwa wanaongoza Wizara nyeti za nchi hii. Nakutakia kila la kheri mama na Mungu akubariki sana na akupe afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa shukrani zangu kwa Kamati nzima ya Uongozi, chini ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni, kwa ushirikiano walionipa kwa kipindi chote nilichokuwa Msemaji Mkuu wa Wizara hii. Aidha, nawapongeza wanachama, watendaji na viongozi wote wa chama changu cha CHADEMA, kwa kutetea na kuimarisha demokrasia nchini. Sisi CHADEMA tunaamini, mabadiliko ya kweli yatapatikana kwa kuboresha elimu, kilimo cha kisasa, kuongeza ajira, afya kwa wote na kutokomeza rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi na nadhani mwaka huu ni safari yangu ya mwisho. Kwa hiyo, nasema *bye bye. (Kicheko/Makofi)*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kwanza, ambayo kwa ujumla, mimi sijachangia tangu Bunge lianze, sikuwepo nilikuwa kwenye matibabu kule India na nakushukuru sana wewe binafsi, pamoja na Ofisi yako, kwa kuweza kunihudumia kwa matibabu hayo na nimepona. Kwa kweli nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa hotuba yake nzuri sana. Nimekuwa mzoefu katika Bunge hili, hotuba hii ina *data* nyingi na inaonesha mafanikio makubwa kwa kipindi cha miaka 10. Kwa kweli naye amekuwa mzoefu katika Wizara hii, pamoja na Wataalam wake, nawapongezeni sana kwa jitihada ambazo mmefanya kwa miaka hiyo 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vile ninachangia kwa mara ya kwanza na mimi napenda niungane na wenzangu kuwapa pole familia ya Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, pamoja na Marehemu Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga. Mungu aziweke roho za marehemu hawa mahali pema peponi, *Amina.*

Katika kuchangia kwangu katika hotuba, kuna malengo makubwa ya Wizara ambayo nimeyaona na kuna mikakati ambayo inatakiwa kufanywa. Lakini napenda nizungumzie suala la utalii, ambayo ni malengo makubwa na ni sehemu katika Wizara hii ambayo inaleta fedha za kigeni. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba, tunajivunia sana kwamba, kuna utalii na ongezeko la watu. Lakini ukiangalia kwa makini sana, ni kwamba, ongezeko la watalii ni kidogo sana ukienda mwaka hadi mwaka karibu tunarudia takwimu hizo hizo, zinaongezeka kwa shida sana na tunatembea tunajaribu kutangaza, lakini matokeo yake yanakuwa ni madogo sana. Nisingependa uwezo wetu mdogo utufikishe mahali pa kubinafsisha. Maana yake tumezoea kama tunashindwa tunatafuta watu wa kubinafsisha, sijui kama tumelibinafsisha kwa matangazo. Lakini napenda hii ifanye kazi kwa bidii sana kama usipowekeza hutapata. Kuwekeza kwetu ni kudogo katika kuangalia bajeti tumetenga kama shilingi bilioni mbili tu katika utalii. Ni kidogo sana.

Ukizungumzia utangazaji wa kisasa katika dunia na nikisema hili ni wazi, ukitaka kutangaza lazima utangaze. Nilifurahi sana nilipokuwa India nikiangalia *BBC,* wenzetu wa Zanzibar wametangaza kabisa, wameweka ndani ya *BBC* mambo ya utalii, nchi nzima baada ya saa moja Zanzibar inaonekana. *(Makofi)*

Sasa unapozungumzia suala la utalii Zanzibar, inakua na Tanzania Bara iko hivi, kwa sababu ya ukubwa wake. Ni kwamba, wenzetu wamethubutu kuingia katika vyombo vikubwa vya kutangaza na sisi ni lazima sasa tuingie katika vyombo kama *BBC.* Tuingie katika vyombo vya kutangaza ulimwenguni na tuhakikishe kwamba, tumo. Unapita mahali lazima utangaze. Sasa hivi TVT ndiyo inatangaza kidogo, *ITV* bado, hatujatangaza kabisa mambo yetu ya utalii katika Tanzania. Kwa hiyo, nasisitiza kwamba, hata sisi wenyewe hatuwezi kutangaza wakati robo tatu ya Watanzania

hawatembei, hawaendi hata katika mbuga zetu. Tukiuliza kati ya Wabunge hapa waliokwenda safari hii Serengeti au Tarangire ni asilimia ngapi, hakuna wanaomba kwenda nje tu, lakini kwenda Ngorongoro ni shida. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunatangaza kitu ambacho sisi Watanzania hatupendi, hata wanafunzi na taasisi mbalimbali haziutambui huu utalii wetu wala hatuuthamini. Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri, juzi aliposalimiana na wanafunzi, akatoa fursa ya kutembelea katika mbuga za wanyama. Nadhani sasa tukitaka kutunza au kuwaangalia hawa wanyama, inabidi taasisi zetu ziwe na mpango kabisa wa kwenda kutembelea mbuga zetu za wanyama, ili Wananchi wajenge tabia, tuweze sasa kujenga ari ya kupenda wanyama na kuhifadhi. Sasa tunatangaza watu wa nchi nyingine waje katika nchi yetu, lakini sisi Watanzania hatuendi kutembelea hizo mbuga! Hii ni hatari kabisa. Kwa hiyo, nasema kwamba, kuna haja ya Watanzania sasa kuanza kujenga tabia ya kutembelea mbuga zetu ili kuweza kuongeza hata pato la ndani.

La pili, napenda niseme kwamba, sasa hivi robo tatu ya magari mazuri yanatoka Japan. Wao wametangaza biashara yao ya magari, lakini sisi hatuna kitu chochote ambacho tunaweza kupata Japan na Japan sasa hivi wanatembelea dunia nzima kwa utalii.

Baada ya kusema hayo, kuna mambo mengine ambayo naweza nikayazungumza. Kuna suala sasa hivi la hifadhi za kijamii *(WMA)*. Mheshimiwa Waziri, amekazana sana katika kipindi chake kukabidhi Wananchi hifadhi hizi. Lakini sijui kama ni wataalam wametengeneza taratibu, kuna ukiritimba mkubwa sana wa miongozo ya *WMA* kwamba, inashindikana kutekelezeka. Wananchi wameshafundishwa. Nina mbuga tatu ambazo sasa hivi wangeweza kufaidika, unaondoka. Hii Sheria haipiti hapa kwa sababu ya ukiritimba mkubwa sana, ingawa umejitahidi sana. Nakupongeza, lakini ni nani atakuja kuwakomboa hawa Wananchi ili waweze kulinda wanyama wao na waweze kufaidika?

Kwa sababu kuna mvutano mkubwa kati ya wanaotumia mbuga hii sasa hivi na Sheria hii ya *WMA* na wanajitahidi kuzuia ili Wananchi wasifaidike, ili wasiweze kulinda wanyama wao kwa sababu wao ndio wanafaidika sasa hivi. Kwa kweli hili unaondoka lakini Wananchi wanahangaika. Watanzania walikuwa wanasubiri kwa hamu sana na sasa hivi kuna wawindaji ambao wameshakaa katika maeneo hayo miaka 10 hakuna chochote walichofanya, ni kudanganya Wananchi au wanajenga darasa moja kudanganyia pipi,kwamba kuleni hii basi mezeeni. Lakini nakuomba sana uimalizie hii kazi na Wananchi wanasubiri. Nadhani umeanza, lakini kwa kweli umeanza kazi takatifu ambayo nina hakika kabisa kwamba, baadaye itawakomboa Watanzania.

Jambo lingine ambalo nataka nilizungumzie ni kwamba, tunayo mapori yetu ya akiba, sasa hivi yameshinda hata kupata zawadi, *Global Equator Initiative Award* na *SULEDO,* lakini sasa yalikuwa yanaendeshwa na wafadhili, ndiyo maana tukapata hiyo zawadi na bado wapo. Lakini sioni mkono wa Serikali kuja kuangalia msitu huo, wafadhili wakiondoka itakuwaje? Sijaona ikitembelewa na kuangaliwa kama inavamiwa, inatunzwa na inathaminiwa, ni Wa-Swedish tu ndiyo walikuwa wanapenda, wakaja

wakahifadhi, sisi tukasaidia tukashinda. Kwa hiyo, naomba sana ikiwezekana katika suala hili, mlitilie maanani ili baadaye yawe manufaa kwa nchi yetu.

La mwisho, ni suala la fedha za wanyamapori, asilimia 25. Mwanzoni Wizara ilikuwa makini sana, ikituma fedha hizo inafuatilia na kuhakikisha inafanya kazi ambayo ilitarajiwa. Sasa hivi mnatoa tu. Ni vizuri sasa muweze kuangalia kwa sababu zinatoka fedha nzuri na zinatakiwa zifanye kazi ya kuendeleza wanyama, pamoja na sehemu zilizotoka na miongozo ikaziwe na ziweze kufuatiliwa kwamba, zinafanya kazi iliyokusudiwa. Kwa hiyo, naomba sana katika suala hili ni kwamba, muandae kitengo maalum ambacho kinaweza kutoa *feedback* ya fedha hizi zinavyotumika.

Baada ya kusema hayo yote, nakutakia kila la kheri, narudia tena kukupongeza katika kazi yako nzuri na kwa kusema kweli kwa kuiendeleza Wizara hii ambayo ni nyeti katika nchi yetu. Mimi ni mhifadhi mzuri tu na napenda kazi ya Wizara hii na nayapongeza mashirika makubwa haya ya *TANAPA* na Ngorongoro, kwa jitihada zao, naomba wawe na ubunifu sasa, pamoja na uvuvi wa kuweza kuongeza mapato maradufu. Kwa sababu wana uwezo mkubwa, wawekeze na wawapeleke wataalam wawafundishe, lazima kuwe na elimu ya juu zaidi kwa wataalam kwa sababu wafanyakazi kama huwapeleki kusoma, basi Shirika linadumaa. Ni lazima wawe na *Ph.D.* na *Masters* ndiyo wanaweza kutoa haki. Wataalam wenye *diploma* ndiyo wamejazana, hakuna lolote. Lazima wapate *Masters, Ph.D.* na kadhalika. Ndiyo kazi inaweza kutoa tija hizi ambazo mimi nazizungumzia. Wenye *diploma* hawatoi kitu chochote pale. Kwa hiyo, lazima fanyeni kama Bandari hii ya Tanzania, wataalam ni *Ph.D.* na *Masters* tu, ndiyo wanazunguka Bandarini pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nafurahi kupata nafasi hii ili nami niweze kuchangia kiasi katika Wizara hii. Napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ambao wamefariki. Nawaombea baraka na kheri, roho zao Mwenyezi Mungu aziweke pema Peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, ninaumwa ndiyo sababu na sauti yangu imekuwa kidogo inagota. Wizara hii kwa bahati nzuri inaongozwa na Waziri mwanamke. Huyu mama kwa kweli ni shujaa na nampongeza sana kwa jinsi alivyoweza kuitetea Wizara hii, mahali ambapo palikuwa pamevamiwa. *(Makofi)*

Wizara hii ilivamiwa na watu wa nje hasa Wachina na Watanzania wenzetu, wakajikuta wameingia kwenye mtego bila kujua, wakauza mali yetu. Lakini kwa ushujaa wake Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, alisimama kidedea, akatetea, magogo yetu hayakuweza kutoka nje mpaka pale Sheria ilipofuatwa ndipo magogo yale yakaweza kuondoka. Nampongeza sana kwa ushujaa huo ambao ameuonesha, vinginevyo

wangesema ingekuwa mwanaume labda ndiyo. Lakini bahati nzuri ni mwanamke, shujaa, asiyejali, anachapa kazi barabara kuzidi wanaume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa siku ya leo nataka kuzungumzia mambo ya kale. Tanzania ina mali nyingi sana ya mambo ya kale. Mambo ya kale yanavutia watalii na Watanzania. Lakini bahati mbaya, nimegundua kwamba, Watanzania na Serikali yenyewe, wanajua umuhimu wa mambo ya kale lakini hawajatilia umuhimu zaidi. Ukichukulia hali ya sasa hivi, nchi yetu iko kwenye ngazi ya maendeleo ya Kitaifa na kama ingefuatilia umuhimu wa mambo ya kale, nina hakika ingekuwa imezingatia kuyahifadhi.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu katika kuzunguka kwangu, nikiwa katika Kamati ya Akina Mama na Watoto na pia katika kipindi hiki cha mwisho katika Kamati ya Maliasili na Utalii, nimezunguka nimekwenda Kigoma, Kilwa, Mafia na Bagamoyo. Kuna mambo ya kale mengi sana. Lakini kinachosikitisha ni kwamba, utakuta ni nyumba ndogo tu inayoonesha mambo ya kale na kumbe sisi mambo ya kale yako mengi na mali yetu nyingi ya mambo ya kale ya Tanzania iko Kenya kwa ndugu zetu jirani.

Inasikitisha kwamba, Tanzania haijachukua hatua ya kurudisha mali yetu na Wakenya wanatuita mpaka keshokutwa kwamba, turudi tukachukue mali yetu. Sasa kama Serikali kweli ingekuwa imeweka maanani, kwa nini mpaka wenzetu watuitie mali yetu?

Je, wangekataa kuitunza tungefanyaje? Ina maana mali yetu ingepotea na sisi tuna mapori makubwa hapa nchini hayana kazi. Kuna wasamaria wengi ambao wanajitolea kutupa msaada. Sasa misaada ya fedha inayokuja hii tukimwelekeza kweli mfadhili mmoja katika pori fulani ambalo Wizara ingeweza kuchagua asingeweza kweli kutujengea majumba mengi hata nyumba moja kubwa na kuweza kuhifadhi mali zetu za mambo ya kale. Tungeweza kama tungeelekeza nguvu zetu kutunza mali zetu.

Lakini kwa sababu Serikali, pamoja na Wizara haijaweka umuhimu katika jambo hili, inaona ni mambo ya kawaida. Wataalam tunao, lakini siyo wengi wa kutosha.

Naishauri Wizara hii irudishe mawazo nyuma, ikumbuke mambo ya kale, ni muhimu kwetu sisi Watanzania na hasa watoto wetu ambao tunataka nao wajifunze mambo ya kale. Watajifunza vipi mambo ya kale wakati yako Kenya?

Lakini yakirudishwa hapa nchini, wanafunzi watafundishwa na kisha watakuwa na hamu ya kusema twende Mkoa fulani mambo ya kale ndiko yalikofugwa au mambo ya kale ndiko yalikotunzwa.

Ninaishauri na ninashawishi Serikali ichukue hatua za makusudi, irudishe mambo yetu ya kale, mali ambayo iko Kenya mpaka sasa hivi na ninawaomba Wakenya wasituchoke, watuvumilie, kwa sababu wenzetu huenda walikuwa na mwamko wa

kuweza kutambua mambo ya kale yakoje, wakakubali kutunza hadi wakatunza mali yetu ya Watanzania.

Kwa hiyo, nawaomba waendelee na moyo huo ili Serikali yetu iweze kuchukua utaratibu wa kupata pori katika Mkoa wowote, ijenge nyumba kisha ilete mali zetu za mambo ya kale tuweze kutunza sisi wenyewe Watanzania bila kuhitaji kutunziwa na nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ningeomba Wizara hii katika mambo ya kale, tunayo mengi, nimetaja Mafia na Kilwa kuna magofu, tulipokwenda Mafia ilisikitisha sana, tumekuta vitu vingi vya maana na vya muhimu kujifunza. Lakini nasikitika kwamba, hakuna hata Mtanzania ambaye anaweza akakaa chini, akaelezea moja hadi mwisho, kila ukimwuliza unajua mzee fulani angeweza kujua, ghafla mzee fulani alishafariki, sasa kama tutaenda hivyo ni lini basi mambo ya kale haya yaliyoko Mafia tutayapata ukweli wake. Kwa sababu pale panaonesha palikuwa na mambo ya kale ya Wafalme wa kale. Sasa nilikuwa naomba Wizara ifuatilie, ipeleke watafiti ili utafiti uweze kupatikana sehemu hiyo iweze kufanyiwa kazi, kuna vijana waliojitolea kupalilia magofu yale yaweze kuonekana. Wizara iweke umuhimu ili sehemu hiyo iweze kutupa faida kwa sisi Watanzania na watalii pia wanaokuja, ili tupate pesa za kutosha na sisi wenyewe tujifunze falme za kale zilikuwa zinafanya nini, maana zilikuwa nchini mwetu. Falme za kale sehemu za Mafia ilionesha huyo bwana alikuwa na wake sio chini ya 60, lakini wale wanawake walikuwa wanafanya nini na walikuwaje? Hakuna anayejua. Sasa ningeshukuru sana kama Wizara hii ingeweza kuchukua umuhimu wa kutunza taarifa hizo za mambo ya kale.

Pia kwa mambo ya kale, nilipokwenda sehemu ya Kigoma, hakuna hawa wataalamu, bahati mbaya kuna mzee mmoja, sasa hivi ni mzee lakini ukimwangalia ni kijana kwa sababu mwili wake ni mwembamba, lakini ni mtu mzima. Huyo bwana anasimulia habari ya *Livingstone,* utashangaa, anasimulia hata kama amefumba macho atakusimulia *as if* anasoma. Hata kama amelala anasimulia, nafikiri hata akiwa ndotoni anasimulia habari ya *Livingstone*, kwa sababu ameikariri kichwani. Sasa kwanini Wizara, isichukue hatua ikaweza kuzingatia haya mambo, sasa anakua, kuna kufa, kuna kustaafu, amezeeka hawezi kwenda ofisini, haya tutayapata wapi? Tulipojaribu kumwulizia safari hii, anasema kweli kuna kijana kutoka Chuo Kikuu aliletwa hapa kufanya kazi pamoja na mimi, nimejaribu kumfunza, kumwelewesha, kwa sababu ametoka Chuo Kikuu, lakini mambo haya ya kale hakuyajua, lakini mwenzangu akaniona kama mimi mpuuzi, kijana yule alitoroka akakimbia, hakuwa tayari kujifunza na kuyafanyia kazi.

Tulihisi kwamba alikimbia kwa sababu, Wizara ilipompeleka pale ilikwenda ikamuweka wewe ndio mfanyakazi kaa hapa na vijana wetu wa kisasa sio wa kizamani kwamba, zamani ukipewa kazi, unapewa kazi huangalii mafao, lakini vijana wa kisasa hivi anahitaji mafao kwanza, kama mafao hana hawezi kukaa Kigoma, kuangalia mambo ya kale, mambo ya kale yanakufaa wewe. Sasa Wizara lazima izingatie hayo, vijana tulionao sio wa kale ni vijana wa kisasa, wanahitaji mafao ambayo ni pesa, wanahitaji nyumba na fedha za kujikimu za kutosha. Lakini Wizara haikuangalia hilo, kijana

aliyeenda ni wa Chuo Kikuu, kweli wa Chuo Kikuu afike na kurudi bila sababu, sababu ni mafao. Sasa naiomba Wizara iliangalie vijana wetu tunavyowapeleka kwenye mambo ya kale, wapewe mafao ya kufaa ili waweze kuzingatia na wafanye kazi ya haki kama inavyohitajika kuiweka nchi yetu katika kumbukumbu za mambo ya kale. Watoto wetu wanaokuja hata sisi tuliopo wengine hatuyajui kama hukuzunguka hujui kama kuna mambo ya kale mazuri zaidi. Kuna mahali ambapo kuna nyayo zilizokanyangwa zimeaachwa hapo kama hukwenda darasani huzijui lakini kama zimewekwa mahali hata usiyesoma utakwenda kupaona kumbe hapa ndio pana hivi na hivi. Naomba Wizara ilizingatie hilo kwa makini sana.

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie pia habari ya kumbukumbu. Hapa nchini mimi kwa kuangalia kwangu sana, labda umeangalia kumbukumbu zaidi za Marehemu Baba wa Taifa, hizo kidogo zipo, japo sio zote, hata kwenye vitongoji alikopitia, lakini kuna mahali pengine kabisa unaambiwa tu hapa alikuwepo, hapa alikuwepo, alipita hapa Mzee Nyerere, hapa alipita mwalimu fulani, lakini hapakuwekewa ule umuhimu wakusema hata mtu akifika, anasema kweli hapa palikuwepo fulani. Mfano tu hapo Pungu Shule ya Sekondari, hapaoneshi kama Rais Mstaafu Mwalizishi, Marehemu Mwalimu Julius Kambarage alikuwa pale. Naomba Wizara, iliangalie hili na ni sehemu nyingi na sio huyo tu, Rais Mstaafu Baba wa Taifa alikuwa na wazee wenzie, Mzee Karume, naye aangaliwe mahali pake ndio kumbukumbu za watoto wetu na sio hao wazee wawili tu, kuna wazee wengi kuna Mzee Rupia na wengine kadhalika hata Wizara inajua kumbukumbu zake zinapatikana wapi. Mbona zamani tuliposoma, tulikuta vitabu vya historia ya watu wa zamani, kwa nini sisi Watanzania, wazee wetu hamuwafanyii hivyo. *(Makofi)*

Naiomba Wizara na Serikali ilizingatie ombi langu. Mheshimiwa Waziri katika taarifa yake, ameonesha kwamba, kweli kuna wataaalamu na nakubaliana naye kwamba, kuna wataalamu wazuri sana katika Wizara yake. Lakini ni wachache mno ukilinganisha na ukubwa wa nchi yetu na ukilinganisha na maendeleo tuliyomo sasa hivi katika nchi hii. Ninaomba shule ziwepo na kama zipo basi wanafunzi waongezewe utaalamu. Kwa sababu mtoto kama amesoma akapata utaalamu mkubwa, hata ukimpa kazi ataifanya kwa ukamilifu, sasa naishauri Wizara iliangalie hilo kwa makini.

Mheshimiwa Spika, sikuwa na mengi sana, naomba tu kuishukuru, Wizara kwa kazi nzuri ilizofanya na wataalamu wake. Lakini naomba aongeze nguvu kwa wataalamu waliomo kwenye majengo ya kumbukumbu na kwenye sehemu za mambo ya kale kama Bagamoyo, waliopo kwa kweli hawatoshelezi, ninaomba sana muangalie muweze kuongeza, wataalamu waliopo, waende kila sehemu ili kuziweka sawa kumbukumbu zetu sehemu zote ziliko.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza pia wewe na kukushukuru katika kipindi chote hiki tulichokaa katika Bunge hili, inawezekana pia tumekukwaza lakini sisi tunafikiri kama umetukazwa ni kwa bahati mbaya, hukuwa na nia mbaya, umekuwa karibu na sisi. Ninashukuru kwamba, nimetembelea na mimi Tanzania, lakini sikupata bahati ya kwenda nchi za nje kama wenzangu walivyopata, lakini naomba Mungu wakati mwingine kama utarudi kuwa Spika na mimi nikajaliwa kurudi, Mwenyezi Mungu akipenda, siku moja

utasema na huyu mama naye aende. Kwa sababu na wenzetu wasiojua Kiswahili wanakuja hapa, sasa kwa nini sisi tusiojua Kizungu mnasema tusiende kule? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. FATMA SAID ALI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kutoa shukrani zangu za dhati, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Lakini kabla sijachangia kwenye hoja hii, napenda nichukue nafasi hii rasmi, kukupongeza wewe mwenyewe kwa kutupa nafasi sisi Wajumbe wa Tume ya Huduma za Bunge, kwenda kufanya ziara Nairobi - Kenya, Nigeria na Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, imebidi niseme hivi kwa sababu tumeona Kenya wameisifu sana Tanzania na wao kuiandaa Tume yao wamejifunza hapa kwetu Tanzania, ingawa sasa wameboresha imekuwa nzuri zaidi. Hivyo, naamini kipindi kinachokuja utakuwepo na Tume itaboreka zaidi kama ya wenzetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa kazi yake nzuri ambayo anaifanya kwenye Wizara yake, pamoja na Katibu Mkuu, Ndugu Salmon Odunga. Mheshimiwa Waziri, amesimamia Wizara yake vizuri, hata Kambi ya Upinzani wamempongeza na mimi pia kwa niaba ya wanawake wenzangu, lazima tumpongeze kwa sababu ameonesha mfano wa kuweza kusimamia Wizara yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sio kwa maneno tu, nazungumzia kwa *data* na *facts,* ambazo zimo kwenye kitabu chao cha hotuba hii. Wameonesha kwamba, ukurasa wa 12 la kwanza kabisa ni ushindi wa banda la sabasaba, katika Wizara zote, Wizara yake ikawa namba moja. Kwa hiyo, peke yake ni sifa ya aina yake. Lingine imeonekana wazi katika kitabu chake ukurasa wa nane wameonesha utalii umekuwa kwa asilimia kumi na *data* zimeonesha mwaka 1995 watalii kama 295,000 ndio waliotembelea Tanzania. Lakini mwaka 2004, wameongezeka mpaka laki 582.807, hii imeonesha kwamba, kazi nzuri imefanywa kwa sababu tumeona mafaniko. Lakini isitoshe kwamba, watalii wameongezeka wengi na fedha za dola za Kimarekani zimeongezeka, mwaka 1995 ilikuwa kama dola za Kimarekani 259,000, lakini mwaka 2004 dola laki saba orabaini na sita milioni za Kimarekani. Kwa hiyo, kama nilivyosema, inaonesha wazi kwamba kuna hatua zilizopigwa ukilinganisha na miaka ya nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine la kujivunia kwa Tanzania, ni hii kuanzisha tovuti ya kutangaza utalii wetu nje ya nchi na imezinduliwa rasmi na sasa inafanya kazi. Kwa hiyo, hata wenzetu wote walioko nchi za nje, wakifungua hii tovuti wataona maendeleo yetu ya utalii katika Tanzania. Miaka ya nyuma haijakuwepo, tutoe sifa pale tunapofanya jambo zuri. Kazi hii ni nzuri, kwa sababu wakati wote watu walikuwa wanalalamika, tukitaka taarifa hatujui tunazipata wapi lakini sasa *website* iko pale, kila mtu anaweza kuiona.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo namsifu Mheshimiwa Zakia Meghji na linaonesha matunda yake, ni kuweza kufanya vikao vya watendaji kwa Serikali mbili, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Tanzania Bara, hizi Wizara ya Muungano. Mawaziri wote wanasema Wizara zao za ushirikiano lakini hapa vilifanyika vitendo ambavyo matokeo yake tumeona ukipanda ndege zetu za *Air Tanzania, KLM* na nyinginezo, utakuta *pamphlets* ambazo zinazungumzia Tanzania kwa ujumla, Kilimanjaro, hifadhi zote, *beach,* hoteli zote Zanzibar na Bara. Haya ni matokeo ya watendaji kukaa pamoja kwa kushirikiana wakaweza kutengeneza *pamphlets.* Kwa hiyo, hilo ni jambo ambalo sisi tunashukuru sana na tunaamini mafanikio tunapata Tanzania nzima.

Lingine ambalo Wizara hii tunaipa pongezi ni filamu ya kuutangaza utalii, ambayo inaitwa *Tanzania Authentic Africa.* Imepata ushindi wa tuzo nne za Kimataifa, kutokana na ubora na wadhifu wa filamu yenyewe. Waheshimiwa Wabunge, tuwapongeze Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba, basi Mawaziri wengine pia waliokuwa wana Wizara ambazo si za Muungano, waige mfano huu, ushirikiano huu uliokuwepo uzae matunda ili hata utakapokuja kuondoka, wanaofuata waweze kuendeleza yale maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya *TTB,* ni finyu sana ukilinganisha wao wameomba wapewe shilingi bilioni saba, wamepewa shilingi bilioni 2.8, hata nusu ya ile waliyoomba haijafika. Tumepewa kigezo kwamba, 2010 lazima waingie watalii kama milioni moja katika nchi yetu na pia tutapata fedha dola za Kimarekani bilioni moja na laki tano. Sasa tutapataje, wakati hatuwapi nyezo hawa *TTB* ili kuweza kuhamasisha na kuitangaza ili wafungue masoko mengine mapya watalii washiriki wengi. Kwa hiyo hapa, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, waitizame tena kwa sababu wametoa hii shilingi bilioni mbili na laki tisa, hizi ukizichanganua utakuta shilingi bilioni moja na laki sita ni matumizi ya kawaida, shilingi bilioni moja za ujenzi wa *Utalii House,* shilingi milioni mbili mshahara, wamemaliza shilingi bilioni mbili laki nane. Sasa za kwenda kwenye maonesho ziko wapi, za kuandaa *pamphlets* ziko na tumeseme kweli bila ya kwenda kutangaza huko nje watalii watakujaje? Kwa hiyo, sisi hapa tunasema kwamba, tunaomba Wizara ya Fedha, iwasaidie hawa *TTB* angalau wapate waweze kushiriki maonesho. Mwaka 2004 tumeshiriki maonesho kumi ya dunia katika maonesho 22, sasa mwaka huu tutakwenda wapi tena hata moja hakuna na pesa hakuna.

Mheshimiwa Spika, tunataka kweli fedha sisi za kuondoa umaskini, pesa hizi zinakuja, watalii wanatembea na sasa tumeambiwa na Mheshimiwa Waziri kuna, soko la China, soko la Japan na soko la Urusi, wanakwenda kuwinda Abudhabi, maonesho hayo ya *hunting* nao Waarabu wana pesa yao, wanataka kuja kutembea huku kutazama *wildlife, old beach,* watu wanapesa zao wanataka kuja kupumzika, Wajapani wanapenda kuja hapa kupanda Mlima Kilimanjaro na wanapenda maana yake ni *hobby* yao. Sasa kwa nini tena hizi pesa hatuendi huko kwenye maonesho tukawaita, tunawabania?

Mheshimiwa Spika, naomba kwamba, Wizara ya Fedha, iangalie tena kama kweli tunataka hii dola 1.5 bilioni ya pesa za Kimarekani. Lingine napenda kuwapongeza *TTB,*

kwa kuaanda Mwongozo wa huu utalii na utamaduni, ambao unaitwa *culture tourism.* Hapa napenda moja kwa moja, tuwapongeze Wakurugenzi, Ndugu Munguo, pamoja na Ndugu Macha, kwa kazi zao nzuri, ambao wanatusaidia kutuelimisha kuhusu huu utalii na utamaduni. Pia napenda kuishukuru Idara ya Utalii, wameweza maana yake walikuwa katika tafiti tafiti zilizofanywa ikaonekana kwamba, Zanzibar wanawake hawashiriki kikamilifu katika utalii, kwa hiyo, tuliwaomba wakaja Zanzibar wakaandaa semina kwa wanawake ili waweze kuhamasika waingie katika biashara ya utalii.

Mheshimiwa Spika, tunasema kuondoa umaskini na naamini wanawake wanaweza kuondoa umaskini katika hii biashara ya utalii. Sasa napenda nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba, tunaishukuru sana idara hii ya utalii na ni mafaniko yake makubwa tumeanzisha *NGO,* ambayo tunaiita Wanawake na Biashara ya Utalii Zanzibar na mimi ni Mwenyekiti wa muda.
Kwa hiyo, hii imetusaidia sana na tunaamini kama tunaweza kupunguza umaskini sasa haya yote yalikuja kutokana na hiyo semina, ambayo wanawake wamehamaisika na kuweza kuunda chombo chao cha kuweza kuwasaidia kuwaondoshea umaskini na kama mnavyoelewa, Zanzibar utalii umekua mkubwa, mahoteli yako mengi, kwa hiyo, wanaweza kufanya shuhuli mbalimbali ili waweze kujisaidia katika kipato hiki katika utalii.

Mheshimiwa Spika, pia naweza kumpongeza rasmi hapa muwekezaji mmoja Mzalendo kutoka Bukoba, yuko pale *New Kunduchi Beach Hotel.* Kamati yangu ya Uwekezaji na Biashara tuliitembelea hii tukaona ni tofauti na hoteli nyingine. Kwa hiyo, tunapozungumza hoteli sio nzuri, jamani ziko nyingine nzuri za Kimataifa na hii ni *Five Star, facilities* zote zipo mpaka *water world* watoto wanakwenda kucheza pale, wanafurahi ,ukitaka vyumba vya *bungalow* ,au vya kawaida hivi hivi vinapatikana.

Kwa hiyo, naomba wawekezaji Wazalendo, wachukue mfano wa huyu kijana kutoka Bukoba, ambaye ameweza kuweka hoteli nzuri, ambayo sasa hivi watalii wanakuja wengi na imeshajaa kwa mwaka huu. Sasa namwomba tu Mheshimiwa Waziri, labda hawa Hoteli ya Nzoka, tukae tena kikao tuone wapi kuna madosari lakini mifano mizuri ipo.

Mheshimiwa Spika, napenda tena niseme kwamba, naipongeza Wizara hii kwa kuchangia asilimia 16 kwenye Pato la Taifa, hili ni jambo zuri kwa sababu wameonesha wamekusanya shilingi bilioni 28 mpaka Mei, 2005, kutokana na shilingi bilioni 24 za 2004. Jamani imefanya kazi Mheshimiwa Waziri, nakuomba kama hujaambiwa, nakwambia kachukue fomu wilaya yoyote unayotaka, kama Jimbo, kama Viti Maalum, Wananchi wameona kazi yako na wanajua mchango wako, naamini watakuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia, naogopa nisigongewe kengele. *(Makofi)*

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii adimu ili na mimi niweze kuchangia machache kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, hotuba mara zote ikiwa nzuri, iliyochambuliwa kinaga ubaga, mambo yote yako bayana, inakuwa ni shida kuchangia. Lakini kwa sababu nimeomba, itabidi nichangie machache. Utalii ni sekta muhimu sana kimaendeleo na inachangia kiasi kikubwa sana kimapato, Kusini utalii umelala, vivutio vingi vipo lakini havitumiki kwa shughuli ya utalii.

Mheshimiwa Spika, inaeleweka wazi, wakati wa Awamu ya Kwanza na nusu ya Awamu ya Pili, Kusini tulikuwa vitani, tulikuwa tunapambana na nchi zilizokuwa bado hazijapata uhuru na wawekezaji wengi hata Serikali yenyewe, ilikuwa inaogopa kuwekeza Kusini, kwa kuogopa kama wakiwekeza miradi hiyo itabomolewa. Leo hali hiyo haipo, Kusini kote wamepata uhuru, lakini hali hiyo inaendelea, vivutio vingi vilivyoko Kusini havitumiki kwa maendeleo toka Mkoa wa Lindi, Mtwara hadi Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, tatizo liko wapi, hali hiyo itaendelea mpaka lini, ni kweli kuna mambo muhimu yanayotakiwa ili utalii uendelee, miundombinu kama barabara, umeme, maji inahitajika, miundombinu hiyo kweli ina hali mbaya, kama Wizara inahitaji kueneza utalii nchi nzima na wanatekeleza shughuli moja ya utengenezaji wa barabara na hicho ni kikwazo kimojawapo, sioni kwa nini Wizara haiwezi kuwekeza kwenye miundombinu barabara ili vivutio vilivyojaa Kusini viweze kutumika kwa watalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano wa Mbinga, tuna jiwe kubwa sana naona linaongoza Afrika, linaitwa *Mbuji,* ni kivutio kimoja kikubwa sana. Tuna vivutio vingine kama Milima ya Matengo. Kama umewahi kufika Mbinga, imefunikwa na kahawa, ina utamaduni wa kuchukua maji toka chini kabisa na kuyazungusha hadi milimani ili yatumike kumwagia kahawa. Ni vivutio vikubwa sana, ni teknolojia ya ajabu iko pale toka lini sijui, ni vivutio vikubwa. Tuna mwambao wa Ziwa Nyasa, tuna samaki wa mapambo, tuna vivutio kama Lipalamba Pori la Akiba, hivi vyote vikitumika vikaweza kutambulika na kutangazwa, vinaweza vikasaidia sana kuboresha mapato ya utalii nchini. Lakini sisi nchi imeng'ang'ania vile vile vituo vilivyokwisha tambuliwa toka miaka nenda rudi na wanawekeza hapo hapo na wanaboresha hapo hapo, lakini miundombinu mingine katika sehemu nyingine imebaki kama sio maliasili ya nchi hii. Naiomba Wizara ibadilike iwekeze sehemu hizo. *(Makofi)*

Tunahitaji maendeleo na maendeleo hayawezi kupatikana kama miundombinu na hivyo vitu nilivyovitaja, vivutio hivyo, kama haviwezi kutambulika Tanzania yenyewe na hata kiulimwengu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kulitambua Pori la Lipalamba na kulitengea fedha kwa ajili ya kuliendeleza. Lakini tuna tatizo moja la miundombinu barabara, barabara ya kutoka Mbinga kwenda Lipalamba sio nzuri ningemwomba Mheshimiwa Waziri, kupitia kwako, awekeze katika barabara ili kulipa hadhi Pori hilo la Akiba la Lipalamba, liweze kutambuliwa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie juu ya uvuvi. Juzi juzi tu nimeuliza swali hapa juu ya wavuvi wetu wa Ziwa Nyasa, kwa nini wavuvi hawa wasifutiwe leseni za

mitumbwi na nyavu na inafahamika wazi, kufuatana na taarifa, Wizara inatamka kuwa Ziwa Nyasa halina samaki na hao wavuvi sio kama wanavua kibiashara, wanavua ili waweze kupata tu chochote ili waweze kuishi. Sasa kweli mwananchi ama mvuvi huyo, anaitwa mvuvi kwa sababu anashughulika na kuvua samaki, lakini kwa kweli sio mvuvi ila ni mtu tu anahangaika ili kujisaidia katika maisha. Naiomba Serikali iondoe kero hiyo, iwaondolee leseni hao wavuvi wanaotumia mitumbwi na nyavu kwa kupata samaki ili waweze kuishi. Serikali imeshakiri kama ziwa lile halina samaki na inaonesha wazi wazi mipango yote ya maendeleo haiendi Ziwa Nyasa, ni kutokana na ziwa lile halina samaki, kuna mpango mzuri tu wa uhifadhi wa mazingira ya bahari ya shilingi bilioni 62.75 na hii sehemu ni mkopo na sehemu ni ruzuku na hii itatumika kuwakopesha wavuvi wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini hii isitolewe hata sehemu walau hata shilingi bilioni mbili katika hiyo shilingi bilioni 62.75 kwa wavuvi wa Ziwa Nyasa. Toka tuzaliwe hatujapata msaada wowote toka Serikalini kwa ajili ya wavuvi. Nini hasa tatizo, tuambiwe. Serikali iseme kama maji ya Ziwa Nyasa siyo yetu, wanaogopa kuwekeza kwa sababu maliasili maji sio yetu, watuambie. Serikali itamke hilo maana ni ajabu miradi yote inaelekezwa maziwa mengine, inaelekezwa pwani na mradi mkubwa kama huo nao unaelekezwa sehemu nyingine, lakini hakuna mradi wowote ulioelekezwa Ziwa Nyasa. Wale wavuvi ingawa wanavua kwa kuishi watakwenda wapi; watategemewa nini na mwisho wake itakuwa nini?

Mheshimiwa Spika, Ziwa Nyasa lina tabia ya ajabu ni tofauti kabisa na Maziwa kama Victoria na Maziwa mengine, Ziwa Victoria maji yanapungua, ukiangalia gati zilizokuwa zinatumika nyingi tu ziko nchi kavu maji yanapungua. Lakini ajabu ya Ziwa Nyasa, maji yanajaa mabonde yote yaliyoko karibu na ziwa yanakwisha, yanamezwa na maji. Ningeiomba Serikali, ifanye utafiti tatizo ni nini? Mwisho mabonde yatamezwa na maji na watu watakosa sehemu hata ya kuishi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo ningeomba sana Wizara ifanye utafiti na la kumalizia kama nilivyosema, hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni nzuri, imechambua utekelezaji wa mwaka wa fedha 2004/2005 vizuri kabisa, kwa undani kabisa na mipango yake ya mwaka 2005/2006 iko wazi kabisa na ninawapongeza sana kwa hilo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu kwa mipango yao mizuri.

Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia machache kwa leo na ninakutakia afya njema na maisha marefu. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri, Makatibu na Wataalamu wa Wizara, kwa kazi zao nzuri. Ninawaombeeni muendelee hivyo ili nchi yetu iweze kusonga mbele, lakini msisahau Mikoa ya Kusini, muendeleze utalii Kusini, muendeleze uvuvi Kusini ili Kusini nako kuweze kufahamika katika nchi hii, iweze kutoa michango inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, asilimia mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Kwanza kabisa, napenda na mimi niungane na wenzangu kwamba, hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni nzuri sana, imeeleza mambo yote yaliyopangwa yafanyike na yamefanyika. Kwa misingi hiyo basi, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu wake na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa hotuba hii. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, napenda niungane na Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga kwamba, inaelekea sasa umejengeka utamaduni kwamba, utalii maana yake ni Mlima Kilimanjaro na hili limejionesha moja kwa moja na hoja ya upande wa Upinzani. Wametumia zaidi ya nusu ya masuala yote yakielezea Mlima Kilimanjaro, kama vile ndio utalii peke yake. Kwa hiyo, naomba kabisa tafadhali hili suala pamoja na kwamba ni Mlima Kilimanjaro ni sahihi, lakini utalii hauwezi ukawa endelevu kwa kuangalia kivutio kimoja.

Kwa misingi hiyo, naomba na ninakubaliana na Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga kwamba, sasa lazima tupanuke, tuangalie yale maeneo ambayo yana vivutio lakini bado havijatangazwa na mimi naweza nikasema hapa wazi kabisa, wataalamu watanisamehe hapa. Nikiuliza leo katika miaka mitano, ni wataalamu wangapi wametembelea Mikoa ya Kusini, inawezekana ni mmoja au wawili, wengi hawajaenda huko. Kwa hiyo, safari zote zinaelekezwa eneo moja. Ninaomba kwa kuwa mimi ni lala salama, ninawasamehe lakini ningependa suala hili likae kwenye kumbukumbu na ninamtakia Mheshimiwa Waziri, arudi tena ili moja ya mambo ambayo namwomba ayazingatie akijaliwa na ninaamini atajaliwa kurudi tena, basi liwe ni hilo kuangalia kwamba, hata zile sehemu ambazo zina vivuti vizuri na hazikupewa vipaumbele, basi hili liwe moja ya vipaumbele vyake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda niungane vilevile na Mbunge wa Kiteto kuhusiana na suala la maeneo ya Hifadhi ya Jamii *(WMAs)*. Kwa hakika sioni kama palikuwa na umuhimu wowote wa kuanza kutunga taratibu za kudhibiti maeneo kabla hayajaanzishwa. Kwa sababu kufanya hivyo kweli ni kupunguza kasi ya kuanzisha maeneo, Wananchi wengi wamehamasika sasa, badala ya kuwapa motisha inaelekea tunawadhibiti na naungana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, udhibiti huo inaelekea ni shinikizo kutoka kwa wale ambao wananufaika sasa. Sasa isije ikawa kwa mtindo huo, tutafikia mahali tutakapoona sasa mambo ndio yanaanza kuwa mazuri tutajikuta kwamba, maeneo ambayo sasa hivi bado yana wanyama wa porini watakuwa wamekwisha. Kwa sababu utaratibu huu ulipoanza ulikuwa ni kuhamasisha watu ili yale maeneo ambayo hayana hadhi ya kihifadhi, Wananchi wachukue majukumu na walifanya hivyo na katika maeneo mengi wanyama wameanza kurudi na hivyo kuongeza uwanja wa hifadhi tena kwa hiari.

Mheshimiwa Spika, sasa ningeomba Wananchi tuwape, tutangaze pale wanapotaka kuanzisha waanzishe halafu wakishaanzisha iwe ni juu ya wataalamu kwenda kuwasaidia na siyo kuanza kuwatungia sheria ambazo zitawafanya wasiweze kuanzisha haya maeneo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba sasa nizungumzie suala moja ambalo ninaamini kabisa kwamba ni suala la uhai wa nchi yetu, linalohusiana na Uhifadhi Maliasili. Napenda kwa namna ya pekee, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa sababu miaka ya nyuma Wizara ya Maliasili na Utalii, ilikuwa na migogoro mikubwa sana hasa katika masuala ya ugawaji wa vitalu vya uwindaji, utoaji wa leseni za uvuvi na kadhalika. Nashukuru kwamba, migogoro hii sasa hivi kwa kweli haipo, kwa hilo ninapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme wazi, kimsingi sekta zote zinazojumuisha zimefanya vizuri, lakini sina budi kuisemea sekta moja nayo ni sekta ya misitu. Takwimu zinaonesha kwamba, tunayo misitu minene kama asilimia 2.9 na hii misitu ya waziwazi kama *Open Wood Lands* ni kama asilimia 39.6. Lakini vilevile inasemekana kwamba, kiasi ambacho misitu hii inaharibika kinatisha, kuanzia hekta laki mbili mpaka laki tano kwa mwaka. Sasa nimesoma vilevile idadi ya miti ambayo tunapanda, kwa mfano, miti iliyopandwa mwaka 1993/94 sasa sielewi kama hii ndiyo inafanana na kiwango ambacho tunafyeka hiyo misitu.

Mheshimiwa Spika, kama suala la upandaji misitu halitapewa uzito wa namna ya pekee, basi ni dhahiri kabisa kwamba, nchi hii itakuwa inajinyonga yenyewe, tunaanza kukinyonga kizazi cha sasa. Matumizi ya misitu ni makubwa sana, sina uhakika na uhakiki wake. Zamani kazi ya kupanda misitu ambayo sasa hivi tunaivuna ilikuwa ni ya Serikali, bwana misitu alikuwa anaheshimiwa kwa kupanda miti, kuisimamia na kushirikiana na Wananchi. Serikali au Mamlaka za Wenyeji *(Local Government)* wakati ule walikuwa na misitu yao, leo nina wasiwasi sijui kama misitu ipo, kazi ambayo inafanyika sasa hivi ni kuvuna. Pengine Mheshimiwa Waziri, atatuambia baadaye kwamba, hiki kiasi tunachopanda, je, kinalingana na kiasi tunachovuna na je, miti yote tunayopanda inakua? Nakipongeza sana Chama cha Mapinduzi, kwa kuchagua rangi ya kijani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bendera ya Chama cha Mapinduzi ni kijani na mimi ningependa kuona kwamba, nchi hii hatimaye inakuwa kijani. Mheshimiwa Waziri, ningependa kushauri kwa upande wa Serikali, inafahamika kwamba, asilimia 90 ya nishati inategemea misitu, watu wanachoma mkaa, watu wanakata magogo na kadhalika. Ziko Taasisi za Serikali kama magereza, mashule, wanajeshi, hizi Taasisi zinatumia sana kuni. Kilimo na mifugo ni moja ya maeneo ambayo yanapunguza maeneo yote ya misitu.

Sasa sipingi mfumo wetu wa sasa hivi, naogopa kwamba, suala la usimamizi wa misitu kule kunakohitajika hasa ngazi ya vijiji haupo. Baada ya kuwapeleka wataalamu wa misitu kwenye ngazi za Wilaya hakuna wataamu wengine wanaoajiriwa, waliobaki wamezeeka, huu ndio ukweli. Sasa sijui kama Wizara hii kama ndio chombo cha Serikali chenye dhamana ya kuangalia misitu yote kwa ujumla wake, kwa sababu baadaye atakayelaumiwa ni Mheshimiwa Waziri, mwenye dhamana ya misitu na siyo mamlaka nyingine. Sasa kule mambo yanapoharibika inakuwaje tunaacha hivi hivi? Ningeshauri ifikie mahali, tufanye sasa tathmini, je, huu mfumo tuliokuwa nao kweli utasaidia kuongeza misitu yetu au unapunguza misitu yetu?

Mheshimiwa Spika, suala la uharibifu wa misitu katika nchi hii ni suala ambalo kila mtu analiona, lakini hakuna anayetaka kuchukua hatua za dhati kabisa kuhakikisha kwamba, tunajenga utamaduni wa kwamba labda baada ya miaka 10 nchi yetu iwe ya kijani. Nashauri kwamba, hizi Taasisi kama magereza na mashule, wawe na mashamba yao na Serikali nayo irudie tusidanganyane hapa, hakuna mfanyabiashara sasa hivi atakayeenda kuwekeza kwenye misitu, ambayo anajua kwamba atavuna baada ya miaka 20 au 40. Nadhani Serikali lazima ibadilishe mfumo wake kuhakikisha kwamba, suala la kuiweka nchi hii kuwa ya kijani liwe ni la msingi kabisa, la Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa mchango wangu huu, napenda nichukue nafasi hii tena, niseme wazi kabisa kwamba, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na napenda vilevile kuwashukuru sana yeye mwenyewe, pamoja na watendaji wote, kwa kazi nzuri wanayofanya. Lakini suala la misitu, bado nasisitiza kwamba, Serikali ijipange upya, mfumo wa sasa hauleti tija katika Idara ya Misitu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, nami asubuhi hii nichukue nafasi ya kukushukuru kwa jinsi ya pekee, kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nichukue nafasi ya pili, kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, pamoja na Katibu wake Mkuu, Ndugu Salmon Odunga, Wakurugenzi na Watendaji wote, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika kufikisha malengo na majukumu ya Wizara waliyopewa na Taifa hili. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze kwa jinsi ya pekee, ambapo Wizara ya Maliasili na Utalii imeweza kuchangia Pato la Taifa kwa asilimia 16. Huu ni mchango mkubwa sana na ambao unaonesha kwamba, Watumishi wa Wizara hii na uongozi mzima, wana mshikamano na wako kifua mbele kutetea maslahi ya umma wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kumpongeza vilevile Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Anne Makinda, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika kuisimamia Serikali hususan Wizara hii ya Maliasili na Utalii, nampongeza sana. Mama huyu ni mwenye uwezo mkubwa wa akili, busara na utulivu na sisi tunajivunia kwa kazi yake nzuri anayoifanya. Namwombea mafanikio katika Jimbo lake na utumishi wake kwa Wananchi wetu katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Napenda kuanza na yale yanayohusu Jimbo langu kule Same. Ya kwanza ni kero ile ya Mbuga ya Mkomazi Umba, ambayo Mheshimiwa Waziri humu ndani wakati akijibu swali nadhani mwaka 2004, aliahidi kwamba, mbuga ile ingekuwa Hifadhi ya Taifa *(National Park)*. Lakini sisi tulipeleka maombi rasmi, kupitia vikao vinavyostahili yapata miaka mitatu sasa na bado uamuzi haujafikiwa na Mheshimiwa Waziri, aliahidi

hapa kwamba, mwaka 2005 ile mbuga ingekuwa *National Park.* Nimesikitika kuona kwamba, nimesoma hotuba yake yote mstari kwa mstari sijaliona hilo, ningemwomba leo alisemee hili Wananchi kule Same wanasubiri. Leo tarehe 18 Julai, 2005, akiwasilisha hotuba yake, angesema kitu kuhusu Hifadhi ya Mkomazi Umba kwamba, hatma yake imekuwa vipi maana aliahidi mwaka huu?

Sasa mwaka wa fedha unakwisha tunaingia katika uchaguzi na Serikali nyingine mpya itaanza na ninakumbuka Mheshimiwa Rais, alipotembelea Wilayani Same pale, aliwaahidi Wananchi kwamba, wapeleke maombi yao kupitia vikao sahihi ili waweze kupatiwa *National Park.* Kwa nini tunadai *National Park?* Tunahitaji *National Park* kwa sababu kwanza, eneo lile ambalo limeshikwa kwa ajili ya kuhifadhi wanyama wale na mazingira ni kubwa sana na Wananchi wameachia mashamba yao na makazi yao kwa ajili ya hifadhi hiyo. Lakini tunapoingia katika kipindi hiki cha MKUKUTA, sisi tuna imani kwamba, kwa kuwa na *National Park,* tutaweza kukuza uchumi wa Same, ambao hivi sasa umedorora sana. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri, kwa sasa hivi tunapoingia katika Mpango huu wa MKUKUTA, atuhakikishie hapa leo kwamba, Same itapata ile mbuga kuwa Hifadhi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo Mheshimiwa Waziri aliahidi kuhusu mbuga hii na Wananchi wanaoizunguka mbuga hii ni kuhusu Bwawa la Chato. Hili bwawa tuliomba Wizara iweze kutoa msaada wa kulichimba na likaandikwa andiko na gharama zikapelekwa Wizarani yapata miaka miwili iliyopita kuwa, zinahitajika shilingi za Kitanzania milioni 455. Mheshimiwa Waziri, alidai kwamba, fedha zile ni nyingi sana kwa Wizara yake kwa hiyo na sisi tukajishughulisha tukaiomba Wizara ya Maji na Mifugo itusaidie na Waziri wa Maji na Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, akakubali kwamba, gharama zote za ufundi na kitaalamu, Wizara yake itaweza kuzilipia kwa kutoa wataalamu na kusimamia ile kazi, fedha ambazo ni karibu shilingi milioni 160. Kwa hiyo, inapunguza zile gharama za shilingi milioni 455 na sisi kule kwa ujumla wetu, kiwilaya tukasema tutachangia shilingi milioni 100 na wadau ambao wako katika ile mbuga nao wakakubali kutushiriki ili tuweze kupata shilingi milioni 100. Sasa yapata miaka miwili, Wizara hii imekaa kimya.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni makini sana na mimi sina wasiwasi na Mheshimiwa Zakia Meghji, ni Waziri ambaye ana uwezo mkubwa, lakini sasa kwa nini anafumbia macho maendeleo ya kule Same. Nashangaa na yeye mwenyewe anaelewa kwamba, lile bwawa lilikuwa muhimu sana kwa ajili ya wanyama wa ile hifadhi. Lilikuwa muhimu sana kwa ajili ya jamii inayozunguka pale na lilipokauka wanyama wengi walihama kwenda *Tsavo National Park,* ambayo iko Kenya. Kwa kukosa maji na wakati ule kwa ajili ya kuwindwa, sasa imekuwa ni hifadhi, wanyama wana-*migrate* kwenda *National Park* ya jirani wakitafuta maji. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri, atuasaidie bwawa lile lijengwe katika mwaka huu wa fedha, kwa sababu fedha alizokuwa ameona ni mzigo mkubwa kwa Wizara yake, sasa amepata msaada wa karibu shilingi milioni 260. Sasa siamini kwamba, Wizara yake kwa jinsi ilivyo na mapato inayoweza ku-*generate* kwa Taifa letu, basi Mheshimiwa Waziri atashindwa kiasi cha shilingi milioni mia mbili na kitu zilizobaki. Namwomba sana, kwa siku ya leo aweze kutupatia majibu kwa sababu Wananchi kule wanasubiri kupata jibu kwa sababu gani bwawa lile halijajengwa?

Mheshimiwa Spika, la tatu ni kuhusu kituo cha Mradi wa Misitu cha *Jica* pale Same. Kile kituo kilianzishwa kwa mradi wa Wajapan kwa ajili ya kukuza mazingira na misitu pale Same na pale Same ni jangwa sana ukipita barabarani. Lakini baada ya mradi ule kwisha kituo kile kikatelekezwa, nasema kimetelekezwa, inawezekana nikalitumia neno hili katika hali ambayo ni kavu kavu sana, lakini nafikiri nakosa neno laini zaidi ya hilo. Kimetelekezwa kwa sababu sasa Wizara imeanza kuchukua rasilimali moja moja ya ule mradi, walianza kuchukua Basi sijui wamelipeleka wapi na leo ningependa kufahamu lile Basi limepelekwa wapi na kwa nini?

Ya pili, wakaja wanataka kuchukua ile *escavator* ndogo ambayo ndio lilikuwa linatumika kwa ajili ya kukuza mazingira na misitu pale. Sasa wanachukuwa kimoja kimoja kana kwamba watu wa Same hawakuwa na hitaji la ule mradi. Miradi ya Kitaifa inapoanzishwa na inapokwisha, nategemea Wananachi pale mradi ulipoanzishwa ndio wa kwanza kunufaika na kubakia na ule mradi, sasa ni vipi mnagawana nchi nzima mradi mdogo kama ule!

Ningependa Mheshimiwa Waziri, anipatie majibu Wananchi wamekuwa wakiliuliza sana hili, kwamba huu mradi uliletwa hapa kwa ajili ya hali ilivyo ya mazingira kuwa mabovu na misitu kukatwa ovyo ovyo lakini sasa vifaa vyake vinachukuliwa. Mwisho kabisa, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, achukue hatua za madhubuti kabisa za kuhakikisha kile kituo hadhi yake inarejeshwa. Same inakuwa jangwa, kile kituo tukitumie katika njia fulani ya kuweza kukuza mazingira, pamoja na misitu. Nina imani akishirikiana na Waziri mwenye dhamana ya mazingira, pamoja na yeye mwenye dhamana ya misitu, wanaweza kufanya kitu ambacho watu wanaopita katika ile *highway* wa Kitaifa na Kimataifa, wataona Serikali yetu inawajali watu wake na inajali mazingira ambayo ni *agenda* ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia katika hoja hii kidogo limeongelewa na mzungumzaji aliyepita na mimi nisingependa kutumia muda mwingi hapa. Ni kuhusu hifadhi na kukuza misitu. Misitu yetu inakwisha kwa kasi kubwa sana zaidi ya tunavyopanda, hata Mheshimiwa Waziri, katika ukurasa wa 55, jedwali Na. 4, ameweza tu kutoa miti wanayopanda lakini hawezi kueleza kwa takwimu ni kiasi gani misitu yetu inaharibika.

La pili, ninashindwa kuweka tofauti kati ya Waziri mwenye dhamana ya misitu na yule mwenye dhamana ya mazingira. Hao wanaochoma mkaa kwa ajili ya kuuza na ninaambiwa sasa mkaa unauzwa nje ya nchi, imekuwa ni biashara, kwa nini tunaruhusu hili na linaandikwa kwenye magazeti na Serikali iko kimya. Wanachukua mkaa wanapeleka Tanga wanapakia kwenye mashua wanapeleka Zanzibar, mwingine unaondokea Tanga unakwenda Dubai, unakwenda nchi za nje, sisi tunabaki na mazingira tupu. Serikali imechukua hatua gani na ina mpango gani wa kudhibiti hili suala la mkaa? Watu wetu maskini wanapotumia mkaa kwa ajili ya kuuza nje kwa kweli hilo ni kosa la jinai, ni kosa kubwa sana na je, Sheria zetu zinaruhusu?

Mheshimiwa Spika, ningeomba Mheshimiwa Waziri, aweke mfumo wa kuratibu shughuli za utalii vijijini, huko ndipo mahali watu wetu walipo ili nao waweze kufaidika na shughuli za utalii katika nchi yetu. Watu wa nje wanapenda sana kufahamu mambo yetu ya humu ndani na kama watu wa nje wanapenda kufahamu mambo, basi yako huko vijijini na angewekea uratibu kuanzia Wilayani, Mikoani, kwenye Kata na Vijiji, nina imani kwamba, hili lingeweza kutusadia sana katika kuboresha uchumi wetu wa Vijijini.

Mheshimiwa Spika, sasa la mwisho ni kuhusu vyuo vyetu hivi vinavyofundisha vijana wanaohusika na shughuli za hoteli na utalii. Hivi vyuo vyetu kwa kweli ni *substandard,* kama taarifa ilivyoeleza, sasa tunachukua wapishi kutoka nje kwa ajili ya kuja kupika labda *Italian Pizza.* Kwa nini tusichukue walimu wa kutoka nchi za nje wakaja kufundisha katika shule zetu za kitalii ili vijana wetu wa Tanzania waweze kupika *Italian Pizza,* siyo hapa ndani ya nchi yetu tu lakini na nje ya nchi. Badala yake sisi tunasema bora kuajiri Mtaliano, bora kuajiri Mchina, bora kuajiri Mkorea, kwa sababu anaweza kupika hiki. Hivi Watanzania wetu wakifundishwa hawawezi kupika *Italian Pizza?* Sasa hivi vijana wetu wanalalamika hawana ajira lakini tunaachia milango wazi kwa ajili ya ajira za nje. Ningekuomba Mheshimiwa Waziri, ukaliangalie hilo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kuhusu utalii, ukiangalia pale katika jedwali Na. 8, 9 na 10, mapato ya uwindaji ni kidogo sana kulinganisha na mapato ya utalii na hizi kampuni za uwindaji zinazidi kuwa nyingi. Namwomba Mheshimiwa Waziri, aliangalie hili, wanyama wanakwisha, je, kasi ya wanyama wanavyowindwa na watalii wetu wanapokuja inaangaliwaje?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda unanitupa mkono, napenda kuchukua nafasi ya mwisho, kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, kwa kazi nzuri ambazo ametufanyia, sisi Wabunge wote tunajisikia ni baba yetu, ni kiongozi wetu bila upendeleo. Nakuombea kila la kheri kwa Mwenyezi Mungu, aweze kukupa baraka na mafanikio ya kipindi hiki na kipindi kijacho kwa sababu nakuona bado nguvu unazo. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, nimalizie kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na kumwomba Mheshimiwa Waziri, aweze kutoa majibu ya zile kero nilizozieleza ili Wananchi waweze kupata majibu. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia kwenye hoja ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia kwenye hoja ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, mimi nimelelewa kwenye Wizara hii na katika miaka hii mitano ambayo nimekuwa hapa karibu kila mwaka nimezungumza neno kuhusiana na Wizara hii na nakushukuru kwa vile nimepata fursa leo ya kuweza kuchangia miwili au matatu.

Lakini nianze kwa kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Zakia Meghji, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara kwa kazi nzuri ambayo inaendelea na ushahidi wa kazi hii nzuri umo katika majedwali yaliyoambatanishwa na hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambayo *indications* zote zinaonyesha kuna *improvement* kubwa sana. Tunawapongeza kwa kazi nzuri ambayo mmekuwa mkiifanya. *(Makofi)*

Pia tunakupongeza Mheshimiwa Waziri kwa vile katika kipindi hiki cha Bunge hili umetuletea hapa mabadiliko makubwa ya Sheria ya Misitu ambayo tuliipitisha, Sheria ya Uvuvi ambayo tuliipitisha hapa na Sheria ya Ufugaji Nyuki ambayo pia tuliipitisha wanayosema ni sheria ya aina yake Afrika nzima.

Lakini bado iko sheria ya Wanyamapori *(The Wildlife Act)* ambayo bado haijafika hapa tunaendelea kukumbushia, tunajua kabisa kazi kubwa inafanyika kwenye Wizara ya kuandaa Sheria hii huenda mwishoni mwa mwaka huu katika kikao kitakachofuata hasa Januari, 2006 sheria hii nayo ikaletwa hapa ili wanyama wetu waweze kupata fursa ya kuweza kulindwa vema kupitia sheria rasmi ya wanyamapori na wakati huo huo mabadiliko na marekebisho ya sheria za *TANAPA* na Ngorongoro tunazitarajia pia nazo zitakuwa zinafanyiwa maandalizi kwa siku zijazo.

Nimpongeze sana Mama Anne Makinda, Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Maliasili na Mazingira kwa uongozi wake mzuri na kwa kweli tumejifunza mambo mengi kutoka kwa Mwenyekiti wetu wa Kamati. *(Makofi)*

Mimi mchango wangu uanze na suala la chura wa Kihansi. Najua kabisa chura hawa hawako chini ya Wizara hii uko chini *NEMC,* lakini taarifa ambazo tumepata hivi karibuni zinasema kwamba chura hawa wameisha kabisa, sina hakika ya taarifa hiyo ukweli wake ni kiasi gani kwa hiyo tegemeo letu limebakia kwa wale chura waliokuwa wamehifadhiwa Marekani peke yake.

**MBUNGE FULANI:** Vyura.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Vyura. Nashukuru sana.*(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo mtu anaweza kulitazama kiharaka haraka akaona la kawaida, lakini ni jambo la ajabu kabisa. Mimi nasema *NEMC* wameshashindwa, lazima wakubali kwamba wameshindwa ku - *manage* Kihansi, sasa *NEMC* wakabidhi, naishauri Serikali wakabidhi shughuli ile kwa Wizara ya Maliasili na Utalii na hasa Idara ya Wanyamapori kwenye kitengo kinachoshughulika na masuala ya maeneo ya majimaji wanaita chepechepe ili tuwe na uhakika wa uhifadhi wa vyura hawa.

La pili, tunao utaratibu ambao umezoeleka sana katika Wizara hii wa kutoa asilimia 25 ya fedha zinazotokana na uwindaji wa kitalii kwenda katika baadhi ya Wilaya husika. Ushauri wangu ni kwamba jambo hili litazamwe upya, Wizara ikae chini iangalie namna bora zaidi ya kuendesha jambo hili kwa vile fedha hizi zimekuwa zikitengwa kila mwaka zinakwenda katika baadhi ya Wilaya nchini japo wanyama ni wa nchi nzima

lakini baadhi ya Wilaya zimekuwa zikifaidika lakini matumizi halisi ya fedha hizi yamekuwa hayana maelezo mazuri.

Lakini baadhi ya Wilaya zinapata *multiple funding* ambazo ziko karibu na hifadhi za Taifa wanapata kutoka *TANAPA,* ziko karibu na *Game Reserve* Wilaya hiyo hiyo inapata *Wildlife Department* bila kupitia *Tanzania Wildlife Professional Fund* na Wilaya hiyo inaweza ikapata kutoka kwenye hii asilimia 25. Kwa hiyo, matokeo yake baadhi ya wenzetu wanafaidika zaidi ya wengine kwa hiyo, iko haja ya kutazama suala zima za *equity* kwa vile raslimali hii ni ya Taifa zima ni kweli hawa waangaliwe zaidi kidogo lakini pia isiwanyime fursa wengine kuweza kufaidika kutokana na raslimali hii ambayo kwa kweli kimsingi ni ya nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa tatu unahusiana na suala la hifadhi za kijamii zinazoitwa *Wildlife Management Areas* ambazo Mheshimiwa Waziri mwaka jana au mwaka juzi alizindua *regulations* zake. Ni wazo zuri na ninaipongeza Wizara kwa kwenda taratibu katika kutekeleza jambo hili kwa vile ni jambo jipya, lakini tukubaliane tu kimsingi kwamba wanyama nje ya hifadhi wanaisha, tena wanaisha kwa haraka sana, kwa hiyo, tufike mahali tuone namna ya kutekeleza jambo hili.

Mheshimiwa Spika, pamekuwa na ugumu kidogo wa uanzishwaji wa *WMAs* kwenye maeneo ambayo hivi sasa kisheria ni *Game Controlled Areas.* Ningelishauri hilo jambo litazamwe vizuri ili kurahisisha baadhi ya maeneo ambayo ni *Game Controlled Areas* kuweza kuwa *Wildlife Management Areas,* lakini ushauri wangu ni kwamba tuendelee kwenda taratibu na jambo hili kwa vile wanyamapori ni raslimali ambayo inaweza ikaisha haraka sana endapo tu maamuzi fulani fulani yanaweza yakafanywa kwa haraka bila kuzingatia na kutazama taratibu muhimu zinazoendana na ulinzi wa maliasili hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu hasa iliyonifanya nisimame leo ni kuzungumzia sekta ya wanyamapori kwa upana wake. Mapori ya akiba katika nchi yetu na mapori ya hifadhi yanafikia *almost* asilimia 30 ya nchi hii, hayo ni maeneo makubwa sana na milima yetu muhimu iko humo katika kuhifadhiwa iwe ni Mpanga, Kipengele au iwe ni Kilimanjaro au *Mount Meru,* Maeneo ya Visiwa vya Lubondo na kadhalika. Maeneo ya hifadhi za kawaida za mbuga ni maeneo ya hifadhi za kawaida za mbuga ni maeneo makubwa sana.

Katika uchumi wetu na katika matumizi ya fedha zetu sisi Watanzania tumekuwa tukijali sana Sekta ya Huduma za Jamii, Elimu, Afya na kadhalika. Hili ni wazo nzuri kwa maana ya kupambana na umaskini kuwaondoa watu kwenye matatizo hayo. Lakini ukiwa mchumi mahiri unaiangalia sekta nyingine inayoitwa sekta ya Huduma za Kiuchumi kwa sababu Sekta ya Huduma za Kiuchumi ikikua matunda yake yatatawanyika kwenda kuibua sekta ya Huduma za Jamii, maana yake Huduma ya Jamii ukitumbukiza kwenye Afya fedha inakwenda moja kwa moja, ukitumbukiza kwenye elimu inakwenda moja kwa moja hairudi saa ile ile, haikuwezeshi mwakani kuwa bora zaidi katika kutatua matatizo yako ya umaskini.

Kwa hiyo, nashauri kwa Serikali ijayo ya awamu ya nne kuangalia sana Sekta za Huduma za Kiuchumi kuzitazama kipekee na hasa kwa mfano Sekta hii ya Wanyamapori. Wenzetu Kenya au hata Uganda wana *Ministry* kabisa, *Ministry of Wildlife and Tourism* na hawana *Wildlife* tuliyonayo sisi.

Kwa hiyo, nashauri maeneo kama haya yatazamwe yapewe nafasi ya kuwa hata Wizara kamili ili yaweze kuchangia ipasavyo katika uchumi wetu na yana uwezo huo mkubwa sana. Kwanza tuyatambue, tuyaibue, tuyawezeshe kwani yana uwezo mkubwa sana wa kuchangia katika kutuondoa katika umaskini mkubwa tulio nao.

Lakini ili uhifadhi uwe na maana na hifadhi zimekuwa zikiongezeka kila wakati ni lazima watumishi walioko katika hifadhi zetu mbalimbali ziwe ni Ngorongoro, *TANAPA* au Hifadhi zetu za Idara ya Wanyamapori, watazamwe vizuri watumishi wale.

Hili ni kundi la watumishi katika nchi hii ambao wanaishi katika mazingira magumu nadhani kuliko kundi jingine lolote lile. Aliwahi kuuliza Mheshimiwa Christopher Wegga, safari moja kwamba hivi hawa watumishi wa wanyamapori nao ni watumishi? Mtumishi yuko kule Lumisule, yuko Liparamba, Mpanga Kipengele, Brigi, Kimisi, Swagaswaga huko, Selui kule Migiruwe ndani kule, Madaba ndani ya *Selous* ni maeneo ya ndani kweli kweli wanaishi na wanyama. Baadhi ya maeneo hata maji safi ya kunywa hawana watumishi hawa, wanyama wanakunywa maji hayohayo na wao wanakunywa maji hayohayo.

Naishauri sana Wizara na Serikali kwa ujumla kuendelea kuwatazama sana Watumishi hawa kipekee, watoto wao wapate huduma ya Elimu ya Msingi na Sekondari. Kuna wengine hawatachukulia *Serengeti National Park* peke yake, kuna watimishi wa *Game Post* kadhaa, mtumishi yuko kule Tabora B, ndani kabisa hakuna cha shule ya chekechea wala kitu gani inabidi mtumishi apeleke mtoto wake nyumbani kwake alikotoka au aende akampangishie kwa ndugu yake mahali fulani au rafiki yake ili aweze kupata elimu.

Kwa hiyo, tutazame jambo hili, tusiliachie Wizara ya Elimu hili tulichukue wenyewe kama ni *challenge* yetu Wizara tuone ni namna gani watoto hawa watapata fursa ya kupata elimu wakiwa karibu na wazazi wao.

Kuna suala la Bima ya maisha ya watumishi. Tulisema suala moja la kule Gombe mwaka jana au mwaka juzi mama mmoja akipita na mtoto wake mmoja yuko mgongoni na mmoja akitembea naye kwa miguu bahati mbaya wale sokwe mtu wakamrukia yule aliyekuwa akitembea kwa miguu. Katika mama kumwokoa yule mtoto aliyekuwa akitembea kwa miguu yule wa mgongoni akachukuliwa na sokwe mtu akauawa yule mtoto. Lakini sheria zetu haziruhusu hata kutoa fidia fulani kwa familia za watumishi, kwa hiyo, nashauri hili litazamwe kipekee siyo tu kwa *TANAPA,* kwa Ngorongoro lakini zaidi zaidi kwa watumishi wa Idara ya Wanyamapori kwa sababu wao wanabanwa na Sheria za Serikali ambazo kidogo ni ngumu ngumu hivi tuzitazame kipekee, hawa ni watumishi ambao wako katika mazingira maalumu kabisa. Maisha yao na maisha ya familia zao yatazamwe vizuri kwa maana ya elimu ya watoto, kwa maana ya matibabu,

wapate chai kama walivyo watumishi wa mijini katika maofisi yao, wawe na ofisi nzuri, wawe na nyumba nzuri na naipongeza Wizara kwa sababu wanaanza kujenga nyumba nzuri sana kwa watumishi hawa wale ambao wako porini lakini waendelee kwa jitihada hizo. Wawe na magari ha uhakika na nina hakika kabisa Wizara ina uwezo huo na inafanya hivyo hivi sasa. Huo ndiyo ushauri wagu kwa upande wa watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko suala la uwindaji wa kitalii limekuwa likizungumzwa mara nyingi kwamba uwindaji wa kitalii unamaliza wanyama wetu. Nipende kusema kwamba *concept* hiyo si kweli, uwindaji wa kitalii ni uwindaji ambao ndiyo wa uhifadhi kweli kweli kwa sababu katika mahali kwenye tembo au ndovu 10,000 unaweza ukawinda kwenye hifadhi hiyo 10 tu, wale 10 kipato chake kinasaidia kuhifadhi hawa elfu kadhaa ambao wamebakia kwenye pori lile. Ni uwindaji muhimu, ni uwindaji ambao unachangia kwenye kiwango kikubwa sana pato linalowezesha kutusaidia katika uhifadhi, tukiondoa uwindaji wa kitalii hakuna tena uhifadhi katika nchi hii haiwezekani kwa hiyo, ni lazima uwindaji huu uendelee, ni uwindaji mzuri ambao hauharibu wanyama. Uwindaji unaoharibu wanyama ni huu wa kwetu sisi katika Wilaya, mtu anapewa leseni ya kuwinda swala mmoja anakwenda kupatika *pick up* nzima imejaa swala hilo ndilo tulitazame kwa leseni zinazotolewa Wilayani kwetu.

Mheshimiwa Spika, Milima ya Ukaguru inaisha mapangano yake katika Wilaya za Kongwa na Mpwapwa. Pamekuwa na mipango ya kulinda Milima ya *Usambara East,* Milima ya Uruguru, Milima ya Udzungwa, Kihansi na hii ya Uluguru ndiyo inaishia Kongwa na Mpwapwa. Milima hii imekuwa ikiathirika vibaya sana, ningeomba Wizara iitazame milima hii ya maeneo ya Kongwa na Mpwapwa kipekee ili na yenyewe iweze kupata hadhi ya kulindwa vizuri ili bayonuai iliyoko katika milima hii itufaidishe sisi tulioko sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho nimpongeze tena Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu Ndugu yetu Salmon Odunga, Mkurugenzi wa Wanyamapori Ndugu Emmanuel Severe, hongera sana umebadilisha Idara imefika mahali ambapo inaheshimika sasa, ndugu zetu wa Kenya wanakiri kabisa kwamba Idara ya Wanyamapori ni nzuri zaidi kuliko yao. Ndugu Lyimo, Paul Sarakikya na wengine wote nawapongezeni sana.

Mheshimiwa Spika, nasema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. HASHIM A. Z. SAGGAF:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niseme kuwa naunga mkono hoja hii mia kwa mia na vile vile nimshukuru Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kazi nzuri ambayo wanafanya na niwapongeze kwa juhudi zao za kazi hiyo wanayofanya. Mheshimiwa Waziri ana bahati ya kuwa na timu nzuri ambayo inamuunga mkono na ndiyo maana nadhani anafanya kazi zake kwa ufanisi.

Kuna utaratibu ndani ya Wizara ambao anauzingatia vizuri na anaufanyia kazi vizuri yeye na timu yake na kuna taratibu nyingine vile vile ambazo zimeundwa wakati yeye ni Waziri katika kipindi chake na kazi hizo vile vile chini ya utaratibu huo ameweza kuzifanya kwa ufanisi mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini nia yangu hasa ni kuhoji taratibu zenyewe ambazo nadhani ziko baadhi si nzuri sana na ndizo zinazopelekea kutunga sera ambazo nazo lazima zitakuwa hazitoshelezi.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijafika huko niseme machache tu juu ya *assets* hizi za utalii ambazo tunazo. Ukweli ni kwamba bado hatujaamka na kutambua umuhimu wa utalii katika nchi yetu. Mimi nimeishi Uingereza miaka 16 na wakati huo nimeona *aggression* na *PR* ilivyokuwa nzuri ya Wakenya katika kutangaza mali yetu sisi kama vile ni mali yao wao na tumeshaona ishara na tunajua jinsi walivyokuwa wanatangaza ya kuwa Mlima Kilimanjaro ni wao, Serengeti ni yao lakini wao wanafaidika wakati sisi tulikuwa tumelala.

Mheshimiwa Spika, tunajivunia tuna vivutio vingi vya asili kuliko sehemu nyingi sana duniani kama Ngorongoro, Manyara, Serengeti, Kilimanjaro na kadhalika, lakini bado mapato yetu kutokana na utalii hayalingani na thamani ya ukubwa wa *assets* hizi ambazo tunazo. Tunapata misaada mingi sana katika hifadhi ya wanyamapori na mazingira yetu kutoka nje lakini hata hivyo mahesabu tunayoyapata bado mimi nina wasiwasi nayo kidogo kuwa pengine siyo sahihi. Kasoro ziko wapi? Kasoro inatokana na sisi kutokuwa wabunifu, *imaginative* katika kutumia maliasili zetu na vile vile kutumia hii *asset* kubwa sana tuliyokuwa nayo ya utalii.

Mheshimiwa Spika, ukichukua Kenya kwa mfano, Kenya wanaichukulia utalii kama ni moja ya *Top Foreign Currency earness* za Taifa lao, si hivyo tu kwa miaka mingi utalii umekuwa ni *number one* katika *Foreign Earness,* katika *budget* yao ya mwaka. Na Uganda vile vile mwaka jana wameweza kufanya utalii ni *number one* katika mapato yao ya Kitaifa wakiwa wamepata zaidi kuliko mapato ya *Export* ya Samaki na Kahawa kwa pamoja na Uganda ni nchi ndogo tu hata bahari hawana. Lakini wameweza ndani ya mwaka mmoja mwaka jana kuongeza ujio wa watalii kutoka watalii zaidi ya laki tatu na zaidi mpaka laki tano elfu kumi na mbili za zaidi, ongezeko la takriban asilimia 50. Mbali na namna tunavyoelezwa katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri.

Sasa tatizo najiuliza liko wapi? Kwa nini sisi tumekuwa nyuma namna hii? Kwa nini maendeleo yetu sisi ya kitalii yako nyuma namna hii? Nadhani ni kwa sababu sisi siyo wabunifu na Mheshimiwa Waziri anajua mimi ni shabiki wake mkubwa. Lakini inabidi mara nyingine kwa sababu ya matatizo yamo ndani ya Wizara na malalamiko yako ni mengi sana inatubidi wakati mwingine tufungue masikio yetu tuwasikilize wale ambao wanazusha hoja ya kuwa pengine katika Wizara hii kuna zoezi la maslahi binafsi.

Mheshimiwa Spika, Thailand hawana vivutio vya utalii, kivutio kikubwa cha utalii Thailand ni *Sex Tourism.* Ni utalii wa ngono lakini kila mwaka wana *register* kitu kama bilioni 8 dola katika utalii. Mwaka 2000 kuamkia mwaka 2003 waliweka lengo ya

kuwa wafikie bilioni 8.5 na ulipofika mwaka 2003 wakashindwa kufikia wakapata bilioni 8 tu wakakosa ile nusu, Waziri wa Maliasili na Utalii ikabidi ajiuzulu kwa sababu ya kukosa ile nusu. Sasa najua sisi utaratibu huo hatuna lakini inaonyesha jinsi wanavyothamani utalii wenzetu wa nje.

Lakini hata Uturuki, Uturuki mwaka jana walipata bilioni 9 dola katika utalii peke yake na wana polisi kuwalinda watalii wanaitwa *Tourist Police.* Hawa polisi wa kawaida hawagusi wanawalinda watalii na wanawaheshimu kwa sababu ndiyo wanaowaletea chakula, lakini sisi kwetu kwa hakika watalii wanaokuja hatuwathamini, hawawezi kutembea mitaani mwetu wao peke yao lazima watembee kwa vikundi, polisi wanawanyanyasa, vibaka wanawanyanyasa na wakitoka nje kwa hakika wanatupelekea sifa mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, sasa labda nirudi kidogo tu kwenye yale ambayo yalikuwa hayanipendezi katika utaratibu ambao niliutaja awali. Mimi ni mwindaji na ni mmoja katika watu watatu ambao ni waanzilishi wa Chama cha Uwindaji Tanzania na vile vile kulikuwa na wakati ambao nilipata kuomba kitalu cha kuwindia kibiashara kwa bahati mbaya nilikosa lakini hayo ni mengine. Ninachotaka kusema hapa ni kuwa ni haki ya kila Mtanzania Kikatiba awe na nafasi na uwezo wa kuweza kwenda kuwinda na ndiyo maana tokea Uhuru mbali na *Game Reserves* na *National Parks* na kadhalika yametengwa maeneo maalum kwa Wazalendo ambayo yanaitwa *Open Areas* ili Watanzania kwa mila yao na desturi zao waweze kuwinda. Kwa bahati mbaya hizi *Open Areas* hivi sasa zinaingiliwa kwa kasi sana na zinagaiwa, zinakatwakatwa kama vitalu na wanapewa wafanyabiashara wa nje.

Mheshimiwa Spika, niseme tu katika *Wildlife Policy* ya mwaka 1998, huyu mwindaji mzalendo si mdau. Si mdau hata kidogo pamoja na kuwa katika *policy* hiyo hiyo inatajwa na nataka ninukuu inasema: *"It the right of the indigenous Tanzanians to have legally excess to wildlife"* na inaendelea kusema: *"It is the right of Tanzanians Citizens to have legal excess to utilize wildlife."* Kwa bahati mbaya kuna *contradiction* katika *policy* hiyo kwa sababu chini ya *Community Based Conservation* mdau siyo mwindaji mzalendo na vigezo vilivyowekwa katika orodha ya wadau wanasema ni *Sharing of Revenue* ambayo inatokana na wanyamapori kwa hiyo hao ndiyo wadau lakini kwa makusudi kabisa mwindaji Mtanzania mzalendo ameachwa kwa makusudi kabisa ameachwa nje.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kuwa naye awe ndani ili na yeye ahesabiwe kama mdau kwa sababu na yeye vile vile ana *play a part* katika *management* ya wanyamapori pamoja na *protection* ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, ningemnukuu Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, alichosema Shinyanga mwaka 2001 mwezi wa Agosti. Alisema hivi na ninamnukuu: "Sera zetu tangu enzi za *TANU* maliasili ni mali ya Taifa la Watanzania na watu wake, siyo mali ya kabila au eneo au watu wa mahali fulani peke yao." Sasa katika hii *policy* ninayoizungumzia *Wildlife Policy* chini ya kichwa cha *user rights* na *permits* imetoka *Government Notice Number 543* ya mwaka 2002 mali asili imekuwa *transferred* kwa

wanavijiji peke yao, wao wai-*manage* na siyo Watanzania wengine na nadhani hili ni kosa.

Mheshimiwa Spika, hata *format* yenyewe hawazungumzii *management* ya wanyamapori, wanazungumzia *absolute ownership* wanawapa wanavijiji. Sasa mimi nasema Serikali inawagawanya wananchi na ni kinyume cha Katiba ya nchi hii kwa sababu kila Mtanzania ana haki kutumia mali asili ya wanyamapori na siyo wanavijiji peke yao.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi ni kuwa Wizara yetu haina utaratibu wa kutuhakikishia kuwa makampuni ya uwindaji ya kitalii hayatumii majina tofauti ili waweze kupata vitalu. Ninao mfano hai kabisa. Kwa mfano, kuna mtu anaitwa Gerald Pasanini yeye si Mtanzania, ana kampuni tatu hapa Tanzania, lakini anamiliki si chini ya vitalu 18 na kuna kampuni nyingine inaitwa *Tanzania Game Trackers* wanamiliki si chini ya vitalu 10 sasa Watanzania watapata wapi vitalu wao waweze vilevile kujikuza kibiashara.

Mheshimiwa Spika, isitoshe kuna maeneo kama vile Moyowowi, Muhesi, Kigozi, Kiziga na Ugala ambayo yako pembezoni na *Selous,* kuna watu wa nje ambao wamepata vitalu vyenye ukubwa wa *square kilometres 2800* yaani mpaka *European Union* wanatuambia bila kutustahi, wanatuambia *you people are mismanaging your natural resources* kwa sababu kitalu kimoja kiko baina ya *square kilometres 450* mpaka 500.

Mheshimiwa Spika, nilitaka niseme hayo lakini ningepedekeza ya kuwa *licence* zote hizi zirudishwe ili zigaiwe upya. Lakini hawa wazungu waliopewa vitalu hivi wamefanya hekima wameweza kuidanganya Wizara na wakapewa *Extension* mpaka mwaka 2009 eti kwa sababu wana *bookings* ndefu sana, lakini utafiti unaonyesha hakuna *out fitter* yoyote ambae ana *booking* inayozidi miaka 2. Lakini wamepewa mpaka mwaka 2009.

Mimi naomba hii irudi, hizi *licence* zirudi lakini vile vile pamoja na *licence* hizi kurudi naomba vile vile iwekwe *moratorium* kuhusu mapori yetu tuache ku-*export* mbao na magogo kutoka kwenye mapori yetu kwa miaka 30 inayokuja ili mapori yetu yaweze kupumua upya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ningependa nichukue dakika mbili au tatu zilizobaki kuwatangazia wananchi wangu ya kuwa safari hii mimi sitagombea Ubunge. Walinipokea vizuri, nimeishi nao vizuri, walinipenda, walinipa ushirikiano mzuri na mimi nawashukuru sana na nawatakia kila la kheri kwa sababu wamekuwa ni watu wazuri kwangu na mimi nimewapenda kwa kiasi changu tumeshirikiana vizuri sana. Ni matumaini yangu ya kuwa watakapomchagua mtu mwingine watakuwa makini na watampa ushirikiano mzuri kama walivyonipa ushirikiano mimi.

Mheshimiwa Spika, hapo hapo ningependa nikushukuru wewe kwa jinsi ulivyotuangalia na kutuongoza vizuri katika Bunge hili, niishukuru Serikali vile vile mawazo yetu mengi sisi Wabunge wameyapokea wameyaingiza katika sheria na katika

azma zote za Serikali niwashikuru vile vile Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mzuri tumependana, tumecheka, tumefurahi na tumeweza kuwahudumia wananchi vizuri. Kwa hiyo, na mimi nawatakia kila la kheri muweze kurudi hapa kama mlivyokuwa na ninawapa baraka zangu zote. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante nashukuru. Waheshimiwa Wabunge kipindi cha asubuhi kimefikia mwisho, wasemaji wa mchana watakuwa ni Mheshimiwa Henry Shekiffu akifuatiwa na Mheshimiwa Herbert Mntangi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.58 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii kipindi hiki cha mchana kuanza kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Kwa kuwa nilikwishatoa rambirambi zangu katika hotuba zangu mbalimbali, nianze moja kwa moja kuchangia katika suala la hotuba ya Waziri.

Awali ya yote nishukuru na kumsifu sana Waziri kwa kazi nzuri ambayo wenzangu waliopita kwa kweli wametaja maeneo na asilimia ambazo ameleta mafanikio katika Wizara yake. Pia vile vile nishukuru kwamba huwezi ukafanya kazi peke yako kama Waziri bila ya kuwa na watendaji wazuri. Namfahamu sana Katibu wake Mkuu Ndugu Odunga ni mchapakazi mzuri, ni mtu aliyetulia, hana makeke, anasikia maagizo. Kwa hiyo, kwa kweli naamini kabisa kwamba mafanikio ya Mheshimiwa Waziri ni mafanikio ya watumishi wote ambao walikuwa chini ya Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Lakini kwa utendaji wa Waziri mimi napenda kutamka kwa kweli sitasoma yale mafanikio yake maana yake Mama Fatma Said Ali Mchumo, asubuhi alieleza vizuri sana kuhusu sifa zake. Lakini nasema ni watu wachache katika utendaji wake na kwa sababu hiki ni kipindi cha mwisho cha lala salama, basi mimi sijui mwaka huu atapitia mlango gani. Kama ni Viti Maalum nasema wale wanaopiga kura basi wajue kwamba hiki ni chombo. Kama ameamua Jimbo basi nafikiri huko anakokwenda huyo anayemwendea aambiwe kwamba yupo ajue kuna chuma. Sasa niseme kwamba naamini utendaji utakuwa mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nisingependa kuchangia mengi kwa sababu katika hotuba ya Waziri yale mambo mengi ya Kitaifa yameelezwa vizuri sana. Sera imetekelezwa, dira imeangaliwa kwa undani na yote ambayo yameelezwa kwa kweli yameendana na sera za Wizara yenyewe na sera za Chama cha Mapinduzi pamoja na mipango iliyobuniwa na kuwekwa. Kwa sababu si rahisi kwa Waziri kuzungumzia kero zilizoko katika majimbo, mimi leo nitajielekeza zaidi katika kero na maeneo ambayo naomba Waziri asaidie kuboresha katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka huu niliuliza swali kuhusu kukauka kwa chanzo cha maji katika Mji wa Lushoto ambacho kukauka huko kulisababishwa na miti inayoitwa mikaratusi. Mikaratusi kwa jibu la Waziri ni kwamba haipaswi kupigwa marufuku lakini ziko aina nyingi za mikaratusi ambazo bila kuzijua nyingi ya hizo zinanyonya maji. Maeneo mengi yamekauka maji kutokana na miti hii ya mikaratusi. Sasa kwa sababu wananchi wetu hawajui aina ipi hainyonyi maji, miti hii imeleta uharibifu mkubwa sana katika nchi yetu na hasa katika Milima ya Usambara hasa Lushoto. Katika chanzo cha maji na Waziri aliniahidi na bahati nzuri nimemwandikia kwamba miti hii inaitwa mikaratusi ing'olewe katika chanzo cha Kwembago vinginevyo Mji wa Lushoto tutakosa maji. Chanzo kingine kinachoitwa Kibohelo nacho miti hii imeanza kumea kule kwa sababu miti hii iliwekwa katika mpaka, sasa unapoanguka mti au moto ukiingia kwa bahati mbaya miti hii ikishashika moto basi inaota kiajabu sana. Kwa hiyo, naomba hatua za tahadhari na za haraka zichukuliwe kuitoa miti hii katika Hifadhi ya Msitu wa Magamba ili isilete madhara makubwa katika eneo hili. Waziri aliahidi lakini nimeliona niweke katika *Hansard* kwa sababu wananchi sasa hivi wanaangalia angalia Mbunge amefanya nini wasikie na hili nimelitamka.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ni kero katika eneo langu ni eneo la uendelezaji na usimamizi wa mashamba ya miti. Lushoto kama inavyoeleweka ni eneo ambalo halina misitu mingi. Ni eneo ambalo tangu wakati wa Mkoloni misitu mingi ilikuwa ni ya kupandwa. Sasa kwa bahati nzuri misitu mingi katika eneo hili ilikwishakomaa na ikavunwa. Lakini uvunaji haulingani na upandaji. Yako maeneo ambayo yamevunwa lakini mpaka leo hayajapandwa. Kwa mfano, kuna eneo la Ng'ambe kulikuwa na msitu kule ambao ulikuwa ni wa Serikali umevunwa haujapandwa. Kuna msitu wa Mazumbai umevunwa haujapandwa. Sasa hivi ukifika pale ni peupe na unaelewa kule ni milimani mvua hazisimami kwa sababu hakuna miti. Kwa hiyo, mazingira yanachafuka, mwenendo wa mvua haujulikani, matokeo yake ni hayo.

Kwa hiyo, namwomba Waziri ajitahidi sana, upandaji wa miti ulingane na uvunaji wa miti hasa katika Jimbo langu na Wilaya ya Lushoto kwa ujumla. Hili ni eneo la hatari na naomba sana kwa sababu miti imevunwa, imepandwa miaka 30 iliyopita, imevunwa katika miaka hii 10 iliyopita lakini ni eneo dogo mpaka sasa hivi limepandwa miti. Naomba hili lipewe mkazo wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa nizungumzie ni usimamizi wa raslimali zetu hasa raslimali misitu. Wilaya ya Lushoto ina tatizo kubwa la uhaba wa ardhi na kutokana na hilo maeneo mengi ni hifadhi za Taifa. Ni misitu ambayo inahifadhiwa na inalindwa na Serikali. Sasa linalotokea ulinzi katika maeneo haya ni hafifu sana matokeo yake watu wanavijiji na wananchi kwa ujumla wanaingia katika maeneo haya. Wanaiba mbao, wanaangusha miti na miti hii mingine ni mti ambayo ni adimu. Ni miti ambayo kwa kweli ina kivutio kwa watalii kwa sababu haipatikani katika maeneo mengi. Ikikatwa ina maana kwa kweli tunaondokana na historia ya aina ya miti hiyo.

Mheshimiwa Spika, pale Mjini Lushoto kuna miti ambayo imepandwa na mingine ilikuwepo panaitwa *Civil Culture.* Kale ka msitu pengine kamebaki na ile misitu ni miti

ya asili. Lakini miti mingi katika hifadhi imekatwa. Kwa hiyo, namwomba Waziri azidishe na hili sitalichelea kusema wengi wanaotuhumiwa kuhusika na wizi wa mbao ni wafanyakazi wenyewe maana wanawaruhusu watu wanaingia katika maeneo haya, wanaiba mbao wakiona. Siamini kabisa kwamba watu hawa hawajulikani, watu wanajulikana, wanatajirika wakionekana. Kila mtu anajua kabisa kwamba ni kutokana na misitu. Sisi katika ngazi ya Wilaya tumejitahidi. Mkuu wa Wilaya na sisi viongozi kulikuwa na kizuizi pale Soni ili mbao zisitoke, kwa bahati mbaya kutokana na utaratibu wa kuondoa vizuia kizuia kile kimeondolewa. Sasa wizi wa mbao kule milimani nina uhakika baada ya miaka 15 au 20 misitu hiyo itakwenda na kule kutakuwa jangwa tutakwenda kupata wapi maji. Nina uhakika misitu au milima ya Usambara ndiyo inayopeleka maji katika bonde la Mto Pangani. Kinyume chake ni kwamba hata Hale itakosa maji. Matatizo yake yameanza kujitokeza.

Hivi leo maji hayajai vizuri katika Mto Pangani. Utakuta kwamba katika eneo la Hale ambako ndipo kuliko na chanzo cha umeme wa Hale maji ni machache na maji hayaongezeki pamoja na kupungua kwa mvua lakini ukweli ni kwamba ni kutokana na uharibifu wa mazingira ambao umefanyika katika milima ya Usambara. Sasa kwa sababu Wizara yake inasimamia hili hasa la misitu, mimi namwomba Waziri atusaidie na kwa kweli ahimize watendaji na watendaji hawa wasikae katika maeneo haya kwa muda mrefu, mtu akishajukuu leo anamkuta baba mkwe ndio amekutwa na mbao, ufanye nini. Kibinadamu basi unaanza kuitoroka toroka kesi, mzee hebu ngoja tuangalie mwishowe mbao zinaozea hapo hapo, kesi ya baba mkwe imepotea na Taifa limepata hasara. Kwa hiyo, namwomba sana Waziri kwa kuzuia ni vizuri wafanyakazi wasikae katika maeneo yale kwa muda mrefu ili kuepuka uzoefu na kuepuka uenyeji katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningeomba nichangie na kama nilivyosema nitajielekeza zaidi katika maeneo ya jimbo langu, nitazungumzia utalii. Hivi leo ukifika Lushoto utaamini kabisa kwamba utalii umekomaa, hatukosi pale watalii kila wiki. Watalii 50, 60, 90 na tumejitahidi hata kufungua ofisi ya kuvutia watalii pale. Kuna *The Friends of Usambara,* lakini hawa hawajapata msaada wa kutosha. Mimi naamini tukiwapa msaada wa kutosha kwa historia Lushoto ndiyo yalikuwa Makao Makuu ya Wajerumani na kule ziko kumbukumbu nyingi za Wajerumani kwa hiyo, utakuta wanakuja wengi na hii *cultural tourism* ambayo imezungumzwa kwa kule wana mambo mengi historia za kule kwa kweli napenda kuwahakikishia kwamba mara nyingine hata sisi wenyewe hatuijui historia kule kuliko Wajerumani. Kumbukumbu zilizoko Ujerumani kutoka Milima ya Usambara ni nyingi zaidi kuliko tulizonazo hapa nchini. Kwa hiyo, Wajerumani wengi wanakuja kwa kusoma kumbukumbu kule.

Mimi ni juzi tu ndio nimejua kwamba kulikuwepo na Gavana wa Kizungu na majina jina la Lushoto halikuwa jina ambalo lilikuwepo, lilikuwa jina ambalo lilitolewa na Mkuu wa Wilaya wa kwanza wa Kijerumani ambaye alikuwa Lushoto. Sasa jina hili kwa kule nyumbani kuliita ndiyo tukaita Lushoto. Lakini yenyewe na nitakuletea maandishi yao yapo na majina ya Wakuu wa Wilaya waliokuwepo. Kwa hiyo, kumbukumbu hizi Wajerumani wanapokuwepo kule wanapenda kutembelea kuja huku sasa wanahitaji nini. Kwanza wanahitaji miundombinu ambayo ni mizuri. Nashukuru Serikali imejitahidi sana. Miundombinu kutoka Mombo mpaka Lushoto ni lami. Sasa

hivi tunaendelea nafikiri tutafika Magamba. Lakini kwa sababu ya hali mbaya ya maeneo yale ya milima kwa kweli kwa barabara zinazokwenda katika maeneo ambayo yanapendwa na watalii hii ni vizuri Wizara ikazitambua barabara hizi zenye maeneo ya historia ili zifike kule hasa wakati kama ni masika. Kwa sababu inapokuwa kiangazi kwa wenzetu kule sisi kwetu huku ni masika ndio wanapenda kuja huku. Kwa hiyo, kwa kusisitiza hili limechangiwa na Wabunge wengine naomba sana tujitahidi ili tuhakikishe kwamba miundombinu na kuitangaza Lushoto. Kutangaza milima ya Usambara na milima mingine na maeneo mengine ifanyike.

Baada ya kusema hivyo mimi napenda kurudia sina mengi ya kuzungumza kwa sababu utendaji ni mzuri na kwa kweli sioni sababu nizungumze sana. Tunapenda kuipongeza Wizara na wote ambao wamefanya kazi nzuri. Mnaturahisishia Wabunge kazi, inatuwia sisi hatuna ya kuzungumza, tunafurahi utendaji ukiwa hivyo. Naomba kuunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa maoni machache katika Wizara yetu hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nami niungane na Waheshimiwa wenzangu kutoa rambirambi kwa Waheshimiwa waliotutoka wote na bahati nzuri nilikuwa nimeshachangia na pia rambirambi kwa jirani yangu hapa Mheshimiwa Salama Khamis Islam, kwa kufiwa na mama yake mzazi *inshallah* Mwenyezi Mungu ampe subira kwa kuwaweka wote mahali pema peponi waliotutangulia. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie fursa hii kwanza na mimi kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya hasa ukiangalia jinsi ya utendaji kwa kushirikiana na watendaji wake Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Mameneja wa Idara zake na wafanyakazi wote wa Wizara hii katika Taasisi mbalimbali zilizokuwemo jinsi inavyokwenda na hata kuimarisha na kuwa chachu ya kuweza kupata mapato makubwa kabisa katika nchi hii kupitia Idara zake Uvuvi, Utalii na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze sana wote na namwombea kila la kheri Mheshimiwa Waziri, Mwenyezi Mungu ambariki amuepushe na kila shari za hapa duniani na ahera.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo nilikuwa nataka kulizungumzia ni suala la utalii hasa katika Kisiwa chetu cha Mafia. Mafia sasa hivi ni eneo zuri kabisa ambalo limo katika sehemu kubwa inayoleta mapato kupitia utalii. Lakini ukiangalia kitu kinachotuadhibu kule kama kawaida ni miundombinu. Miundombinu hali yake sio mizuri, ni mibaya sana. Bila ya kupoteza wakati na kwa kuwa tulishalizungumza katika Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, lakini nilikuwa namwomba tu Mheshimiwa Waziri ajaribu kama Wizara yake inavyotoa michango katika kupeleka huduma mbalimbali kwa kushirikiana ama na Wizara ya Ujenzi au Wizara ya Mawasiliano na kadhalika basi ajaribu naye pia kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano kupitia *TIA* basi waangalie juu ya uwezekano wa kutoa mchango kupitia Wizara yake katika uwanja wetu wa ndege

wa Wilaya ya Mafia kama ilivyofanyika katika maeneo ya Makuyuni kwenda katika *gate* la Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, Wizara yake kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi imeweza kufanikisha barabara ile kuwa nzuri sana, naamini na yeye akiwa na uwezo huo kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi nafikiria kwamba uwanja wetu utaboreka kwa sababu Serikali imetoa shilingi milioni 700 basi na wao wakihangaika wakitoa chochote ikiwa shilingi milioni 300, 500 ikifikia bilioni moja basi japo mita 700 mpaka kilomita moja zinaweza zikatengenezwa na uwanja wetu ukaboreka na nauli ikapungua na watalii ambao pengine wenzao wana ndege zao wakaweza kufika kwa urahisi katika Wilaya yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa uchache ni huo upande wa utalii. Naingia kwenye suala la uvuvi. Mafia asilimia 70 ya wakazi wake ni wavuvi. Tunayo hifadhi ya bahari ambayo inasaidia japokuwa kwa upande mwingine inakuwa kero kwa wananchi, lakini kwa kupitia tu baadhi ya wanasiasa ndio wanaokwenda kuvuruga kule lakini naamini sasa hivi wananchi wanaelewa na hali ya Kisiwa cha Jibondo imetulia na tunakwenda nao vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kuna mfuko huu unaitwa *Japan Social Development Fund.* Huu mfuko nasikia kwa bahati mbaya sijaingia ndani katika kuuchambua lakini umeleta fedha nyingi sana katika Wilaya yetu ya Mafia pamoja na Wilaya za Rufiji na Kilwa. Sasa nilikuwa nataka nimwulize Mheshimiwa Waziri kwamba vipi hizi fedha zipo na kama zipo lini zitakuja Mafia, Kilwa na Rufiji ili ziweze kuwasaidia wavuvi na wananchi wanaokaa kandokando wenye kujishughulisha na masuala ya uvuvi?

Lakini pia kuna huu mradi wa *MASEMU* nao nilitaka nifahamu kwamba Wizara inaufahamu vipi kwa kuingia katika maeneo yetu ya Rufiji, Mafia na Kilwa? Ukiangalia kuna mradi mwingine tena wa *Siskep* ni matarajio gani ambayo wananchi wa Mafia, Rufiji na Kilwa wayategemee kupitia miradi hii? Nilikuwa naomba tu baadaye Mheshimiwa Waziri anifahamishe ili wananchi wa maeneo haya haswa wa Kisiwa cha Mafia waelewe Serikali imejiandaa vipi katika kuboresha hali za wavuvi na wananchi katika kuondoa umaskini na kuwaendeleza katika maeneo hayo niliyoyataja kwa maana ya Mafia, Kilwa na Rufiji. Hotuba imenimaliza kwa sababu imekwenda *in deep* na maendeleo yataonekana lakini nikiyapata hayo basi naamini mambo yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Spika, suala lingine kuna meli za uvuvi ambazo zinavua nje ya maeneo yetu ya Wilaya ya Mafia na bahati nzuri Serikali imeliona hilo na imeanza kufuatilia, imeweza kukamata baadhi ya meli na tumepata ushuru mbalimbali. Lakini kuna meli ambazo zinavua na zimesajiliwa ama kupewa leseni ndani ya nchi yetu. Meli hizi zina wafanyakazi, hawa wafanyakazi wana umoja wao. Sasa mimi nitazungumzia wafanyakazi wa Meli za Uvuvi Tanzania ambao wana chama chao kinachoitwa *WAMEUTA.* Hakika hawa wafanyakazi ndio wanaosaidia Idara ya Uvuvi katika kukusanya hao samaki, kamba au mazao mengine ya baharini ambao ndio wanaoleta Pato la Taifa katika nchi yetu kwa kupitia Idara ya Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, lakini hawa wafanyakazi wanalalamika kuwa uongozi wao ni mbaya, Mwenyekiti, Katibu na Mweka Hazina wao. Leo ukiangalia Katiba hii ambayo ninayo *copy* wanasema kila mwaka wanachama watapaswa kukaa mara moja ili kuangalia hali ya mapato na matumizi katika chama chao na kuweza kupanga mikakati mizuri ya maendeleo ya chama chao. Lakini wafanyakazi ambao baadhi yao wamekuja hapa Bungeni na ninao kwenye *gallery* ile kwa sababu ni wananchi wangu wa Mafia, vijana wengi wanatoka Mafia wanakuja kuvua lakini wanadhulumiwa na wao wanakatwa kila wanapofanya kazi kwenye meli asilimia 7 ya mshahara wao kila mwezi. Lakini wanapokaa kutaka kuuliza nini kinachoendelea basi wale wakubwa wao, Mwenyekiti, Katibu huwa wanawazungusha zungusha. Sasa nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri awasaidie kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kwa sababu wamejitahidi kwenda mpaka kutaka kumwona Mheshimwa Profesa Juma Kapuya, wameshindwa. Sasa tunaomba Mheshimiwa Waziri Mama yangu Zakia Meghji, uwasaidie hawa wananchi waweze kupata maslahi yao ili na wao waboreke. Kwa sababu hawa kama wanataka kufanya hujuma wanaweza wakafanya hujuma. Kuna taarifa ambazo sina ushahidi nazo inawezekana hata ule mzigo uliotumwa nje wa Kampuni ya *TANPESKA* nina wasi wasi kwamba hawa wafanyakazi walifanya hujuma ya kutia uchafu na baadaye ule mzigo ulirejeshwa. Sasa wanasema tunadharauliwa, hatusikilizwi. Japokuwa lile tendo wanalolifanya hawajielewi nani wanamkomoa maskini. Sasa nilikuwa naomba tu ili kuondoa migogoro hii basi hawa watu waweze kusaidiwa na waweze kufanya mkutano wajue haki zao.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa leo sina mengi ni hayo tu. Kikubwa ni kuwapongeza wote na namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuniteua mimi kuwa mmoja wa wajumbe wa Bodi ya Hifadhi ya Bahari na naomba nishukuru kwa heshima aliyonipa hiyo. Tumeweza kushirikiana na wajumbe wenzangu chini ya Mwenyekiti wetu Profesa Nuhu na naomba nimshukuru kwa mawazo yake na naamini *inshallah* tutarejea na tutaendelea kuwa washauri kupitia maeneo haya ya Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, mchango wangu unalenga kwenye Hifadhi ya Pori la Akiba la Lukwika, Lumesule lililoko ndani ya Jimbo na Nanyumbu, Wilayani Masasi. Wananchi ambao maeneo yao yalichukuliwa na Hifadhi hiyo kwa nyakati mbalimbali baadhi yao hawajalipwa fidia ya mazao yao pamoja na uongozi wa Hifadhi kudai kuwa wananchi wote waliostahili kulipwa fidia wamelipwa na nyaraka mbalimbali kuonyeshwa, bado uongozi wa vijiji husika na wananchi wake wanadai kuwa bado fidia hiyo hajalipwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano mmojawapo wa viongozi wa Wilaya ya Masasi Mheshimiwa Waziri alijionea wazi jinsi ulipaji wa fidia hiyo ulivyokiuka

taratibu za kulipia fidia. Ilielezwa kuwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya haikuhusishwa. Mhasibu au mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya hakuhusishwa.

Naomba Serikali kufanya uchunguzi juu ya suala hili ili kurudisha imani ya wananchi kwa Serikali yao. Kwa vile wananchi bado wanalalamika ni vizuri jambo hili likachunguzwa kwa makini kubaini kasoro zilizopo na kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine la Hifadhi ya Pori la Akiba la Lukwika, Lumesule ni kubadilika mpaka mara kwa mara bila ya utaratibu unaokubalika. Wananchi wa maeneo yanayozunguka hifadhi wanadai kuwa mipaka ya Hifadhi hiyo imekuwa inabadilishwa mara kwa mara kuelekea pande wa vijiji. Kwa hiyo, wananchi ambao maeneo yao huingizwa ndani ya mipaka mipya ya hifadhi hawalipwi fidia kwa maeneo hayo mapya. Naomba Serikali kuhakikisha kuwa uongozi wa hifadhi unafuata taratibu zilizokubaliwa wakati wa kupanua mipaka ya hifadhi ya Pori la Akiba la Lukwika, Lumesule. Taratibu hizo ni pamoja na kushirikisha uongozi wa vijiji na wananchi wenyewe na fidia kamili kulipwa ya mazao.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaoishi kuzunguka Hifadhi ya Pori la Lukwika, Lumesule hukabiliwa na kero kubwa la wanyama kuharibu mazao yao mashambani. Athari hizi huwapata wananchi wanaoishi katika Kata za Napacho, Chipuputa, Nanyumbu na Masuguru. Kwa kuwa eneo ambalo wanyama hao hushambulia ni kubwa sana kunahitajika Askari wa kutosha kuwadhibiti. Kwa hivi sasa idadi ya Askari hao ni ndogo sana hivyo kushindwa kupatikana katika eneo lote wanapotakiwa. Serikali ingehakikisha kuwepo Askari wa kutosha katika kila Kata badala ya Askari hao kuwepo Makao Makuu ya Wilaya Masasi ambako ni mbali mno na eneo la Hifadhi.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. HASSY H.B. KITINE:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kufahamu na kupata maelezo juu ya mipango ya *TANAPA* kuendeleza Hifadhi ya Taifa ya Kitulo, Pori la Akiba la Mpanga, Kipengere lililoko kati yaWilaya ya Makete na Njombe.

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kuunga mkono hoja ya Waziri wa Maliasili na Utalii kwa asilimia mia kwa moja.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri afikirie kukikuza Chuo cha Maliasili cha Likuyu – Sekamaganga ili kuhusu masomo ya kuwafunza Wapagazi *(Porters)* wa kuwasindikiza watalii wa Mlima Kilimanjaro, Meru na kwingineko, ikijumuisha pia wale *Guides* watoe maelekezo kwa watalii mfano wale wa Ujiji, Kwihara, Kaole, Bagamoyo, Sanane na Makaburi ya Mashujaa wa Majimaji pale Jumba la Makumbusho la Songea, Mjini Ruvuma. Tayari Chuo hiki cha Likuyu ni cha Kimataifa. Baadhi ya wanafunzi wake sio tu wanatoka Wilayani Namtumbo na kwingineko Tanzania bali wametoka mbali kama Zimbabwe na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, napendekeza pale Chuoni wanafunzi wanafunzwe ufugaji wa nyuki, utengenezaji mishumaa, kusindika asali kwenye chupa na utengenezaji wa mizinga ya mbao ili wahitimu wa mafunzo warudipo wawe na ujuzi huo na hivyo kuwafanya wasipende kuwasha moto kwenye misitu yenye mizinga yenye asali

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii kwa mabadiliko makubwa aliyoyafanya katika Wizara hii na hususan Sekta ya Utalii ambayo imekuwa ikipanda mwaka hadi mwaka. Nashauri ili kukabiliana na tatizo la malazi kwa watalii wawapo mbugani katika kipindi cha *peak period* ambapo hoteli zilizopo hufurika ni vyema makampuni binafsi yakahamasishwa na kupewa *tender* ya kujenga makambi ya *tents* ambazo ni *modern* ndani ya mbuga ili watalii wayatumie kwa kulipa na hii itaongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, ni kweli shughuli za uvuvi ndani ya Ziwa Victoria zimeongeza ajira na mapato kwa wavuvi wa hasa baada ya kufunguliwa viwanda vya samaki katika Jiji la Mwanza na Bukoba (Kemondo). Hata hivyo, mafanikio hayo yameathirika upande wa pili na hasa afya na lishe ya wananchi wanyonge ambapo bei ya samaki hivi sasa hawaimudu. Wavuvi wengi wamekuwa wakiuza samaki viwandani ambako bei ni nzuri na wananchi kuambulia vichwa vya samaki vinavyochambuliwa baada ya kukokotoa minofu.

Mheshimiwa Spika, vile vile wananchi wamekuwa wakikumbana na dhahama kubwa pindi wakikutwa hata na samaki mmoja au wawili wadogo wa mboga, pindi wakikutana na mabwana uvuvi au askari katika maeneo ya Nyamukazi, Ntoro, Kifungu yaliyoko kando kando mwa Ziwa Victoria /Bukoba Mjini wamekuwa wakivamiwa na vyombo vyao na mali zao kuharibiwa.

Katika hili namwomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi wa tukio lililotokea Ntoro katika Kata ya Kahororo/Bukoba Mjini la askari kuvamia eneo hilo, kuwadhalilisha akinamama, kupiga watu, kuharibu mali kiasi cha kupafanya mahali pale hivi sasa pasikalike. Je, walitumwa na Serikali kufanya uharibifu huo? Je, wananchi wachukue hatua gani za kudai fidia ya mali yao iliyoharibiwa? Naomba Mheshimiwa Waziri atoe maelekezo na utaratibu ambao utawezesha kukidhi kwa mambo yote mawili:-

(a) Minofu ipatikane kwa ajili ya mauzo ya nje ili wazungu wapate lishe bora lakini na pia wananchi nao katika hali zao wapate lishe ya samaki kwa kuwekewa utaratibu wa kuvua na kupata kitoweo cha samaki.

(b) Utaratibu wa kisheria na kanuni zilizopo za uvuvi katika *Lake Victoria* kwa kiasi kikubwa zinajielekeza kuwalinda walaji wa Ulaya. Hivyo taratibu na sheria hizo zirejewe na kuangalia namna ya kuwasaidia hata walaji wa humu ndani na hasa wale wa kipato cha chini huko vijijini.

Mheshimiwa Spika, mambo hayo yanaweza kuwezekana endapo yafuatayo yatafanyika kati ya mengi yanayoweza kufanyika:-

Moja, uvuvi katika Ziwa Victoria ufanyike kwa misimu na ikubaliwe na nchi zote tatu za Afrika Mashariki. Kuwepo msimu wa kuvua na kuuza viwandani na kipindi kingine wavue lakini viwanda viwe vimefungwa.

Pili, kuwepo vibali maalum vya kutolewa na Halmashauri zetu kwa kushirikiana na Wizara kwa ajili ya wavuvi wadogo kabisa wanaovua kwa ajili ya matumizi ya kawaida na sio viwanda *(domestic consumption).*

Mheshimiwa Spika, namtakia kazi njema Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yake. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Moja, maslahi na vitendea kazi kwa watumishi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi ya watumishi na kuwapatia vitendea kazi vya kisasa hasa wale wanaofanya kazi katika mbuga za wanyama ili waweze kupambana na majangili wanaohujumu uchumi wa nchi yetu kwa kuua wanyama ovyo.

Pili, barabara zote zinazoingia kwenye mbuga za wanyama zikarabatiwa ili kuvutia watalii wengi ambao wanaingiza fedha katika nchi yetu.

Tatu, watumishi na Wizara ya Maliasili na Utalii walioko Wilayani hapa nchini wapatiwe vitendea kazi na kupewa mafunzo zaidi ili kuboresha utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, nne, kwa kuwa mradi wa Hifadhi Ardhi Dodoma *(HADO)* ulikuwa unafadhiliwa na wafadhili wa nje. Je, ni nani anayefadhili mradi huo kwa sasa, je, Serikali inachangia fedha kiasi gani kusaidia mradi huo na je watumishi kwa sasa wanaowajibika kwa nani na ulipaji wa mafao yao?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. SHAMIM P. KHAN:** Mheshimiwa Spika, moja, nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Pili, nampongeza Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa kazi nzuri anayofanya kuliendeleza gurudumu la Maliasili na Utalii. Namshukuru sana Katibu Mkuu, Ndugu Salmon Odunga, kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri, akisaidiana na wataalam wengine.

Mheshimiwa Spika, tatu, miaka michache iliyopita Tanzania ilikuwa haifahamiki ulimwenguni . *Tasmania* ilikuwa inafahamika sana badala ya Tanzania. Lakini leo hii Tanzania ipo katika ramani ya ulimwengu. Hata ile dhana potofu kwamba Mlima Kilimanjaro upo Kenya imefutika. Shukrani na pongezi kwa wote kwa kazi nzuri kufanya marekebisho.

Nne, kikwazo kikubwa ni lugha. Kuna haja ya kuanzisha *centre* kwa wahudumu wetu pamoja na wengine wote wanaohudumia watalii kama madereva, *guides, game warders* kujifunza lugha za wenzetu kama Kiingereza, Kifaransa na kadhalika ili waweze kuwasiliana na hao watalii angalau yale maneno machache ya kila siku.

Tano, nitashukuru sana kupata taarifa kama ikiwezekana ya vyura vya Kihansi. Je, Wizara inafanya nini kufaidika na eneo hilo ili tupate watalii wengi? Nini *progress report* ya wale waliochukuliwa kwenda nje ya nchi?

Mheshimiwa Spika, sina mengi Mungu awabariki, Mheshimiwa Zakia Meghji, nakuombea kila la kheri katika uchaguzi ujao.

**MHE. TEMBE K. NYABURI:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba niwaombe Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu kutatua tatizo la mpaka wa Hifadhi ya Serengeti na vijiji vinavyopakana na Hifadhi hiyo Wilayani Bunda.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Wanyamapori na wataalam wa Wizara hii si mara ya kwanza kusikia kilio cha wananchi wa vijiji vya Bunda mpakani na Hifadhi ya Serengeti wakidai kurudishiwa maeneo ya zamani yaliyomegwa na kuwa Hifadhi miaka 1997/1998 bila ya kushirikisha wananchi wa vijiji husika. Ukiangalia mihutasari ya Serikali ya vijiji husika usogezaji wa Hifadhi hadi Mto Rubana badala ya tuta la zamani la Kawanga haukuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu wakati Idara ya Wanyamapori inaandaa mpango wa kufanya Mto Rubana ndio uwe mpaka Idara iliandaa warsha ya kudokeza azma yake. Katika warsha hiyo kila kijiji walichukuliwa wajumbe kati ya wawili au watatu tu na wao katika mapendekezo yao walipendekeza kabla ya kutekeleza mpango huo ni vema Idara ingefanya mikutano ya hadhara katika vijiji husika jambo ambalo halikufanyika na Idara ikafanya ujanja kwa kutumia mapendekezo ya wachache wale na kutangaza mpaka mpya.

Mheshimiwa Spika, hivyo mpaka mpya ulitangazwa bila wananchi kuwa na taarifa yoyote. Suala hili ni tatizo kubwa na likipuuzwa linaweza kuja kuzua tatizo kubwa huenda kuliko lile la mapigano ya Kilosa-Morogoro.

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe na baadhi ya wafugaji tumefika Wizarani, kufuatilia suala hili na tukaongea na wahusika wale wale walioshiriki kupindisha

utaratibu wa suala hili. Naomba Wizara ishughulikie tatizo hili kwa upekee kabisa bila kupuuza. Ahsante.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kupata nafasi hii kwa minajili ya kuchangia hoja hii ya Maliasili na Utalii.

Pili, nampongeza sana tena maridhawa kabisa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa bidii zake kazini, kwa ufuatiliaji makini, kwa uadilifu murua sana, kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais kazi vizuri na kwa kutoa ushirikiano mzuri kwa Wabunge. Namtakia uchaguzi mwema, Mungu ampitishe.

Tatu, nawapongeza wafuatao kwa kazi ya kukamilisha Makadirio ya Wizara hii, Katibu Mkuu, Makamishna na Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na wasaidizi wengine wote. Pia Mwenyekiti wa Bodi ya *TANAPA* na wajumbe wake kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini, naomba kuwasilisha shukrani kwa Serikali kupitia Waziri na Bodi ya Hifadhi ya Wanyamapori Nchini *(TANAPA)* kwa kazi nzuri zifuatazo:-

(1) Wananchi na *TANAPA* kwa kujenga vyumba vya madarasa katika shule za msingi za (i) Chubi na (ii) Itaswi.
(2) Kukubali kushirikiana na wananchi wa kijiji cha Idindiri kwa kujenga zahahati kijijini hapo 2005/2006.
(3) *TANAPA* kujenga ukumbi mkubwa kwenye Sekondari ya Aman Abeid Karume Tarafani Pahi shukrani sana.
(4) *TANAPA* kujenga nyumba ya Mkuu wa shule hiyo imekamilika.
(5) *TANAPA* kujenga hosteli mpya, ambayo itachukua wanafunzi wasiopungua 90 shuleni hapo.
(6) *TANAPA* wapo tayari kwa miradi mingine iwapo wananchi wakiomba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sifa hizo naomba Mheshimiwa Waziri atafakari na kutoa majibu muafaka kwa hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, hoja namba moja ni kucheleweshwa kwa ujenzi wa barabara ya Chubi-Itaswi-Kisaki kupitia *TANAPA.*

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulikubaliwa tangu mwaka 2000/2001, hadi leo bado utekelezaji kwa nini? Serikali na *TANAPA* walishauri kukwepesha barabara isipite eneo fulani ili isiathiri bwawa Kisaki na pia Hifadhi na wataalam walizingatia ushauri huo, wakafanya makisio mpya, je, sasa Serikali inawambia nini wananchi hao? Kazi itaanaza lini? Mvua zikinyesha ni kisiwani huko? Halmashauri inasemaje na *TANAPA* nao wamejizatiti vipi?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ni mtu makini sana kwa nini hilo linampiga chenga? Akumbuke ahadi yake ya kufikia eneo hilo mwaka wa nne sasa ataitimiza lini?

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, kule Kondoa kuna Hifadhi ya Pori ya Swagaswaga. Pori hili lipo karibu sana Mji wa Kondoa, linapakana na Kijiji cha Mongoloma, wakati wakiweka mipaka tayari kijiji hicho kilikuwepo. Kijiji kilianza na ni kijiji kwa mujibu wa operesheni vijiji ya mwaka 1974/1975.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya sasa yameingia ndani sana ya kijiji hicho, watu wa kijiji hicho wahamishiwe wapi? Watafidiwa na nani? Kwa nini mpaka huo usisogezwe nyuma kwa faida ya binadamu na hilo pori ni faida ya hao watu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atume Tume ikaone na kuzingatia maisha ya watu yaani kilimo chao, ufugaji wao, ujenzi , uvunaji kuni na kadhalika. Watu ndio kipaumbele, wanyama baadaye. Fanya hima kuhusu hili! Tukumbuke kipaumbele ni watu kwanza.

**MHE. OMAR MJAKA ALI :** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaitumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja Katibu Mkuu, watendaji na wataalamu wote wa Wizara hii kwa hotuba yake hii nzuri yenye mafanikio makubwa ya kimaendeleo ya kiuchumi kwa Taifa letu hili la Tanzania na kwa wananchi wote wa Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ni nzuri na ninaiunga mkono kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri imeelezea juu ya suala zima la ulinzi wa rasilimali ambapo tunaelezwa kuwa doria kuhusu uvuvi haramu na biashara ya magendo zinazoendeshwa baharini, Ziwa Victoria pamoja na Ziwa Tanganyika, ambapo watuhumiwa na zana zao haramu walikamatwa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana kazi hii nzuri ambayo imefanywa na Wizara hii kuzuia uhalifu katika maziwa na Bahari zetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, sasa sijui wahalifu hao hapo nyuma walipewa elimu inayowajulisha kuwa kufanya vitendo hivyo ni makosa ya jinai au kuna utaratibu gani unaowawezesha wahusika hao wa uhalifu kutambua kuwa uhalifu wanaoufanya ni makosa ambapo yanaweza yakawaingiza katika matatizo ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, je, adhabu sahihi kwa wahalifu hao ni ipi, kati ya vifungo, fani au kuharibiwa vifaa vyao?

Mheshimiwa Spika, vile vile katika sehemu zetu za Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika ni maeneo ambayo hufanyika uhalifu mkubwa ambao unafanywa na wahalifu kutoka nchi za jirani kama vile *DRC,* Burundi, Rwanda na kadhalika. Je, wahalifu hao ambao ni hatari sana kwa maisha na maslahi ya wananchi wa nchi yetu ya Tanzania wanaoishi na kufanya shughuli zao katika Maziwa haya, wanachukuliwa hatua gani kwao wao wenyewe na kwa nchi zao.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu hivi sasa imo katika vita vikubwa vya kupambana na umaskini wa wananchi na kwa faida ya nchi yetu kwa ujumla, jambo ambalo kwa kweli wahalifu wa nchi hizi za jirani wanaweza kukwamisha mipango hii iliyowekwa na Serikali yetu kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu wa nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii inatueleza kuwa Wizara ilitoa elimu kuhusu uvuvi bora, uhifadhi na matumizi endelevu ya misitu na wanyamapori, umuhimu wa maeneo ya kihistoria na uhifadhi kwa kurusha hewani vipindi 82 vya radio na 14 vya televisheni.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara kwa kutoa elimu hiyo kwa umma na kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza, je, elimu hii imewafikia walengwa kama ilivyokusudiwa, kama haikuwafikia walengwa kuna utaratibu gani mwingine ambao unaweza kutumiwa ili elimu hii iweze kuwafikia walengwa wote waliokusudiwa na kwa mafanikio yaliyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, nauliza hivi kwa kuwa na hofu ya kuona kuwa pengine kuna baadhi ya maeneo ya nchi yetu redio yetu haipatikani au kama inapatikana muda wa kipindi kinachotolewa unawawezesha wananchi hao kuwa wapo majumbani au katika maeneo yao yanawawezesha kukisikia kipindi hicho na kuhusu vipindi vinavyorushwa katika televisheni je, vinawafikia wananchi walioko vijijini?

Mheshimiwa Spika, ninauliza hili kutokana na kuwa katika nchi yetu bado kuna vijiji vingi sana havijapata huduma za umeme ambao ndiyo msingi muhimu katika matumizi ya televisheni na kadhalika. Sasa utaona kuwa misitu mingi na kadhalika ipo vijijini ambako ndiko kuliko na wananchi wengi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara kuongeza utaratibu mwingine wa kutoa elimu ya aina hii kwa wananchi badala ya kutumia vyombo hivi viwili tu yaani redio na televisheni.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa mpango huu wa elimu pia ungetolewa kupitia mikutano mbalimbali inayoendeshwa katika vijiji vyetu na Halmashauri zetu hapa nchini ambapo watendaji wa vijiji na Halmashauri kwa kushirikiana na wataalam na Maafisa kutoka Wizara hii ya Maliasili na Utalii kutoa elimu hii ambayo inaweza kuleta mafanikio makubwa zaidi na yenye faida kubwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, vile vile nampongeza sana sana Mheshimiwa Waziri na Wizara yake hii ya Maliasili na Utalii kwa kuelezea suala zima linalohusu Utawala Bora ambapo imeelezwa katika ukurasa wa 46 wa hotuba yake Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, hotuba yake Mheshimiwa Waziri inatueleza kuwa Wizara imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa viongozi na watumishi ikiwa ni hatua ya kujenga uwezo wao katika utendaji unaozingatia misingi ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli naipongeza sana hotuba hii na Wizara kwa ujumla kwa kuweka misingi hii ya uwezo wa viongozi na watendaji wake.

Mheshimiwa Spika, bila ya kuwa na viongozi na watendaji wenye uwezo, huwezi kuleta mafanikio yoyote yale kwa maendeleo ya watu na nchi kwa ujumla. Utawala bora ni msingi wa yote hayo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, hongera sana kwa kazi nzuri ambayo Wizara hii imefanya tangu iongozwe na Mheshimiwa Zakia Meghji, hususan katika fani ya utalii pongezi nyingi. Maoni na mapendekezo ni kuwa ni muhimu itafutwe njia itakayookoa miti asili kutokana na uchomaji wa mkaa kwa wingi mno kiasi kwamba sasa inatisha, uchomaji misitu hovyo/kiholela kila mahali kana kwamba hakuna Serikali za vijiji. Je, hakuna adhabu yoyote ambayo ingeweza kuwawajibisha wahusika na usimamizi (Serikali) na ukataji wa magogo, mimi nashauri kwamba ni bora kwa sasa biashara hiyo isitishwe kwa muda fulani ili miti mingi ikue/iote na Serikali kujipanga upya katika kusimamia shughuli hii.

Mheshimiwa Spika,Wizara ifanye utafiti wa kupata maeneo mengine ambayo ni maeneo muhimu sana kwa utalii kutokana na jiografia yake ilivyo. Naamini yapo maeneo yanayovutia sana utalii lakini bado yanahitaji utambuzi na maandalizi hasa maeneo ya Nyanda za Juu na Kusini mwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, binafsi natoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wote kwa kuiletea Tanzania sifa miongoni mwa Mataifa hususani kwa kunyakua zawadi kubwa na ya kwanza katika Maonyesho (Nje na Ndani – Sabasaba) na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, namtakia Mheshimiwa Waziri kila la kheri katika kuhitimisha hoja ya leo, *God bless you*.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Zakia Meghji, Mbunge na Waziri wa Maliasili na Utalii kwa hotuba yake nzuri na yenye uchambuzi wa kina ambayo ameitoa asubuhi hii. Hotuba hii imeonyesha umahiri wa Mheshimiwa Waziri alionao katika kuendeleza Sekta ya Maliasili na Utalii. Pongezi sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kuhusu ombi la wananchi wa Kijiji cha Mese la kusaidiwa usambazaji wa umeme katika kijiji hicho kupitia *TANAPA,* tunaendelea kukusanya takwimu za kuonyesha

gharama halisi za mradi huo na muda si mrefu tutaziwakilisha kwa Waziri kama alivyoelekeza kwa ajili ya utekelezaji. Nitaendelea kuwahamasisha wananchi wa kijiji husika pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Hai ili iweze kushiriki kikamilifu katika mradi huo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:**Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Zakia Meghji, Mbunge na Waziri wa Maliasili na Utalii kwa hotuba yake nzuri sana, iliyo na maelezo ya wazi na takwimu muhimu. Naunga mkono hoja yake kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumpongeza Bwana Salmon Odunga, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kwa kuongoza timu ya watendaji wa Wizara hiyo na mashirika yake kwa ushirikiano mzuri uliozaa ufanisi na kumwezesha Waziri kuwa na hoja nyepesi humu Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imejitoa kwenye kuendesha biashara na ushuru moja kwa moja, kwa nini isiwezeshe Bodi ya Utalii ili iongoze uwekezaji wa kitalii. Kwa mfano, kumilikishwa kwa niaba ya Serikali maeneo fulani ya utalii fukweni, mbugani, milimani na kadhalika. Halafu bodi *(TTB)* ikatafuta wawekezaji wa kushirikiana nao. Kwa njia hiyo, bodi itatumia thamani ya maeneo hayo kama mchango wake wa kihisa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara hususan Waziri mwenyewe na watumishi wengine akiwamo Katibu Mkuu Ndugu Odunga kwa kazi nzuri iliyofanywa na Wizara hii kwa miaka mitano iliyopita. Pia naipongeza Wizara kwa hatua mbalimbali zilizochukuliwa kulinda mali asili zetu. Kwa mfano, usimamiaji wa uvunaji magogo na kusafirisha magogo hayo nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu ya ushauri. Usimamizi na uendelezaji mashamba ya miti Wilayani Lushoto. Kuna shamba la Mazumbai na Ntambwe katika Jimbo langu la Lushoto. Kwa kipindi kirefu mashamba hayo hayajapandwa. Naomba nipate jibu kwa nini mashamba haya hayapandwi? Ni muhimu sana kwa uboreshaji wa mazingira katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, uondoaji wa miti ya mikaritusi katika chanzo cha maji Kwembago kwa ajili ya mji wa Lushoto. Naomba sana kama ulivyoahidi wakati unajibu swali langu Bungeni kwamba Wizara yako itachukua hatua ya uondoaji miti ya mikaritusi katika eneo hili ambalo lipo katika hifadhi ya misitu magamba. Miti hii ina madhara makubwa katika chanzo hicho cha maji.

Mheshimiwa Spika, ulinzi wa maliasili kwa ujumla. Tunashukuru jitihada za Wizara kuweka ukanda wa milima ya Usambara katika mpango wa uimarishaji utalii. Ni

muhimu kuhimiza ujenzi wa miundombinu. Hoteli na barabara katika maeneo haya ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuandika haya naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wake wote kwa taarifa na kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, ni mfano wa kuigwa wengine kwa kazi nzuri sana, anajituma, msikivu pamoja na kwamba Mkoa wa Mtwara tunamhitaji aboreshe Sekta za Utalii. Hiyo hainifanyi nisiwe mkweli katika kumpongeza, nami namtakia kila la kheri.

Mheshimiwa Spika, mimi nashangaa kwa nini Wizara hii yenye shughuli nzito, tena shughuli zake zinaipatia Taifa Pato kutokana na uzalishaji, isiyo na Naibu Waziri wa kumsaidia kujibu maswali na kadhalika, mwenyewe ajibu maswali, afuatilie wavuna magogo, afuatilie uvuvi haramu Mikoani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ijayo Wizara hii pia iwe na Naibu na Mungu akimjalia kupita Mheshimiwa Waziri abaki katika Wizara hii ili aendeleze kazi zake, maana ameonyesha kuiweza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na *Mtwara Corridor* haiwezekani kustawi kama sekta mbalimbali hazistawishwi pamoja na ukosefu wa miundombinu, wapo wanavikundi waliojitokeza kwenye uvuvi vijana na wanawake ila wanapata matatizo ya nyavu na nyenzo mbalimbali za kuwawezesha kuzalisha samaki kwa wingi vikundi hivyo vipatiwe mikopo.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mtwara una hoteli za watalii, Ruvula na Mikindani, haipati wageni kulingana na matarajio na kwa nini Wizara inaachia hali hiyo Wizara inahitajika kuelewa hilo na kutembelea na itangaze ili wageni wajue Mkoa wafike Mtwara na iwawezeshe wenye hoteli kuwa na kipato.

Mheshimiwa Spika, hali ya Tanzania siyo nzuri ukiangalia baadhi ya Mikoa inaonyesha vipara vipara kutokana na uvunaji wa misitu na jitihada za kurudisha hali nzuri ya kijana, misitu ni ndogo sana kulingana na umuhimu wake, nashauri Wizara iweke mikakati kabambe ya kuwezesha Mikoa inajali ustawishaji wa upandaji wa miti.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache napenda kuunga mkono hoja ya Waziri mia kwa mia.

**MHE. MOHAMED JUMA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utalii unahusisha sehemu za nchi zenye vivutio mbalimbali ni vyema sana utafiti ukafanywa

tena kitu gani zaidi hapa nchini kinaweza kuwa kivutio cha watalii lakini hadi sasa vitu hivyo havijajulikana na hivyo kutangazwa kuwa ni vituo vya utalii.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ambao mimi mwenyewe nimeuona katika safari zetu katika nchi hii tukiwa na shughuli za Kamati ya Miundombinu ni ule Mlima wenye maumbile na mandhari ya ajabu sana. Mlima wenyewe ni ule wa Kitonga katika Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Spika, mimi nilipouona mlima ule kwa kweli niligundua kuwa nao ni kitu kimoja cha miujiza ya Mungu na sidhani kuwa kitu cha aina ile hakiwezi kuwa kivutio cha utalii na sijui kuwa kinapatikana sehemu nyingine ulimwenguni. Ni vyema sehemu ile ikaangaliwa kwa mtazamo huo.

Mheshimiwa Spika, kitu huweza kuwepo lakini thamani yake isijulikane na hivyo kubaki bila tija yoyote kwa wale waliojaaliwa nacho. Naomba Wizara hii iangalie juu ya umuhimu wa mlima ule iandae mazingira bora kwa utalii na uutangaze rasmi mlima ule kama kivutio cha utalii.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kushauri Wizara kwa makusudi izuie ukataji wa miti fulani ya asili kwa faida ya kizazi kijacho. Miti hii ni pamoja na mibuyu, midamba na kadhalika. Baadhi ya mibuyu yenye umri wa miaka zaidi ya 2000 eti inakatwa bila sababu. Miti hii iitwe *National heritage trees* watu wasiruhusiwe kuikata miti hiyo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kujibu baadhi ya hoja zilizoletwa na Waheshimiwa Wabunge kwa kuzungumza na kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nasema baadhi kwa sababu muda nilionao nafikiri nusu saa au saa moja. Lakini saa moja pia haitatosha kabisa kuweza kujibu hoja zote hizi. Kwa maana hiyo hoja kadhaa tutaweza kuzijibu kama kawaida kwa maandishi.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa maandishi na kuzungumza. Naelewa kwamba hoja nyingi ni za kujenga hasa Wizara yetu. Ni hoja ambazo siku zote kwa kweli zinasaidia katika utendaji kazi wa siku za usoni.

Hoja nyingine ni mapendekezo na hoja zingine zinataka kutoa maelezo ili kuweka sawa masuala mbalimbali ili yaweze kueleweka. Lakini labda hoja zingine ni zile ambazo pengine tunaweza kusema kwamba tunasikia kwa wakati huu lakini tutaweza kufuatilia. Kwa mfano, hii hoja ya mwisho ambayo Mheshimiwa Abdulkarim Shah, aliyoieleza ya Mafia tumelisikia hapa na wafanyakazi nasikia wako hapa kwa hiyo,

tutashirikiana na Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, ili kuangalia ni jinsi gani tunaweza kurekebisha jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwataja wafuatao ambao waliozungumza ambao ni Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, ambaye ni Msemaji wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira na Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini ambaye ni Msemaji wa Upinzani Wizara ya Maliasili na Utalii.

Wengine ni Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mbunge wa Kiteto, Mheshimiwa Martha Wejja, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Fatma Said Ali Mchumo, Mbunge wa Mlandege, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi, Mheshimiwa Dr. Ireneus Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki, Mheshimiwa Mwalimu John Singo, Mbunge wa Same Mashariki, Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, Mheshimiwa Hashim Saggaf, Mbunge wa Dodoma Mjini, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mbunge wa Lushoto na Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mbunge wa Mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale ambao walioweza kuchangia kwa maandishi ni wafuatao, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Mbunge wa Namtumbo, Mheshimiwa Samwel Chitalilo, Mbunge wa Buchosa, Mheshimiwa Tembe Kerenge Nyaburi, Mbunge wa Bunda, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mbunge wa Nanyumbu na Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mbunge wa Vitongoji.

Wengine ni Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, Mheshimiwa Shamim Khan, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mbunge wa Mkanyageni, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, Mbunge wa Makete, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega na Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mbunge wa Lushoto.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa wengine waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir, Mbunge wa Mwembe Makumbi, Mheshimiwa Khalid Suru, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge Morogoro Kusini Mashariki, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini, Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib, Mbunge wa Chonga, Mheshimiwa Lydia Tecla Boma, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini. Napenda kusema tunawashukuru sana kwa mchango wao huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumza kama nilivyosema kwamba sitaweza kuzijibu hoja zote japokuwa watendaji wamekaa leo mchana na wengine nafikiri hawajala hata *lunch* kuweza kujibu hoja karibu zote na ziko kwa maandishi. Kwa hivyo, tutaweza kuwaletea mara baada ya hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kwanza kabisa kuzungumzia hoja ambazo zimezungumziwa katika sekta ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, katika sekta hii ya wanyamapori mambo kadhaa yamejitokeza na haya yamezungumzwa kwa upande wa Kamati ile ya Maliasili na Mazingira na pia Msemaji Mkuu wa upande wa Upinzani.

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kwamba *average quota* ambayo ni ya uwindaji inayotumika kwa sababu mara nyingine watu wanasema kwamba uwindaji unafanyika na wanyama wengi wanauawa na kuna matatizo. Lakini niseme kwamba kwa Kampuni zile za uwindaji ambazo zinawinda karibu zote hazifikii asilimia mia moja ya *quota* ambayo inayopewa.

Mheshimiwa Spika, nasema asilimia moja namaanisha kwamba kwa mfano umeambiwa utawinda labda simba 10 au 20 basi hawamalizi simba hao kwa sababu kuna siku kadhaa ambazo unapaswa kuwinda. Kwa mfano, simba anawindwa kwa siku 21 ukimaliza siku ile ya 21 basi baada ya hapo huwezi kuendelea kuwinda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *average quota* ambayo inatumika ni kama asilimia 69 na tunaweza kusema hakuna Kampuni ambayo inafikia asilimia 70.

Mheshimiwa Spika, *TAWIRI* imekuwa inafanya sensa pia ya wanyama, kwamba wanyama wetu kwa kweli wamekuwa wanaongezeka hasa kwa sababu ya ushirikishwaji wa wananchi. Kwa hiyo, upande wa *poaching* umepungua kwa sehemu kubwa, na hii inaonekana wazi wazi. Kwa mfano tembo, tembo wameongezeka kutoka 55,000 mwaka 1989, mpaka 100,000 na zaidi hivi sasa. Hii inadhihirisha wakati ule ambapo tunasema kwamba tembo wanangia katika mashamba ya wananchi.

Lakini hata simba nao wameongezeka wengi sana na wanatoka katika hifadhi hizi na kuingia katika maeneo ya wananchi. Kwa hiyo, unaweza kuona kwamba sio sahihi pale ambapo tunasema labda wanyamapori wamepungua, lakini wanyamapori wameongezeka kutokana na ushirikishi wa wananchi katika uhifadhi wa wanyamapori kama nilivyosema.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni suala hili la mapato ya uwindaji. Mheshimiwa Mbunge mmoja ameelezea kwamba mapato ya uwindaji yanaonekana kwamba yamepungua ukilinganisha na mapato ya utalii. Sasa labda niseme kwamba mapato yale ya utalii ambayo tunazungumzia ni mapato ya utalii kwa ujumla wake, sio maduhuli yale ambayo yanakusanywa. Kwa ujumla wake ni kitu gani ambacho utalii kinachangia? Kwa mfano utalii, tokea mtalii anapoingia *airport* anachangia taxi, anapokwenda kwenye hoteli na kadhalika, sio yale maduhuli.

Hasa upande wa wanyamapori, fedha ambazo tunazungumzia ni maduhuli ambayo yanaonyeshwa. Kwa maana hiyo, maduhuli haya upande wa wanyamapori yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka na hivi sasa kwa kweli tunafanya utaratibu

pia wa kuweza kuongeza maduhuli kwa mwaka kesho 2006. Kwa mfano tutafanya utaratibu labda katika maeneo makubwa ya vitalu yatagawanywa kuwa na vitalu zaidi, kwa maana hiyo, fedha zaidi zitaweza kulipiwa, bei pia ya wanyama itaongezwa au imeshaongezwa, halafu pia kudhibiti na kuwaondoa wawindaji haramu jirani na maeneo ya hifadhi. Pamoja na hayo, tunatoa pia motisha ya asilimia 10 ya kiasi cha mali itakayowezesha kukamatwa kufuatia taarifa ya ujangili.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo mtu anatao taarifa ya ujangili, basi anapata asilimia 10. Hata Waandishi wa Habari ambao wanaandika, kwa mfano wanataarifa, basi ni vizuri zile taarifa kama zikipelekwa na zikaonekana ni taarifa zimepatikana sahihi asilimia 10 ya kile ambacho kinapatikana kinapelekwa kwa yule ambaye ni *informer*.

Pamoja na hayo Makampuni ya Uwindaji ya Utalii, pia zitaweza kusaidia shughuli mbalimbali za uwindaji. Kwa hiyo, unaweza kuona kwamba kwanza upande wa wanyamapori, fedha zinaongezeka lakini pamoja na hayo, tunafanya huu utaratibu ambao tunahisi kwamba tutaongeza zaidi. Kwa mfano kitalu hiki sasa kinalipiwa Dola 7,500. Tumeamua kwamba hivi sasa kitalu kimoja kitalipiwa Dola 10,000, kwa maana hiyo, mwaka kesho 2006 tunatarajia kwamba fedha zaidi zitaweza kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia suala lingine ambalo limezungumziwa hapa nalo ni suala la *WMA*. Suala la *Wildlife Management Area*, hapa limezungumzwa kwamba inaonekana kama vile imechukua muda mrefu, inaonekana kwamba suala hili mbona haliendi haraka na kwamba watu wako tayari kuunda *WMA*.

Sasa niseme kwamba *program* hii ya *WMA* ni kuwashirikisha wananchi waweze kusimamia maliasili yao wenyewe kwa maana ya wanyamapori katika maeneo mbalimbali na niseme kwamba kwa *WMA* ya Tanzania ni tofauti kidogo na *WMA* hasa zilizoanzishwa katika maeneo mengine na kuna maeneo ambayo *WMA* zimeanzishwa lakini hazikufanikiwa. Kwa mfano sehemu za Zimbabwe, Botswana na Zambia walianzisha aina ya *WMA* lakini hazikufanikiwa.

Kwa maana hiyo, ilibidi kwa upande wa Tanzania twende kidogo kidogo kama alivyoeleza Mheshimiwa Job Ndugai hapa,kwamba kwa kweli lazima *process* iwe kidogo kidogo ili tusifanye mambo haraka halafu tukakuta kwamba hatukufanikiwa jambo lolote. Kwa hiyo, tunazo *pilot WMA* 16 ambazo hizi sasa kuna mchakato na kila *WMA* lazima ipitie ule mchakato ili mwisho kabisa ikimaliza mchakato huu na ni *step* nane ambazo lazima hatua nane uzipite na baadaye kupita hatua nane zile mwishoni ndipo unakuwa *WMA*.

Kwa mfano ni lazima kupata ardhi na kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya Kijiji. Kwa hiyo, katika ardhi ya Kijiji lazima kupata ardhi na kuweza kuandaa mpango wa matumizi bora. Lazima kuwepo na kutenga eneo kwa ajili ya shughuli za *WMA* katika eneo hili na pia lazima kuanzisha Bodi, baada ya hapo Wilaya hushauri masuala ya maliasili, pia kuanzisha Jumuiya za Jamii (*CBO's)* yaani *Community Based Organizations*, kuandaa Katiba ya Jumuiya ya Jamii, kusajili Jumuiya, kuandaa pia mpango wa jumla wa usimamizi yaani ni jinsi gani ambapo utatumia eneo lile, utatumia

kwa kitu gani, utatumia tu kwa uwindaji au pia pengine utatumia kwa ajili ya utalii na kadhalika.

Baada ya hapo, unatuma maombi ya *AA* yaani *Authorize Association* kwa ajili ya *WMA*. Kwa hiyo, katika hizi 16, tunaweza kusema kwamba ni tatu tu ambazo zimefikia hatua hii ya *AA* na ambazo zitaweza kupata *WMA* kama *Authorize Association,* nyingine bado hazijafikia. Kuna maeneo mengine ambako bado kuna migogoro ya ardhi, kwa mfano maeneo ya Twatwatwa, Wami Mbiki na Loliondo ambako kuna matatizo ya ardhi, kwa hiyo, hapo napo pia huwezi kuanzisha *WMA*.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kusema kwamba sio kama tumesita, lakini ni kwamba tunataka kuhakikisha kwamba hali hii inakwenda vizuri na hii ni jambo ambalo la kuwapa wananchi uwezo wa kusimamia maeneo yao. Hapa lilikuja swali moja la kwamba kuna wananchi ambao walikuwa wanawinda katika *open areas* na hivi sasa hawaruhusiwi kuwinda katika *open areas* hizi na sasa hivi ni kwamba hizi *open areas* nyingine zimebadilishwa kuwa *WMA*.

Mheshimiwa Spika, *WMA* itawasaidia wananchi au wanavijiji wenyewe kwamba wenyewe ndiyo ambao wanasimamia maeneo haya katika uwindaji na hii inawapa nguvu kiuchumi wananchi wenyewe katika Vijiji hivi. Kwa hiyo, wanaweza kuonekana kwamba watu wa Mijini wamekosa kuwinda au wamekosa kuwinda kwa fedha kidogo kwa sababu walizoea kulipa fedha kidogo kwa kulipa mnyama. Sasa *WMA* au maeneo haya ya Kijiji yenyewe yanaamua itakuwa ni kiasi gani kwa uwindaji wa mnyama.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumziwa ni suala la uwindaji. simwoni Mheshimiwa Hashim Saggaf, naona hayupo hapa, lakini alisema kwamba ame-*declare interest* kwamba yeye ni *interested person.* Ni kweli kwa sababu alikuwa ameomba *hunting block* na bahati mbaya hakupata *hunting block*. Kwa hiyo, alivyozungumza *interested person*, nieleze kwamba tumejaribu sana katika masuala haya ya uwindaji na hasa katika *hunting block* hizi, vitalu vya uwindaji kuwa *transparent* kabisa na kutokuficha chochote kile, yaani kuwa wazi kabisa.

Tunakumbuka kwamba miaka mingi iliyopita kulikuwa na Tume ile ya Marmo kwa kuwa kulikuwa na matatizo mengi sana katika *hunting blocks* ikaamuliwa kwamba kuwe na Kamati ya Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji. Kwa hiyo, Kamati ile iliundwa na mmoja wa Wajumbe ni Mbunge. Kwa hiyo, Kamati ile ndiyo ambayo inakaa na kugawa vitalu hivi na kuna utaratibu wa kugawa vitalu pia.

Labda niseme kwamba huku nyuma watu waliokuwa wanaomba vitalu sio wengi sana miaka toka ya 1970s na kadhalika na wengi waliokuwa wameomba vitalu alikuwa watu wa nje. Lakini baada ya hapo vitalu vikawa kama *hot cake* na hivi sasa unakuta kila mtu anakwambia tunaomba kitalu cha uwindaji. Wengi tu! Lakini tunasema kwamba mara nyingi hakuna vitalu vya uwindaji. Tumejaribu kwa kweli katika maeneo mengine kuangalia ni jinsi gani ambavyo tunaweza kupata vitalu vya uwindaji na pale ambapo kwa miaka mitatu iliyopita na nasema kwamba kila kitu tunafanya kwa uwazi kabisa,

hata watu wanaotaka kuja kuangalia utakuta kwamba katika miaka mitatu iliyopita, vitalu vyote ambavyo vilikuwa wazi tulivigawa kwa Watanzania. Hii iko wazi wazi. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, hata makampuni ya uwindaji wa kitalii yameongezeka. Mimi mwenyewe mwaka 1997 nilipokwenda kuhutubia Chama hiki cha Wawindaji, sura nyingi zilikuwa sio za Watanzania na tulisema kuna haja kwa kweli ya kubadilisha jambo hili kwa wale ambao wana uwezo na hili jambo ni muhimu sana. Kwa sababu hatuwezi tukasema kwamba Watanzania kama hawana uwezo, tuwape tu.

Mheshimiwa Spika, ni wale ambao wana uwezo na hivi sasa kuna Kampuni 46 za Watanzania ni 25, za wageni 12 na zile za ubia wa Watanzania na wageni ni tisa. Zote zina jumla ya vitalu 146.

Kwa hiyo, unakuta kwa kweli tumefanya mabadiliko makubwa, lakini tunaelewa kwamba suala hili ni jambo ambalo linahitaji pia mtaji na ndiyo maana tunafanya hii *process*. Kwa mfano, kuna Kamati maalum ambayo ipo na baada ya kuomba kitalu, ni lazima kuangalia uwezo wa mtu alionao. Kwa hiyo, kuna *points* ambazo lazima zijibiwe kwa mfano mtu ana fedha kiasi gani na kadhalika. Baada ya hapo, inakwenda kwenye Kamati ya kugawa vitalu vya uwindaji na baada ya hapo ndipo mtu anapata kitalu cha uwindaji. Lakini napenda kusisitiza kabisa kwamba kama miaka mitatu iliyopita Kampuni zote na tuko wazi kabisa na hata Mheshimiwa Hashim Saggaf namkaribisha kama anataka kuja kuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nisingependa kusema uongo kwenye Bunge hili Tukufu, kuna suala limezungumzwa juu ya Mkomazi, kwamba kuna maombi ambayo yaliletwa kufanywa kuwa Hifadhi ya Taifa na ninapenda kusema kwamba Mheshimiwa Mbunge amelifuatilia sana jambo hili. *TANAPA* pamoja na Wizara imekubali kwamba eneo hili la Mkomazi liwe Hifadhi ya Taifa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kilichofanyika ni kwamba barua imeandikwa kwa uongozi wa Mkoa ili wananchi waweze kukaa katika ngazi za Vijiji na kadhalika walete mapendekezo yao ili baada ya hapo utaratibu ufanywe. Niseme kwamba ni kweli imechelewa lakini imechelewa kwa sababu timu ile ambayo imeshughulika huko kwenye sehemu hii ndiyo timu hiyo hiyo ambayo imeshughulika katika shughuli nyingine za kufanya hifadhi. Kwa mfano Kitulo pamoja na Saadan na kuongeza maeneo ya Kilimanjaro na Meru.

Timu hiyo ndiyo ambayo ilikuwa na kazi hii na kwa maana hiyo haikuweza kufanya kazi kwa wakati huo. Lakini napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa huko kwamba Mbunge wao amefuatilia suala hili kwa karibu sana na kwamba tunatarajia kwamba jambo hili litafanyika kwa upesi iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lililozungumzwa ni kuhusu tozo ya leseni katika upande wa Utalii. Mheshimiwa Philemon Ndesamburo amelizungumzia hili kwamba kungekuwa na tozo moja badala ya kuwa na leseni mbalimbali, anaona kwamba kuna leseni nyingi tu. Kwa hiyo kungekuwa na leseni moja.

Napenda kusema kwamba sheria ya *TALA* hivi sasa ni kweli kwamba hakuna tozo moja, yaani kuna tozo mbalimbali, inategemeana na shughuli ambayo inafanya. Inaanzia leseni Dola 2000 mpaka Dola 200. Lakini hivi sasa napenda kueleza kwamba sheria ya *TALA* nafanyiwa marekebisho ili iweze kupanuliwa zaidi na pia Sheria ya Utalii inafanyiwa marekebisho na kwa maana hiyo itaangalia uwezekanao wa suala hilo litakuwa namna gani.

Suala lingine ambalo lilizungumziwa ni la malipo ya kupanda Mlima Kilimanjaro kwamba pengine mtu kwa sababu hakufika Kilimanjaro juu, basi asilipe fedha zote. Sasa hii haitowezekana kwa sababu, pamoja na suala zima la *rescue fees*, hii haitawezekana kwa sababu mgeni anatarajiwa kwamba angefika kileleni. Kwa hiyo, kwa fedha zile anazotoa ni kwamba atafika, lakini bahati mbaya inakuwa hafiki. Sasa inakuwa vigumu kuweza kumrudishia. Ni kama vile useme kwamba labda umepanda ndege kutoka hapa mpaka London kupitia Dubai, ukafika Dubai ukapata tatizo ukashuka. Sasa pale inakuwa matatizo, umeshakata tiketi labda *straight*. Lakini pamoja hiyo, hata suala la *rescue* nalo pia haitawezekana. Ninaweza kutoa mfano tu wa gari ambalo umeliwekea Bima halafu mwisho wa mwaka halikupata *accident*, sasa ukienda pale kwenye Ofisi za Bima, hawawezi kukurudishia fedha zako. Kwa hiyo, hili kwa kweli litakuwa ni vigumu sana kulifanya.

Suala la Uwanja wa Ndege wa Moshi Mjini pamoja na suala la Uwanja wa Ndege ambao umezungumziwa wa Mafia, nao pia ni kweli ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni tatizo. Lakini mimi binafsi nilizungumza na Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, alisema angejaribu pamoja na Waziri wa Fedha lakini haikuwezekana kwa wakati ule na wakasema kwamba labda wangeanza kutengeneza Uwanja wa Arusha na baada ya hapo waangalie uwezekano wa kutengeneza Uwanja wa Moshi. Kwa hiyo, hilo nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kweli hilo ni tatizo lakini *of course* Watalii wanaingia kwenye Uwanja wa *KIA*.

Suala la Utalii wa Utamaduni Moshi, Mamba, Marangu na Machame, niseme kwamba Wizara inatambua na kuthamini Utalii wa kiutamaduni na katika maeneo ya Moshi, Mamba, Marangu na Machame kwamba kutakuwa na programu maalum kwa ajili ya maeneo hayo.

Uteuzi wa Bodi ya *KINAFA* na *KINAPA*, labda niseme hakuna uteuzi wa Bodi ya *KINAPA,* ni Bodi ile ile ya *TANAPA* ndiyo ambayo inashughulika na hifadhi zote zile. Nasema kwamba tunachukua mawazo ya Mheshimiwa Mbunge na tutayafanyia kazi.

Suala la mkaa nalo pia limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi tu kwamba mkaa unaondoshwa kutoka Tanzania Bara kwenda Visiwani na kadhalika. Niseme kwamba sheria ya misitu hairuhusu kusafirisha mkaa nje ya nchi lakini sheria hiyo hiyo kwa sababu Tanzania ni moja, inaweza kusafirisha kwenda Zanzibar. Tumezungumza na wenzetu wa Zanzibar kuangalia ni jinsi gani tutaweza kushughulikia suala hilo? Tunafanya utaratibu wa kuweka doria kama vile doria ambazo zinawekwa kwa wanyamapori ili kuona ni jinsi gani kwa kushirikiana na wenzetu wa Zanzibar tutaweza kulishughulikia jambo hilo.

Suala la barabara Mjini Moshi, nalo pia niseme kwamba kwa upande wa barabara zile ambazo zinakwenda kwenye bahari, ni kwamba ushirikiano umekua kati ya *TANROADS*, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Halmashauri husika na Wizara ya Ujenzi. Kwa hiyo, labda Mheshimiwa Mbunge napenda kusema kwamba tutashirikiana ili tuone ni jinsi gani ambavyo wote hao watashirikiana. Kama alivyosema kuwa barabara ile pia inakwenda nyumbani kwangu kule Moshi, inapita kwake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala ambalo limezungumzwa kuhusu Wizara kwamba inafanya nini juu ya kuhifadhi eneo la Kihansi. Niseme kwamba vyura wengi ambao wako huko Kihansi ni kweli kabisa kwamba wamekufa kutokana na hali ya *environment* ambayo ilikuwa hapo. Lakini ametoa wazo. Labda kwa kushirikiana na Wizara nyingine husika tutalichukua wazo hili na tuangalie ni jinsi gani ambavyo tunaweza kulishughulikia.

Kuhusu vyura wa Kihansi, hali ilivyo sasa ni kwamba vyura 500 waliotoka Tanzania wamekufa, tunaambiwa wamekufa wote, lakini vyura waliozaliwa wanaendelea vizuri na wanaonyesha wanaongezeka kwa kuzaliana.

Idadi ya vyura huko Marekani imefikia 165 na hapa Tanzania vyura hao hawaonekani huko Kihansi na uchunguzi unaendelea ili kujua hali halisi ikiwa ni pamoja na kuendeleza mipango ya kuboresha na hatimaye kuboresha mazingira ya asili ya vyura wa Kihansi kwa kuruhusu maji ya kutosha kutiririka mtoni kwenye eneo la vyura hao. Kwa hiyo, hili ndilo ambalo naweza kusema kwa sasa juu ya suala zima la vyura.

Kulikuwa na suala la kucheleweshwa kwa ujenzi wa barabara ya Chubi, Itaswi, Kisaki kupitia *TANAPA* na hili ni suala la muda mrefu nalo pia la Mheshimiwa Khalid Suru. Gharama za kujenga barabara hii ni zaidi ya Shilingi milioni 113.

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka Mheshimiwa Khalid Suru mara nyingi sana amekuwa analiuliza suala hili na Mwenyekiti wa *TANAPA* aliyepita, alikwenda sehemu ile pamoja na wataalam wakaona kulikuwa na matatizo ya udongo uliokuwepo pale ulikuwa wa mfinyanzi, kwa vyovyote vile isingewezekana kutengeneza. Kwa hiyo, ilikubaliwa kwamba wabadilishe sehemu ile ya kupita. Sasa ilikuwa Halmashauri ituletee maelezo ni jinsi gani ambapo fedha kiasi gani zinaweza kutosha na hivi juzi tu tarehe 14 Juni, 2005 kwa kweli tumepata barua hiyo kutoka Halmashauri, ni Shilingi milioni 113 na Halmashauri nafikiri ilisema itatoa Shilingi milioni tano kati ya Shilingi milioni 113.

Mheshimiwa Spika, sasa unaweza kuona kwa kweli Shilingi milioni 113 kwa Halmashauri tano ni hela kidogo sana. Kwa hiyo, ningependa kumshauri Mheshimiwa Mbunge kama Halmashauri nao pia kidogo watajisaidia ili waweze kuongeza fedha hizi ili tuone *TANAPA* nao pia watasaidia kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la Mambo ya Kale ambalo lilizungumziwa juu ya mabaki ya vitu vile ambavyo viko Kenya na ilielezwa kwamba vifanyiwe utaratibu virejeshwe Tanzania. Masalia ya utamaduni ambayo yako Kenya pamoja na taarifa ya

kumbukumbu ya mambo ya kale na kwamba hazitambuliki sehemu nyingi na hasa zile za Mafia, Ujiji na Bagamoyo, pia Wizara iweke mkakati wa kuwa na wataalam wa Mambo ya Kale wa kutosha na iboreshe mazingira ya kazi na vitendea kazi.

Napenda kusema kwamba sote tungelipenda vitu hivi virudishwe Tanzania na hivi sasa tunapata kama asilimia 20 ya mapato yale ambayo yanapatikana kwa wale ambao wanatembelea sehemu hii. Lakini ili kuweza kurudisha hapa, basi lazima uwe na mazingira ambayo yatawezesha vitu hivyo kuweza kufika hapa. Isije ikawa vinafika vitu hivyo, halafu vinakaa kwenye ma-*box* tu.

Kwa hivi sasa tunaweza kusema kwamba bado hatujawa na uwezo wa kutosha wa kuweza kuvileta vitu hivi hapa nchini. Tunajaribu kujenga uwezo wa kutosha ili kuweza kuvileta. *Meanwhile* vitu hivi bado viko Kenya na sisi pamoja na Kenya tunashirikiana kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ile ya Mtaalam kutoka Chuo Kikuu ambaye angeweza kwenda Vituo mbalimbali vya Ujiji na kadhalika, ninaweza kusema kwamba mtumishi kutoka Chuo Kikuu kwenda Kituo cha Ujiji, mpaka sasa hivi Kituo hicho kipo chini ya usimamizi wa Mkoa na taratibu zinaandaliwa ili sasa Kituo hicho kikabidhiwe kwa Wizara. Kwa hiyo, Vituo hivi sasa viko chini ya Mkoa na tunafanya utaratibu ili vihamishiwe Wizarani.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mazungumzo kuhusu Bajeti ya *TTB* kwamba ni finyu na inabidi iongezwe. Ningependa kusema kwamba suala la ufinyu wa *TTB* kwa kweli tunalitambua na ni kweli kwamba ni fedha ndogo, lakini hata hivyo kufuatana na uwezo wa Serikali imekuwa ikiongeza Bajeti mwaka hadi mwaka kama ifuatavyo:- Kwa mfano mwaka 2001 milioni 1.1, mwaka 2001/2002 milioni 1.3, mwaka 2002/2003 milioni 1.4, mwaka 2003/2004 milioni 1.5, mwaka 2004/2005 milioni 1.6 na mwaka 2005/2006 milioni 2.8.

Kwa hiyo, unaweza kuona kwamba kwa kweli pamoja na kwamba Bajeti ni ndogo, lakini Bajeti hii imekuwa inakua. Aidha, mkakati mpya ambao unaandaliwa utabaini maeneo mapya ya kuziongezea Bodi uwezo wa kifedha kwa ajili ya shughuli za utangazaji. Vile vile, Mashirika na Taasisi za Sekta binafsi, kusaidia shughuli hii ya utangazaji.

Kuhusu suala la Thailand kuwa na *Sex Tourism* ambalo limeelezwa hapa, napenda kusema kwamba kwanza, suala la *Sex Tourism* linapigwa vita sana na *World Tourism Organization*. Utalii una *ethics* zake na *ethic* mojawapo ni hiyo *Sex Tourism* na *ethic* nyingine ni kuwatumia watoto wadogo sana wa kike na wa kiume. Kwa hiyo, kwanza niseme kwamba na mimi bahati nzuri nimefika Thailand, kwanza hakuna *brochure* yoyote ile ambayo inatangaza *Sex Tourism* katika Utalii wa Thailand. Huo ni utalii ambao kwa kweli unapigwa vita duniani kote. Sasa labda Mheshimiwa Mbunge anazungumzia *Sex Tourism* iliyotangazwa miaka 40 iliyopita. Lakini kwa kweli ni jambo ambalo lazima hata Tanzania tulipige vita kwa nguvu zetu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwamba mapato yetu hayalingani na thamani ya *assets* zetu, napenda kusema na siku zote nimekuwa nasema hapa kwamba utalii wetu ni *low volume high yield* na ndiyo maana tunataka hata wawekezaji wawekeze katika hoteli za hali ya juu ili watalii wanapokuja waweze kulipa fedha zaidi. Ndiyo maana tumesisitiza hata Chuo cha Utalii hapa ili kuwafunza vijana wetu. Kwa hiyo, sisi tunajali utalii wa mazingira, watalii wachache, lakini ambao wanatumia fedha zaidi na mazingira yetu yanakuwa mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano ningependa kusema kwamba, Kenya mwaka 2002 ilipata watalii milioni moja, lakini kimapato walipata Dola milioni 297 tu. Sisi hatujafikia kupata watalii hao milioni moja. Aidha, Uganda, kwa kweli hizi *figures* ambazo Mheshimiwa Mbunge alizipata, labda alikosea katika kuzinakili. Sio kweli kwamba wanapata zaidi ya watalii laki tano. Kwa sasa Uganda hupata watalii 254,000 na mapato ya Dola za Kimarekani 185 milioni tu. Tunakuwa na Mikutano hii ya Afrika Mashariki, kwa hiyo, *figure* hizi zote tunazielewa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limezungumziwa kwamba hatujaamka kiutalii, napenda kukataa katakata, kabisa. Tunaweza kusema kwamba kuna mabadiliko makubwa sana na hata Mheshimiwa Ndesamburo ambaye ni Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii naye anaona kwamba Serikali hii imefanya kazi kubwa sana katika Sekta hii ya Utalii. Kwa hiyo, tusijiweke nyuma tukasema hatujaamka! Tumeamka, tena tumeamka siku nyingi sana na tuko *aggressive* sana kwa wakati huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba, labda Mheshimiwa Mbunge anazungumzia miaka kama 16 iliyopita, amesema alikuwa London, lakini kwa hivi sasa matangazo ni mengi na ndiyo maana nikasema hata idadi ya watalii inaongezeka kila mwaka. Tanzania inabuni aina mbalimbali za kuvutia utalii, kwa mfano kuna utalii wa utamaduni ambao sasa kuna maeneo 24 ya utalii wa aina hii na ni mojawapo ya ubunifu.

Aidha, utalii wa majini upo hatua za mwanzo, huko Zanzibar kuna *Spice Tours*, kuna Kilwa, kuna mambo mengi sana ambayo kwa sasa hivi tunaweza kusema kwamba yamefanyika. Hata masoko ya utalii, masoko yake ambayo ni *tradition* nayo pia tunaendelea nayo, lakini kuna masoko mapya. Masoko ya zamani yalikuwa Ujerumani, Uingereza na Ufaransa na hivi sasa kuna masoko mapya ya Japan, kwa mfano masoko ya China na kadhalika. *Of course* tunasema bado *challenges* zipo na ndiyo maana kazi bado inafanyika na kufuata *master plan* mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni juu ya lugha ambalo limezungumziwa kwamba kuna haja ya kuanzisha *center* kwa wahudumu wanaohudumia watalii ili kujifunza lugha za kigeni kama vile Kiingereza na Kifaransa. Napenda kusema kwamba, upo mpango wa kuandaa mtaala *(curriculum)* wa Kitaifa kwa ajili ya Vyuo vyote vya Hoteli na Utalii. Hii ni mojawapo ya mikakati ya kudhibiti Vyuo ili viweze kutoa mafunzo bora.

Lugha ni somo la lazima katika mafunzo na Chuo chetu kipya cha Utalii kinachojengwa. Chuo hicho kitakuwa na Maabara ya Lugha kwa ajili ya kufundisha lugha mbalimbali za kigeni. Chuo kitatoa wahitimu 500 kwa mwaka katika fani mbalimbali. Kwa hiyo, tunaweza kuona kwamba suala la lugha nalo tunalitilia mkazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kugusia juu ya uimarishaji wa Vituo vya Mambo ya Kale. Naweza kusema kwamba huu ni msisitizo ambao tunauweka sasa katika Wizara yetu. Ni kweli kabisa kwamba imechukua muda sasa, lakini ni kwa sababu mambo ya kale yalikuwa Wizara ya Elimu na Utamaduni kabla ya kuja Wizarani kwetu. Kwa hiyo, hivi sasa tunaweza kusema kwamba uimarishaji mkubwa zaidi unakuwepo katika Vituo hivyo. Vituo hivyo vimeendelea kuboreshwa kutoka mwaka 1999 Idara hii ilipohamishiwa Wizarani na baadhi ya Vituo vinajengwa *(information centers)* vikiwemo vya Olduvai, Kalenga na kadhalika na pia kujenga Ofisi kwa ajili ya Watendaji wanaohudumia Vituo hivyo.

Lakini pia kumekuwepo na ongezeko kubwa la wataalam wa mambo ya kale kwa kuongeza wataalam 19 kutoka mmoja mwenye digrii ya Chuo Kikuu. Kuongezeka kwa ushirikiano pia kati ya Idara na Mashirika na nchi Wahisani kwa mfano Sweden, France, *UNESCO*, Finland na nyinginezo na hii inatokana na imani waliyojenga Wahisani baada ya Idara kuwa chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, suala la uvuvi nalo limezungumziwa kuhusu kuongeza doria. Napenda kusema kwamba, Wizara hivi sasa ina jumla ya boti tisa zinazosaidia doria kwenye maeneo ya Pwani ya Bahari ya Hindi na kwenye maziwa yetu hapa nchini na Wizara pia imeagiza boti mpya tisa kama ifuatavyo:- Boti mbili kubwa za mita 12 na boti saba za wastani. Boti hizi zitasaidia kuimarisha doria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa *MANCEP* ni muhimu sana, pamoja na kusaidia wavuvi wadogo wadogo katika kuwakwamua kwenye umaskini kupitia MKUKUTA, lakini pia utaweza kutoa mikopo kwa wavuvi hao wadogo wadogo. Vile vile, mradi huu utasaidia maeneo mengine yale ambayo Mheshimiwa Abdulkarim ameyataja na unatarajia pia kununua chombo kikubwa kusaidia doria kwenye maziwa makuu ya *EEZ (Exclusive Economic Zone).* Chombo hicho pia kitasaidia kudhibiti uvuvi haramu na wizi wa raslimali zetu unaofanywa na meli za nje kwenye ukanda wa *EEZ*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama vile katika Sekta nyingine za Wanyamapori na kadhalika, ushirikishaji wa wananchi nao pia unatiliwa mkazo katika upande wa uvuvi na unakuta kwamba kwa sababu ya kushirikiana na wananchi, uvuvi haramu umepungua kwa sehemu kubwa sana. Unakuta katika maeneo haya mbalimbali kwa mfano makokoro, sehemu kubwa sana wananchi wenyewe wanapiga marufuku na hata matumizi ya ndoano kwa uvuvi. Hivi sasa hata akina mama wanavua kwa ndoano kwa sababu ni rahisi sana kuweza kupata samaki katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, suala la misitu nalo pia limezungumzwa hapa kwamba misitu inakatwa. Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba, tulipiga marufuku usafirishaji

wa magogo nchi za nje, lakini pamoja na hayo hivi sasa tumefanya *inventory* ili kuweza kujua misitu au miti aina gani na mingapi ambayo tunayo katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, tathmini ya raslimali ya misitu *(inventory)* ambayo imefanyika katika Wilaya 11 zenye misitu ya uvunaji imekamilika na Wizara inaendelea na uchambuzi wa tathmini hiyo.

Mpango wa uvunaji wa Wilaya nne umekamilika, Wilaya hizo ni Mvomero, Kilombero, Ulanga, Kisarawe na Mkuranga. Uchambuzi wa takwimu za Wilaya za Mpanda, Handeni, Kilindi, Liwale, Kilwa, Rufiji, Tunduru na Nachingwea utakamilika nafikiri itakapofika wiki ijayo. Mpango mzima wa uvunaji unatarajiwa kukamilika Agosti, 2005 ili kuwezesha kufunguliwa kwa uvunaji katika misitu ya asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala hili limesaidia sana kuweza kujua miti yetu iko wapi, ni ya aina gani na kuweka pia utaratibu maalum wa kutoa vibali kwa ajili ya misitu, lakini pia kutia hamasa wale watu ambao wanataka kuwekeza viwanda katika nchi yetu ili kuongeza thamani ya miti yetu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, yako mengi, lakini labda niseme kwamba kwa kuwa huu ni Mkutano wa 20 wa Bunge hili na ni mwisho katika maisha ya Bunge hili, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano ambao walinipa katika kipindi hiki chote. Hata sifa hizi walizonipa kwa kweli ni sifa zetu pamoja kwa sababu nyie mmechangia kwangu mimi, Wizara na Watendaji wote kufanikisha yale ambayo tunayafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba, kwa wale watakaogombea tena, ninawatakia kila la kheri na wale ambao hawatagombea ninawatakia kila la kheri katika maisha yao nje ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kukushukuru wewe na kukupongeza kwa jinsi ulivyoongoza Bunge hili kwa umakini mkubwa sana. Nawashukuru pia Naibu Spika na Wenyeviti na kuwatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati kama huu nilieleza kuwa ilikuwa mara yangu ya kwanza katika maisha yangu ya kisiasa kusoma hotuba ya Bajeti bila ya mume wangu Profesa Meghji kuwepo duniani. Leo hii napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru watoto wangu Nyangu, Mahir, Jamila, Salama na Duli kwa upendo na mshikamano wao walionipa ambao ulinipa nguvu na uwezo wa kutekeleza majukumu yangu kama Waziri na kama mama. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, namshukuru sana dada yangu Rabia Hamdani, yuko pale ambaye amesafiri kutoka Zanzibar na yuko kwenye *gallery* hii. Nasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kuna jambo dogo la utaratibu naona ni vyema nilifafanue. Wenzangu wanaonisaidia kuongoza Vikao hivi kipindi cha mchana nimesikia baadhi yao katika vipaza sauti vya Ofisini kwangu inapofikia hatua hii wanawahoji Wabunge kwamba wanaoafiki waseme ndiyo, wasioafiki waseme siyo. Lakini siyo sahihi. Hoja ni kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii. Mchakato unakuwa bado unaendelea, hoja ya kupitisha makadirio inakuja baada ya Kamati ya Matumizi.

Nadhani hii inachanganywa na utaratibu wa kupitisha Miswada, kwa sababu katika Miswada kabla ya kwenda kwenye Kamati huwa tunawahoji kwa sababu hoja inasema: "Muswada huu sasa usomwe mara ya pili." Hiyo ni lazima iamuliwe kabla hatujakwenda kwenye hatua inayofuata. Lakini kwa kupitisha Bajeti, hakuna hatua ya katikati, tunangoja mpaka mwisho wa Kamati ya Matumizi imeshamaliza ndiyo tunawahoji kuwa na uhakika kwamba Bunge linapitisha makadirio haya. Kwa hiyo, sasa hivi sitawahoji, naomba Katibu tuendelee na hatua inayofuata.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii

Kifungu 1001 – *Administration and General* ... ... ... Sh.1,705,762,200/=

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwenye kifungu hiki cha 1001, *program* hiyo ya 10…

**MWENYEKITI:** Kwa kuwa kifungu kimeshatajwa na Katibu, huna haja ya kukirudia, wewe toa mchango wako.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Sawa. Kifungu kidogo cha 250100, sina haja ya kushika mshahara wa Waziri, lakini katika mchango wangu wa maandishi nimezungumzia matatizo au kero tatu kwenye Hifadhi ya Lukwika – Lumesule.

La kwanza, ni juu ya mipaka kubadilika badilika. Wananchi wanadai kuwa mipaka ya hifadhi hiyo huwa inabadilikabadilika kulingana na Afisa anayekuja pale. Sasa cha ajabu ni kwamba, kila inapobadilika wananchi hawalipwi fidia ya mazao yao. Kwa hiyo, ningeomba maelezo kutoka kwa Waziri ni kwa nini kwanza mipaka inabadilikabadilika? Lakini vile vile ni kwa nini wananchi hawalipwi fidia pale ambapo mipaka inabadilika?

La pili, kuna wananchi kadhaa hasa katika Kijiji cha Mpombe ambao hadi leo bado wanadai fidia. Uongozi wa Hifadhi Wilayani unadai kuwa wananchi wote walikwishalipwa fidia. Lakini wananchi na Serikali zao za Vijiji bado wanasisitiza kuwa fidia iliyolipwa ilikuwa haitoshelezi, ina maana kuwa imepungua. Sasa, hili nimekuwa

ninalipigia kelele kwa miaka kadhaa sasa, lakini suala hili inaonekana bado halijatatuliwa. Kwa hiyo, naomba maelezo ya Waziri juu ya utaratibu ambao utaondoa kero hiyo. Ni hayo tu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Aridi Uledi juu ya kubadilika mipaka katika pori la akiba la Lukwika – Lumesule. Amesema kwamba, mpaka umekuwa ukibadilishwa mara kwa mara kinyume cha taratibu bila kuwashirikisha wananchi wa maeneo hayo. Napenda kusema kwamba, mara nyingine inatokea mipaka inakuwa haikufyekwa kwa muda mrefu na pale ambapo imefyekwa, basi wananchi mara nyingine wanaona kwamba eneo lao limechukuliwa. Lakini mipaka ya pori siku zote inazingatia tafsiri iliyopo katika sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunashirikiana vizuri na Waheshimiwa Wabunge pale ambapo kwa kweli kumetokea matatizo halisi. Hata mimi mwenyewe nilishawahi kufika katika maeneo mengine na kuangalia kama kuna matatizo ya mpaka. Kwa hiyo, mpaka kufyekwa, suala muhimu ni kwamba tafsiri ya sheria iko namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la fidia ya Kijiji cha Mpombe, napenda kusema kwamba fidia hizi zina utaratibu pale ambapo Wanavijiji wanakaa wanapitisha kwenye Kikao mapendekezo yao, yanakwenda katika ngazi ya Wilaya, Mkoa halafu yanakuja katika ngazi ya Wizara. Sasa, sidhani kama jambo hili limefika kwetu.

*(Hapa Mheshimiwa Uledi Alisimama Akitaka Kuuliza Swali)*

**MWENYEKITI:** Aah, si uliishauliza Mheshimiwa Uledi, sasa tena! Wape nafasi na wenzako. Unapouliza uliza yote, usiweke akiba.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nimpongeze Mheshimiwa Waziri. Kwa kweli kati ya watu wanaoni-*impress* ni mama huyu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mama gani unayemzungumzia?

**MWENYEKITI:** Ni Mheshimiwa Waziri, siyo mama.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Wakati mwingine Mheshimiwa Waziri huyu huwa namwona kama *iron lady*. Kwa hiyo, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza kwamba kumekuwepo na *production* kubwa kwa upande wa uvuvi na kumekuwepo na viwanda vingi katika Mji wa Mwanza na hivi sasa Bukoba kuna viwanda Kemondo na kiasi cha minofu ya samaki inayosafirishwa kimekuwa kikubwa. Lakini katika mchango wangu wa maandishi nilimweleza Mheshimiwa Waziri kwamba, kwa kweli pamoja na mafanikio hayo kwa wananchi wa Bukoba, wananchi wa Kagera kwa ujumla na wananchi wa Mkoa wa Mwanza hata Musoma - Mara, ni kwamba kumekuwa na tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa na viwanda hivi na kusafirisha minofu kwa wingi, lakini inaonekana mlipuko huu umewasahau watu wetu kwa lishe ya samaki. Inaonekama mtazamo wa Wizara hii imekuwa ni kuangalia lishe ya Wazungu kwanza na kusahau lishe ya watu wetu na nikawa nimemweleza Mheshimiwa Waziri kwamba, kwa kweli inabidi Wizara kama chombo ambacho kinasimamia shughuli hii kwa niaba ya Serikali, kiangalie ni namna gani kinaweza kuweka utaratibu wa kuwasaidia watu wetu ili waweze kula samaki wala siyo vichwa vya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa watu wa Miji hii kwa sababu samaki wamepanda bei, kwa kuwa wanasafirishwa kwa wingi, wamekuwa wanakula vichwa vya samaki maarufu kama panki. Watu samaki wanawasikia tu! Ziwa ambalo limekuwepo kwa miaka mingi kama sehemu ya uchumi wao, kama sehemu ya kupata lishe bora ya samaki wanaliona tu lipo pale kwa nia ya kuwalisha Wazungu. Ndiyo maana huwa ninapongeza kaulimbiu ya mtu mmoja alikuwa anagombea nafasi ya Urais kupitia Chama fulani kwamba Kiatu kwanza, benzi baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini katika hili kwa kweli lishe ya watu wetu iwekwe kwanza, ipewe kipaumbele na lishe ya Wazungu ije baadaye. Mheshimiwa Waziri nimempa maoni yangu mbalimbali ni namna gani ya kufanya jambo hili na kama atakuwa tayari tuendelee na mchakato wa kuyajadili hata kama siyo humu ndani kutokana na muda, lakini kwa kweli suala la kuwafanya watu wetu kula vichwa vya samaki naomba lifikie mwisho na Serikali ionekane inajali watu wake kuliko Wazungu ambao tunaangalia pesa zaidi kuliko lishe ya watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru kwanza Mheshimiwa Lwakatare kwa kunipongeza. Nilifikiria haulizi swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la samaki, nafikiri tunakumbuka wakati ule ambapo tulifungiwa kusafirisha samaki nje, hali ya wananchi ilikuwa mbaya sana. Niseme kwamba ni aina moja tu ya samaki ambao wanasafirishwa nje, ni aina ya sangara. Kuna aina nyingi sana za samaki kule *Lake Victoria* ambazo wananchi wanaweza kula. *(Makofi)*

Lakini pia Serikali ilifanya utaratibu wa makusudi kwamba uvuaji wa samaki huu usifanywe na wenye viwanda, ufanywe na wananchi wenyewe. Kwa hiyo, wananchi wenyewe ndiyo ambao wanavua, wanapeleka na kuamua bei kwa pamoja na baadaye fedha hizi zinatumika kwa ajili ya maendeleo ya wananchi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri sio sahihi kusema kwamba wananchi wanakula vichwa vya samaki tu, kwani kuna aina mbalimbali za samaki na ni samaki aina ya sangara peke yake ambao wanasafirishwa nchi za nje. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimesimama hapa kumpongeza Mheshimiwa Lwakatare kwa kumpongeza Waziri kwa kazi nzuri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilishauri Wizara kwamba ikiwezekana iamue kuzuia ukataji wa baadhi ya miti ambayo ni nadra kupatikana na iko katika hatari ya kupotea kwa sababu ya watu wetu kutothamini miti katika nchi hii. Kwa mfano, pale Dar es Salaam nyuma ya Makumbusho kulikuwa na mti ambao umeishi zaidi ya miaka 2000 na wenye ukubwa ambao watu watano mnaweza mkazunguza na msikutane, lakini wajenzi wa nyumba bila kujali thamani ya miti na uzuri wa mti huu wameuharibu, wameukata. Sasa, kuna miti mizuri hata katika Mkoa huu, kwa mfano mibuyu ambayo ni mikubwa sana na tusipoangalia baadaye kwa sababu wanatengeneza viti vya kukalia vidogo vidogo vya asili, miti yote katika nchi hii itapotea. Napendekeza kwamba tuwe na kitu kama *National Tree,* tukatambua baadhi ya miti hii kuzuia kabisa isikatwe kama tulivyozuia mnyama kama twiga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya *South Africa* ina *National Flower* na twiga nadhani haruhusiwi kuuawa. Kwa hiyo, mti kama mbuyu na miti mingine ya aina hiyo ambayo iko kwenye hatari ya kupotea tungezuia isikatwe kusudi vizazi vijavyo viweze kuelewa thamani yake. Hata pale Dar es Salaam karibu na Kanisa la *Saint Peters*, wenzetu wakati wanajenga barabara bado waliepuka wakauacha ule mti, lakini Waswahili wanakata tu. Mfano Njombe pale kwenye Mji wa Makambako, ule ulikuwa ni mti. Mkambako ni mti. Leo mti ule haupo, lakini tumebaki na jina tu. Napendekeza Waziri aone umuhimu huo na ikiwezekana alete sheria ya kuzuia baadhi ya miti isitoweke. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Misitu ya mwaka 2002 inatamka wazi kwamba, huwezi kukata miti bila kupata kibali cha Afisa Misitu. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni kweli kuna baadhi ya maeneo ambayo kuna miti ambayo imekuwepo kwa miaka mingi sana, lakini inakatwa. Kwa hiyo, tunapokea ushauri wake na utafanyiwa kazi kwa kuangalia sheria inavyosema. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu 69, *program* ya 10, *sub-vote* 1001, kifungu kidogo 250100. Wakati nikichangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri niliongelea suala la ujenzi wa bwawa la Chato ambalo Wizara ilitutaka tupeleke makisio yake na sisi tuchangie na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ichangie. Sasa, michango ile ilishapatikana, ningependa kufahamu kwamba: Je, Wizara imetenga kiasi gani kwa ajili ya ujenzi wa bwawa lile?

La pili linahusu kile Kituo cha Misitu cha *JICA* pale Same. Kuna baadhi ya mali za kile Chuo zimehamishwa kama vile basi pamoja na eskeveta moja. Je, ni kwa nini vimehamishwa na kama vilihamishwa kwa muda vitarudishwa lini?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli suala hili la bwawa la Chato Mheshimiwa Mbunge amelifuatilia sana na ninapenda kuwahakikishia hata Wapigakura wake kwamba amelifuatilia sana suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewasiliana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ambayo ndio mhusika mkuu na Wizara imesema itatoa fedha kiasi kadhaa, lakini sasa inaonekana fedha ambazo Wizara ya Maliasili na Utalii itabeba ni nyingi. Suala hili leo tumelizungumza pamoja na wenzetu wa *TANAPA*. Kwa hiyo, ningependa labda baada ya Kikao hiki pengine tungeweza kuangalia ni jinsi gani ambavyo Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo itaongeza fedha ambazo ingesaidia katika bwawa hili halafu tuangalie *TANAPA* itaweza kusaidia kiasi gani pamoja na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kituo hiki cha Same, pia ni Kituo ambacho ni cha Wizara. Labda niseme kwamba, eskeveta iko Same na basi liko kwenye Chuo chetu cha Olmotonyi, kwa sababu ni Chuo ambacho kinashirikiana katika shughuli za uelimishaji pamoja na Kituo hiki cha Same.

Kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, eskeveta iko pale pale Same, labda tu aulizie iko wapi, lakini kama hajui iko mahali gani tutamwelekeza.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts* ... ... ... TShs. 879,955,200/=
Kifungu 1003– *Policy and Planning*… … … … Tshs 604,406,300/=
Kifungu 2001 – *Wildlife* … … … … … … … … Tshs 8,332,895,200/=
Kifungu 3001 – *Forestry and Beekeeping*… … …Tshs 9,627, 075,200/=
Kifungu 3002 – *Fisheries* ... … … … … … … Tshs 6,663,504,000/=
Kifungu 4001 – *Tourism* … … … … … … … … Tshs 3,916,744,900/=
Kifungu 4002 –*Antiquities Unit* … … … … … …Tshs 1,239,981,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU LA 69 – WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

Kifungu 1001 – *Administration and General*… … Tshs 200,000,000/=
Kifungu 1003 – *Policy and Planning* … … … … …Tshs 3,025,000,000/=
Kifungu 2001- *Wildlife* … … … … … … … … Tshs 3,053,823,200/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 – *Forestry and Bee Keeping* … … … Tshs 7,251,112,500/=

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, mimi nimeona niulizie hapa kwa sababu kwa kweli sihitaji kushika Shilingi. Hili ni eneo la maendeleo.

Nilipokuwa nimechangia nilizungumzia kifungu 3001, kifungu kidogo 46(29) kuhusu *Support for Forestry* halafu na kifungu 46(30) *Forestry Conservation Management*. Nilizungumzia mambo mawili. Nilizungumzia suala la ukataji wa miti katika chanzo cha maji ya Kwembago na hili niliuliza hapa kwenye swali.

Halafu ombi la upandaji wa miti, sasa kwa sababu eneo hili linahusu mambo ya *Forestry,* nafikiri Waziri angenihakikishia ili niwaambie wananchi wa Lushoto kwamba hela zimetengwa, zipo kwenye fungu hili na mambo yatakuwa mazuri. Ahsante sana.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *Support to Forestry College SADC region,* kwa hiyo, hii haitahusiana na lile ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliulizia.

Lakini kuna *program* ile ya *Tanzania Forestry Program, (TFNP)* ambayo ndiyo inahusika na *program* hizi za *Forestry.* Kwa hiyo, labda pengine fedha hizo zitakuwa kwa upande huo wa *TFNP*.

**MWENYEKITI:** Amesema fedha zipo, siyo katika kifungu hiki, kwa hiyo fedha hizo za kifungu 3001 zinaidhinishwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3002 – *Fisheries* … … … … … … … Tshs 4,586,205,500/=
Kifungu 4001 – *Tourism* … … … … … … … … Tshs 2,554,710,300/=
Kifungu 4002 – *Antiquities Unit* … … … … … … Tshs 1,800,988,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote )*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imepitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2005/2006 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka 2005/2006 yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 12.30 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne tarehe 19 Julai, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*